

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Tisa – Tarehe 8 Februari, 2013

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA:

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha, Mapitio ya Nusu Mwaka Februari, 2013 (*Monetary Policy Statement – The Mid Year Review February, 2013*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla sijawasilisha mezani taarifa niliyo nayo, naomba nitoe salaam za rambirambi na pole kwa waumini wote wa Kanisala Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Kati pamoja na familia ya Baba Askofu Thomas Laizer, kwa kifo kilichotokea jana cha Askofu wa Dayosisi hiyo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze Roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salaam hizo, sasa naomba kwa niaba ya Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwasilisha mezani.

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 (*The Annual Report and Audited Accounts of the National Housing Corporation (NHC) Year ended 30th June, 2011*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri na tumepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo hicho cha Askofu. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nimemwona Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kuwasilisha mezani.

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa Mwaka 2010/2011 (*The Annual Report and Audited Accounts of Tanzania Education Authority for the Year 2010/2011*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha!

MASWALI NA MAJIBU

Na. 107

Biashara ya Dawa za Kulevya

MHE. KIDAWA HAMID SALEH aliuliza:-

Ulimwengu mzima pamoja na Tanzania umekumbwa na janga kubwa la usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

(a) Je, ni nchi zipi zinazoongoza kwa kufanya biashara hii mbaya?

(b) Je, ni wanawake wangapi wa Kitanzania wamekamatwa katika nchi mbalimbali na hapa nchini kwa kufanya biashara hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa za kulevya zinazozalishwa na kutumiwa kwa wingi duniani ni Bangi ikifuatiwa na *Heroin* na *Cocaine*. Nchi zinazoongoza kwa kufanya biashara ya dawa hizi ni kama ifuatavyo:-

- Bangi – Marekani;
- *Heroin* – Afghanistan; na
- *Cocaine* - Brazil.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 2010 hadi 2012 jumla ya wanawake wa Kitanzania 17 walikamatwa wakijihuisha na biashara haramu ya dawa za kulevyta. Kati yao wanawake 14 walikamatwa hapa nchini na watatu walikamatwa Brazil.

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa, katika Bunge la Bajeti liliopita tulielezwa kuwa kuna mkakati wa pamoja wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki za kupambana na tatizo hili. Je, ni nini mafanikio ya utekelezaji wa mkakati huo?

(ii) Naomba Serikali ikawaeleza Watanzania ni nchi zipo ambazo zimeweka adhabu ya kifo katika nchi zao wakati wanapowakamata wahalifu wa aina hi?'

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:-

Wakati wa Bajeti tulisisitiza tukasema kwamba Serikali imeunda kikosi maalum yaani *Task Force* ndani ya nchi ambacho kinajumuisha idara mbalimbali za Ulinzi na Usalama ambazo ndiyo zimeweka nguvu mpya katika udhibiti wa dawa za kulevyta na ndiyo maana utakuta baada ya kuweka kikosi hicho ukamataji umekuwa wa nguvu sana na umekuwa mkubwa sana ukilinganisha na miaka ya nyuma.

Kwa mfano, mwaka 2011 kiasi cha Bangi kilichokamatwa ni tani 17,000 na mwaka 2012 kilo 48,000 ukilinganisha na miaka ya nyuma kama mwaka 2010 ambapo ilikuwa 4,000 na hii ni kwa sababu ya ushirikiano uliowekwa pamoja na kikosi hiki maalum cha *Task Force*.

Hata *Heroine* mwaka 2011 baadaya kuanzisha kikosi hiki cha kupambana na madawa ya kulevyia kinaunganisha nguvu kubwa, kilo 2,655 zilikamatwa mwaka 2011 ukilinganisha na miaka ya nyuma kama mwaka 2008 ambapo kilo tatu tu zilikamatwa wakati kila idara ikifanya kivyake. Kwa hiyo, hapa nilichosema ni kwamba nguvu kubwa imewekwa ndani ya nchi kwa ushirikiano mkubwa wa pamoja ambao Mheshimiwa Rais aliagiza kwa kuundwa kikosi maalum ambacho kitakuwa na washiriki katika vikosi vyote na sehemu zote za ulinzi na usalama.

Lakini kama ulivyosema tuna ushirikiano wa pamoja wa *East Africa* ambao unatumika katika kupashana habari na kuangalia biashara hii inavyofanywa hasa sehemu za mipaka ambao umeleta mafanikio katika siku hizi za karibuni.

Kuhusu swalii la pili la kwamba ni nchi gani inatoa adhabu ya kifo. Naomba niseme kwa sasa jibu hilo sina lakini najua zipo nchi kama China, nchi hiyo jambo kama hili ni moja kwa moja unakwenda. Hiyo nina uhakika nayo! Lakini vile vile na baadhi ya nchi za Kiarabu kama Saudi Arabia. Sasa ukitaka niorodheshe zaidi ya hizo nipe muda, lakini najua angalau nchi hizo zinatoa adhabu ya kifo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swalii linalofuata sijaona tena mtu aliyesimama. Kwa hiyo, tutaendelea na swalii linalofuata ingawa nilikuwa nimemwona Mheshimiwa Richard Ndassa, sasa sioni kama anasimama tena. Mheshimiwa Richard Ndassa, utaratibu ni kwamba lazima usimame kwa mujibu wa Kanuni na jicho la Spika likuone, lakini ukikaa hawezizua kama unataka kuzungumza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa jicho lako kuniona.

Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba mbali na Mkoa wa Iringa unaojulikana kwa ulimaji wa Bangi ambao wanasema kwamba wao ni mboga kwao, ni mkoa gani mwagine unaoongoza kwa kulima Bangi? (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, lakini sijui umeuliza swali hilo kwa sababu wewe unatoka Mkoa wa Iringa, lakini tunaomba Waziri ajibu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kumjibu Mheshimiwa Richard Ndassa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Sijui kama ana mfano wa watu wanaofanana na Bangi watu wa Iringa huyu, lakini Iringa siyo Mkoa unaoongoza kwa kulima Bangi katika nchi hii. Mkoa wa Iringa siyo unaoongoza, Mkoa unaoongoza ni Mkoa wa Mara. Kwa hiyo, huo ndiyo Mkoa unaoongoza na hata ukiniambia nitoe takwimu hapa za Bangi tulioiteketeka na kuikamata kwa kiasi kikubwa ni Mkoa huo wanaotoka akina Mheshimiwa Vincent Nyerere yaani Mkoa wa Mara. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, nadhani tutahitaji kujua hiyo taarifa rasmi ya hiyo mikoa inayoongoza ili tujiridhishe vizuri ndani ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata na linakwenda Ofisi ya Waziri Mkuu na litaulizwa na Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mbunge wa Viti Maalum.

Utegemezi wa Wawekezaji Kutoka Nje

MHE. AMINA ABDULLA AMOUR aliuliza:-

Dhana ya kutegemea Wawekezaji kutoka Nje ni dhana potofu:-

- (a) Je, Serikali inasemaje kuhusu dhana hiyo?
- (b) Je, Serikali itaacha lini kutegemea Wawekezaji kutoka nje?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kutegemea wawekezaji kutoka nje siyo dhana potofu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mafanikio ya kiuchumi ya nchi nyingi zilizoendelea na zinazoendelea duniani yanatokana na jitihada za makusudi za kuhamasisha na kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi hizo.

Lengo la kuvutia uwekezaji kutoka nje ni kupata manufaa yatokanayo na uwekezaji huo ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mitaji, ujuzi na teknolojia mpya na ya kisasa, kuongeza fursa za ajira, fursa za masoko nje ya nchi kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini, idadi ya watalii kutoka nje, mapato ya fedha za kigeni, mapato ya Serikali kutokana na makusanyo ya kodi na kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi wa nchi.

Suala la msingi ni kuhakikisha kwamba, kama nchi tunapata manufaa yanayotarajiwa kutokana na uwekezaji kutoka nje. Hata hivyo, uwekezaji kutoka nje hautazuia wala kuondoa umuhimu na faida za uwekezaji wa ndani. Tunahitaji kuongeza kiwango cha mitaji kutoka nje ili kujenga uwezo wa wananchi wetu wa kumiliki na kuendesha miradi na uchumi wao.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na kuwekeza nchini ili kuvutia uwekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kiwango cha kuweka akiba kama sehemu ya Pato la Taifa hapa Tanzania ni cha chini sana na hakiwezi kukidhi mahitaji yetu ya uwekezaji.

Pia uwezo wetu wa kukopa mitaji ni mdogo, hivyo, tunayo sababuya msingi ya kuvutia mitaji kutoka nje. Serikali itaendelea kuhamasisha na kuvutia uwekezaji kutoka nje na ndani ili kujenga uchumi wenyewe misingi imara na endelevu ambayo itawezesha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kama dira yetu ya taifa ya 2025 inavyotuelekeza. (*Makofî*)

MHE. AMINA ABDULLA AMOUR: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, wawekezaji wanaotoka nje huwa wanakuja na wafanyakazi wao kutoka nchi zao na hii inapunguza ajira kwa vijana waliokuwepo hapa Tanzania. Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti hali hii?

Pili, kwa kuwa, wawekezaji wa Kichina ambao wanauzu maua na wengine wanakuwa na magari ya mkokote kuuza viatu na biashara nyiningine na hii inawapunguzia walalahoi biashara.

Je, huo ndiyo uwekezaji tunaoutaka?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Abdulla Amour Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Kuhusu swali lake la kwanza kwamba wawekezaji wa nje wanakuna na wafanyakazi wao kutoka nje kuchukua nafasi ya waanzania, hili ni tatizo! Lakini kwa mikataba ambayo tunaiweka na kwa ufuatiliaji mzuri wa Serikali na Watanzania kwa ujumla, wawekezaji wa nje wanapaswa kuleta wafanyakazi wale ambao hawapatikani kwa ujuzi au kwa utaalamu ndani ya nchi yetu.

Kwa hiyo, nitalomuhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lote ni kwamba tutajitahidi sana kuona kwamba wawekezaji hawaii na wafanyakazi pale ambapo Watanzania wapo lakini wanapokuja na teknolojia mpya na ni jambo ambalo tunalitafuta na kama hakutakuwa na Mtanzania hatuna la kufanya.

Lakini ni kweli kwamba hatupaswi kuruhusu uwekezaji ambao unawanyima Watanzania nafasi za kazi na manufaa mengine ambayo tunayapata na pia tunapaswa kujua tunataka nini kutoka kila uwekezaji unaowekezwa Tanzania.

Kwa hiyo, kuhusu swali la pili, Wachina wanatembeza mikokoteni na vilevile wanauza maua kwa kweli hili siyo jambo la kuendekeza. Pale ambapo Watanzania wana uwezo wa kuwekeza kwenye shughuli za kiuchumi hatupaswi kuwaendekeza wawekezaji wa nje wachukue nafasi hiyo kwa sababu ni kunyima Watanzania na kuchukua hatamu ya uchumi wao.

Kwa hiyo, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kama hilo lipo basi tutalifuatilia na kama tutahakikisha kwa siku usoni kwamba wawekezaji ambao tunataka waje na mitaji mikubwa waje na teknolojia mpya na waweze kutupatia masoko nje

hawaji kufanya shughuli ambazo Watanzania wanaweza kufanya.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba kuna uwiano gani angalau kwa asilimia kati ya wawekezaji wanaowekeza Tanzania wanaotoka nje na Watanzania wanaowekeza nje?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa majibu yangu ya msingi nilisema kwamba hatuwezi kuepuka kuvutia uwekezaji kutoka nje kutokana na uwezo wetu mdogo wa mitaji.

Kwa hivyo tungependa kuwa na uwiano fulani, lakini kutokana na tatizo la msingi la Watanzania kutokuwa na mitaji ya kutosha na kazi ya nchi sasa ni kujenga uwezo wa Watanzania wawe na mitaji, lakini hata hivyo hatuwezi tukaepuka kuwa na wawekezaji kutoka nje kwa sababu hata America ambayo imeendelea sana hata Wachina wenyewe wanaokuja Tanzania bado wanahamasisha uwekezaji kutoka nje.

Lakini jambo la kufurahisha mpaka sasa miradi ambayo inaendeshwa na Watanzania wa ndani ni mingi kuliko miradi inayoendeshwa na wawekezaji kutoka nje. Ninajua kwamba tuna miradi 1,559 ya kutoka nje mwaka 2011, lakini miradi ya ndani inayoendeshwa na Watanzania ni 3,078.

Lakini unaweza ukakuta kwamba thamani ya miradi ya Watanzania ni ya chini kwa sababu uwezo wetu wa mtaji ni mdogo. Kwa hivyo siwezi nikaeleza hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tunaweza tukaweka uwiano fulani wakati tuko mbali sana na mahitaji yetu ya uwekezaji ili kuweza kujenga uchumi imara. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata, lakini tunakuomba Mheshimiwa Waziri kwa kweli ufuatilie hilo suala la Wawekezaji Wamachinga kukokota mikokoteni na wakichukua nafasi za vijana wetu wa Kitanzania.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Sawa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini.

Na. 109

Kujenga Zahanati Na Kuzipatia Vifaa

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA aliuliza:-

Vita vya kupunguza vifo vya Mama na Mtoto Nchini itafanikiwa kwa kuwa na ujenzi wa zahanati katika kila kijiji na vituo vya afya kwa kila Kata:-

Je, Serikali ipo tayari kujenga zahanati katika Jimbo la Kasulu Vijijini na hatimaye kuzipatia vifaa ili zifanye kazi kwa ufanisi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMII) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha naomba niungane na ndugu yangu Ole Medeye kutoa pole sana kwa waumini wote wa Kanisa la Kilutheri Dayosisi ya Kaskazini, Mjini Kati kwa kuondokewa kwa kiongozi wao mpandwa Baba Askofu Thomas Laizer.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Zahanati nchini unafanyika kwa ushirikiano kati ya Serikali na wananchi kupitia Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (*O&OD*). Kupitia mfumo huu, wananchi wanaibua miradi ya maendeleo kwa kuzingatia aina ya matatizo yaliyopo. Aidha, wananchi wanashiriki pia katika utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuchangia nguvu kazi fedha, Halmashauri inachangia pale uwezo unaporuhusu ili kuhamasisha nguvu za wananchi. Vilevile, miongoni mwa majukumu ya Mfuko wa Kuchocha Maendeleo katika jimbo, ni pamoja na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kasulu Vijijini lina Kata 19 na Vijiji 42. Jimbo hili lina vituo vya afya sita (6) ambapo vituo 4 vinafanya kazi na vituo vingine viwili (2) ni vipyaa. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kununua dawa na vifaa ili viweze kuanza kazi. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wananchi inajenga kituo cha afya katika Kata ya Rungwe pamoja na kufanya upanuzi wa zahanati za Nyamidaho na Makere ili kuzipandisha hadhi ya kuwa vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kasulu Vijijini, lina zahanati 30 zinazotoa huduma katika vijiji 30 vya Jimbo hili. Vijiji vingine 5 viko karibu na vituo vya afya, hivyo wananchi wake wanapata huduma za afya katika vituo hivyo. Kwa takwimu hizi, vijiji 7 tu kati ya vijiji 42 ndivyo ambavyo havina zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa afya ya mama na mtoto, Serikali katika mwaka wa fedha 2011/2012, iliboresha huduma za afya katika vituo vya afya vya Shunga na Nyenge ili viweze kutoa huduma za upasuaji kwa wajawazito. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali iliidhinisha shilingi milioni 56 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati na shilingi milioni 40

kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa vituo vyatya afya na zahanati za Jimbo la Kasulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada hizi za kuboresha huduma za afya katika Jimbo la Kasulu Vijijini zimechangia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 68 katika watu 100,000 mwaka 2011 hadi vifo 60 katika kundi la watu 100,000 mwaka 2012. Aidha, vifo vyatya watoto chini ya miaka mitano vimepungua hadi kufikia 21 katika kila watoto 1,000 ambapo kiwango cha kitaifa ni vifo 51 kati ya watoto 1,000 waliozaliwa hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kushirikiana na wananchi kuboresha huduma za afya katika Jimbo la Kasulu Vijijini kadri fedha zinavyopatikana. (*Makofii*)

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu yaliyoandaliwa kwa kina na mijibu swali, ninaomba niulize maswali mawili.

Kwanza kwa kuwa ujenzi wa vituo vyatya afya nchini na zahanati ni suala la kisera na ni ahadi ya Serikali. Ninahitaji kupata maelezo ni mpango gani umeandaliwa na Serikali kuhakikisha vituo vyatya na zahanati vinajengwa nchi nzima kabla ya mwaka 2013?

Pili, kwa kuwa mijibu swali Mheshimiwa Naibu Waziri amethibitisha kwamba vituo hivi na zahanati hujengwa na Serikali kwa kushirikiana na wananchi. Na kwa kuwa Kata ya Nyamidaho, Kitagata na Rungwe Mpya wameshachangia kwa kiasi kikubwa ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu iliwapatia shilingi milioni ishirini na nane kwa kila Kata.

Je, Serikali iko tayari kutafuta fedha na kuwawezesha Kata hizi ili vituo hivyo vikamilike haraka iwezekanavyo na sio kusingizia kwamba Mfuko wa Jimbo unaweza kusaidia ni miradi mikubwa hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Mbunge na tunachosema sisi Serikali ni hicho hicho. Yaani ukienda kuuchukua ule Mpango wa miaka kumi, hii habari ya zahanati, vituo vya afya vyote utaikuta imo mle ndani na ni kipindi cha miaka 10 utaangalia mle ndani.

Sasa kuna jambo hapa ambalo ni lazima tuelewane. Tunapozungumza habari ya kujenga zahanati kwa kila kijiji na kwamba tunataka kujenga kituo cha afya katika kila Kata. *The bottom line is mpango huo lazima uanze na wananchi wenyewe.* Hii (*O&OD*) ni kitu kinachoitwa (*Opportunities and Obstacles to Development*), yaani Fursa na Vikwazo katika Halmashauri inayohusika. Kasulu wakifika mahali wakasema kituo cha afya sio muhimu kwetu sisi nafikiri kituo muhimu hapa ni kituo cha Polisi, sisi kama Serikali tunaheshimu kwamba Kituo cha Polisi ni muhimu zaidi, ndicho kinachozungumzwa hapa.

Kwa maneno mengine hapa tunachotakiwa kufanya ni *prioritise* mambo yetu pale katika Halmashauri. Halmashauri kama Halmashauri ndiyo inaitwa Serikali. Ukisikia tunasema Serikali hapa ni Halmashauri ndiyo inaitwa Serikali. Ninachotaka kusema hapa *concerns* za Mheshimiwa Mbunge ninazielewa, ukifanya utani utani kidogo hapa watoto watakuwa, ukifanya utani utani hapa akinamama watakuwa.

Lakini kama mmenifuata vizuri takwimu hizi zinaonyesha kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana katika Wilaya ya Kasulu hususan katika jimbo la kwako Mheshimiwa. Ndiyo maana unaona vifo vya akinamama vimepungua na vifo vya watoto vimepungua. Ndiyo maana nimetoa takwimu kuonyesha kwamba ukichukua vile vituo vya afya vilivyopo karibu na vijiji ukijumulisha na vijiji vyenyewe kwako Mheshimiwa Agripina sasa hivi tunahitaji kujenga zahanati saba tu, tutakuwa tumemaliza kazi, tutakuja kuchambua wote sisi kwa pamoja kwa sababu wewe unachosema ndicho tunachosema

sisi ni kwamba hapa tunataka tuwekane sawa tuelewane vizuri.
(Makof)

Kwa hiyo, tunapozungumza habari ya Nyamidaho na zile Kata nyiningine na shilingi milioni 28 zimetoka tumeanzisha na hili naomba nijibu kwa ajili ya Wabunge wengine pia, tumeanzisha kitu kinachoitwa *CHF* ile Bima ya Afya ya jamii ile ndiyo siri ya jambo hili. Mkichanga shilingi 200 Serikali kupitia *NHIF* inawapa shilingi milioni 200 nyiningine jumla zinakuwa milioni 400, zile ni pamoja na vifaa tiba na dawa na pamoja na ujenzi unaofanyika kule. Ninachoeleza hapo naeleza utaratibu na sera na mipango hii ambayo imeulizwa hapa. Nilitoa mfano nikaeleza hapa katika Wilaya ya Rombo waliokota shilingi milioni 250 wakaongezewa shilingi milioni 250 wana shilingi milioni 500 ukizungumza habari ya Rombo leo hakuna mahali ambapo hawana dawa na Mbunge wao yuko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachotaka kusema hapa sauti hii inapanda ni msisitizo tu sio nataka kugombana ni msisitizo tu. Ili tuweze kuwekana vizuri Mheshimiwa Agripina pamoja na wenzako Mheshimiwa Moses Machali wote nyie nawaombeni, kama mnataka tutakuja Kasulu nije nikawasaidie jinsi ya kueleza jambo hili tuje tukalifanye vizuri. Hela hizi zikipatikana ni hela nydingi sana hakuna haja ya kulalamika kwamba hakuna dawa, vifaa tiba, nyumba hazijajengwa. Tunachofanya sisi ni kushirikisha *Constituency Development Catalyst Fund* anayosema hapa kazi yake ni hiyo. Ananiambia usiseme habari hii ya Mfuko wa Kuendeleza. Ule Mfuko kazi yake ni hiyo. Kwa hiyo, ni pamoja na hiyo na mifereji pamoja na visima na kadhalika. Niko tayari kukaa na Mheshimiwa Mbunge tuzungumze zaidi kuhusu jambo hili. *(Makof)*

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba vituo hivi vya afya na zahanati zinajengwa kwa nguvu za wananchi na Serikali. Lakini wako wananchi wametoa nguvu zao wamejenga vituo vya afya na zahanati na vimekamilika lakini havitoi

huduma. Je, Serikali inasema nini ina mpango gani wa haraka kunusuru maisha ya Watanzania hao walitoa nguvu zao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki anachosema ni kweli. Sisi tumekwenda mpaka kule lyonga kule kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumekwenda maeneo mbalimbali katika nchi hii viko vituo vya afya vimeanzishwa na havifanyi kazi kwa maana ya kwamba hawana watumishi *that's is true* na Wabunge wote hapa wakisimama hapa najua hili jambo watalisema. Juzi tumefanya mukutano kati ya TAMISEMI, Waziri wa Nchi, Waziri wangu tulikuwa naye pale pamoja na Waziri wa Afya tukaita na timu ya wataalamu wote tukasema kazi ya kwanza tutakayofanya hapa kwa hivi vituo tunavyozungumza pamoja na zahanati ni kuvi-*register* kuhakikisha kwamba vinaandikishwa vinakubalika na wala hatuhitaji urasimu mwangi. Tumekubaliana hivyo wote tulikuwepo, mimi nilikuwepo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi alikuwepo, Mheshimiwa Mwinyi alikuwepo na Naibu Waziri wake alikuweko pale tukakubaliana kwamba tufanye kazi ya ku-*register* na kuhakikisha kwamba tutapata.

Lakini la pili kuhusu watumishi wanaozungumza hapa tunesema kuanzia sasa hatumtaki Waziri wa Afya atupitishie tena Madaktari au Manesi wapelekwe moja kwa moja huko wanakokwenda. Lakini jana na juzi nimemsikiliza Waziri wa Afya akizungumza kwenye vyombo vya habari moja ya matatizo makubwa tuliyonayo ni kwamba watumishi hawa wakipangwa katika hivi vituo katika maeneo ya pembezoni hawaendi. Sasa mtusaidie hapa, tusaidiane wote kwa pamoja, wakati mwingine matatizo haya tuliyonayo yako ndani ya mkoa kule kule. Kwa hiyo, tumewaagiza Makatibu Tawala wa Mkoa wahakikishe kwamba watumishi ambao wanapangwa katika maeneo haya wanakwenda.

Lakini la pili, tunazungumzia habari ya kuwamotisha. Mkoa wa Rukwa daktari akienda pale wanampa motisha, wakati mwingine wanamsaidia chakula, wanampokea vizuri ukienda pale wananchi

wakikupokea sanduku karibu kwetu hapa wala usije ukafiriki kwamba jambo hilo ni dogo. Wakati mwengine watu wanam-*dismiss* daktari wanamwacha hivi na mke wake na watoto wake, wamefanya vizuri na *retention* ya mkoa wa Rukwa sasa hivi ikifuatana na Mkoa wa Katavi ni nzuri kwa sababu ya moyo wa ukarimu ambao wananchi wa Sumbawanga wameonyesha na watumishi hawa wanaojitolea kwenda kufanya kazi katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, hayo yote tutayafanya na tutahakikisha tunaboresha mazingira ya kazi ili watumishi wanaokwenda katika maeneo hayo waweze kufaidika. (*Makof*)

MHE. MWIGULU L.N. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niipongeze Serikali kwa sera yake ya kujenga zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila Kata, hiyo ndiyo CCM Bwana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhitaji wa kituo cha afya na zahanati unatofautiana kufuatana na umbali wa Kata kwenda kwenye Hospitali ya Wilaya ama barabara kuu. Kata kama ya Tulya ama Kidaru katika jimbo la Iramba na Wilaya ya Iramba na Kata kama Isakamaliwa, Mwamashiga, Mwamashimba katika Jimbo la Igunga, Wilaya ya Igunga. Kata kama Mnazimoja, Nguvu moja katika Jimbo la Igunga ni Kata ambazo ni ngumu sana kufika katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga kufuatana na mbuga zilizoko kule.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kutoa vipaumbele kwenye Kata ambazo ni ngumu kumwahisha mgonjwa kwenye Hospitali ya Wilaya kuliko Kata zingine ambazo ziko karibu na Hospitali au barabara zinakofikika kama maeneo aliyotaja na jimbo la Mkarama Wilaya mpya ya Mkarama? (*Makof/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii very closely tulikuwa tunafuatilia jitihada za Mheshimiwa Mbunge katika jimbo lake la Uchaguzi. Anafanya kazi

nzuri sana katika jimbo lake na hasa katika eneo hili la kuhakikisha kwamba akinamama na watoto wanapata huduma nzuri. Napenda kwa niaba ya Serikali kumpongeza sana Mheshimiwa Nchemba kwa kazi nzuri unayoifanya pale. (*Makofi*)

Nataka tu niseme mambo mawili tunayoyafanya kwa sasa hivi. Kwanza kama alivyosema yeye mwenyewe ni kwamba hizi zahanati na vituo vya afya ambavyo vinaonekana kwamba havifikiki moja ya mambo tunayoyafanya ni kuhakikisha dawa zinakuwepo na huduma zote zinapatikana pale pale katika hilo eneo ambalo analizungumza. Siwezi kuzikariri yeye anazifahamu kwa sababu anatoka kule na moja ni hilo. Lakini la pili, ni kuimarisha mawasiliano kati ya Makao Makuu kwa maana ya Hospitali ya Wilaya na kule Kata ziliko. Lakini la tatu ni kuhakikisha kwamba kama magari yanapatikana *ambulance* tunaweza tukawasaidia pale. Nitakaa na Mheshimiwa kwa jitihada zake alizoonyesha ili tuone namna tunavyoweza kumsaidia katika haya maeneo.

Na. 110

Kuzalisha Wavuvi Wakubwa na Kuwapatia Mikopo

MHE. DUSTAN L. KITANDULA aliuliza:-

Sekta ya Uvuvi nchini hususan katika Ukanda wa Bahari bado haijatumika kikamilifu katika kukuza uchumi wa nchi na kuwaondolea Wananchi umaskini:-

Je, Serikali ipo tayari kuanzisha utaratibu wa makusudi wa kuzalisha Wavuvi wakubwa na kuwapatia mikopo na vivutio stahiki kulingana na mahitaji na mazingira ya wahitimu wa Vyuo hivyo vya Uvuvi kama wafanyavyo wenzetu wa Afrika Kusini walipotengeneza tabaka la Wakulima wakubwa?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako nitumie fursa hii kama wenzangu walivyofanya kutoa pole nyingi kwa familia ya Marehemu Baba Askofu Thomas Olomoljoi Laizer na waumini wote wa Kanisa Iala Kiinjili la Kilutheri la Tanzania (KKKT) na Watanzania kwa msiba huu mkubwa. Mungu ailaze mahali pema roho ya Marehemu Askofu Laizer peponi. (*Amina*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri labda dakika moja tafadhalii. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni sasa hapa nasimama kwa mujibu wa Kanuni nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote kutoa pole kwa msiba huu mkubwa wa Askofu wetu Thomas Laizer na kwa kweli madhehebu yote yanaguswa na kifo hicho ni pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge, lakini vilevile na Watanzania wote.

Kwa hiyo, tunawapa pole wenzetu na tunawaomba Mwenyezi Mungu awape nguvu katika kuhimili msiba huo na Mwenyezi Mungu aipokee roho ya Marehemu mahali pema peponi. (*Amina*)

Hivyo kwa mujibu wa Kanuni hii sasa nadhani tuendelee na ratiba kama pole zitakuwa zimeshatolewa na kitii. Kwa hiyo, wengine wote sasa tutaendelea na kazi na mazingira ya kutoa pole yanaweza kufanyika kwa utaratibu mwingine nje ya ukumbi.

Waheshimiwa Wabunge naomba tuendelee.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwawezesha wavuvi nchini imeweka utaratibu wa kuwapunguzia gharama za uvuvi wazalendo wanaovua samaki katika maji ya kina

kirefu hususan Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone*). Chini ya utaratibu huo wavuvi wazalendo hulipa gharama ndogo za leseni ukilinganisha na wavuvi wa kigeni.

Kwa mfano, ada za leseni kwa kuvua kwa mishipi (*long lining*); wavuvi wazalendo hulipa kiasi cha Dola za Kimarekani 1,000 kwa mwezi mmoja ambazo ni sawa na asilimia 28.57 ukilinganisha na ada ambazo hulipwa na wavuvi wa kigeni ambazo ni Dola za Kimarekani 3,5000 katika kipindi hicho. Aidha, Benki ya Rasilimali (*TIB*) imetoa mikopo ya Tsh. Milioni 680 kwa ununuzi wa vifaa vya Uvuvi, Tsh. Milioni 233.5 kwa ajili ya mitaji ya Biashara ya Mazao ya Uvuvi na Tsh. Bilioni 2 zimetengwa na Benki ya Rasilimali (*TIB*) kama mikopo kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Boti za Uvuvi zinazotengenezwa kwa "Fibre glass".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mradi wa *MACEMP* imefadhili vikundi vya wavuvi katika Halmshauri 16 za ukanda wa Pwani ambapo jumla ya miradi 470 yenye thamani ya shilingi 6,702,865,484.00 inayohusu shughuli za uvuvi imeibuliwa na kutekelezwa. Jumla ya wananchi 8,082 walinufaika na miradi hiyo. Aidha, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimetoa punguzo la kodi ama kufuta kodi kabisa kwa zana za uvuvi kama vile injini za uvuvi na mali ghafi zinazotumika kutengeneza zana mbalimbali za uvuvi na viambata vyake vinavyonunuliwa kutoka nje ya nchi (*East African Publication (2007) on Common External Tariff*). Lengo ni kuwapunguzia wavuvi gharama za uzalishaji na kuwawezesha kuwa na vyombo vyenye uwezo wa kuvua samaki wanaopatikana katika maji ya kina kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zote hizi zinalenga kuandaa mazingira wezeshi wavuvi na kuwa na wavuvi wakubwa, watakaochangia zaidi katika pato la Taifa. Wajasiriamali na Wahitimu wa Vyuo vya Uvuvi watambue kwamba kuna fursa za mikopo katika dirisha la Benki ya Rasilimali (*TIB*) kwa ajili ya shughuli za kiuchumi zikiwemo za uvuvi na tunatoa wito watumie fursa hizo kikamilifu. (*Makofii*)

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ambayo hayaridhishi na yamekwepa kujibu swali nina maswali mawili ya nyongeza. Nchi kama Vietnam inaingiza mapato kwa sekta ya uvuvi yanayokaribia dola milioni 5,200 kwa mwaka nchi kama Thailand inaingiza dola milioni 3,300 kwa mwaka. Nchi kama Iran kwa mwaka uliyopita imeingiza dola millioni 400 kwa ajili ya sekta ya uvuvi. Waziri anataka kutuambia kwa majibu yake haya yupo *happy kwamba* Wizara yake imefanya vya kutosha kuwaondolea umaskini wananchi wa ukanda wa Pwani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Waziri anafahamu kwamba kutengeneza *fiber boat* moja ni karibu milioni 100 na kwamba bilioni mbili anazozisema ni sawasawa na boti kumi. Wizara iko happy kwa hali ya uvuvi ilivyo mbaya katika nchi yetu na wao wanatuambia wamefanya kitu?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane naye kwamba tofauti ni kubwa sana kati ya nchi alizozitaja na nchi yetu. Lakini tofauti haipo kwenye sekta ua uvuvi tu, ipo katika kila sekta na nchi zote alizozitaja ni *middle income countries* na sisi hatujafika huko japo lengo letu kwa mujibu wa dira yetu, (*Development Vision 2025* ni kufika huko. Kwa hiyo nimhakikishie tu kwamba tofauti hiyo ipo kubwa lakini tunajipanga tuanze kuelekea kule maana tumetofautiana na nchi hizo katika mambo mengine mengi ya elimu, teknolojia, mitaji na kadhalika.

Swali la pili; nakubaliana na yeye kwamba kiasi cha *fiber boats* zinazotengenezwa kwa pesa hiyo ya mikopo ni ndogo lakini ni mwanzo na tukijipanga na kuelekea kule kwa uhakika ni lazima tujenge uwezo zaidi wa vifaa hivyo vya kuvulia na uwezo wa watu wetu wanaovua kimitaji na kiteknolojia. Kwa hiyo, sisemi kwamba hapa tulipo tunaridhika lakini hali halisi ni hiyo. Tutaendelea kuwaomba mwongeze Bajeti uwezo ujengwe zaidi, uzalishaji

ufanyike zaidi, maana tuna *potential* kubwa katika uvuvi kushinda mataifa aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. (*Makofii*)

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Sekta hii ya uvuvi ni sekta nyeti sana na hususan kwa wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Jimbo la Kigamboni kwa ujumla, kutelekezwa kwa Sekta hii kumepelekea kuwepo na uvuvi haramu katika maeneo ya Kigamboni, Mjmwema, Somangila, Kata ya Kimbiji hadi Pemba Mnazi.

Swali nataka kujua kutoka kwa Naibu Waziri, ni nini mikakati ya Serikali katika kudhibiti uvuvi haramu na kuhakikisha kwamba wale wavuvi katika maeneo yale wanapewa nyenzo za kutosha ili kufanya uvuvi endelevu?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nikiri na kukubaliana naye uvuvi haramu ni tatizo kubwa katika maeneo ya Kigamboni na Ukanda huo mpaka Kimbiji ukipita kwa kweli mabomu yanasi kika sumu inatumika. Mkakati wetu wa kitaifa wa kukomesha uvuvi harama imeelezwa vizuri katika mkakati mzima wa kuendeleza sekta ya uvuvi. Moja kubwa ni elimu kwa umma na elimu kwa wadau wakuu wa uvuvi wajue kwamba uvuvi haramu unakatazwa. Siyo kwa kuwakwaza wao bali kufanya uvuvi uwe ni shughuli endelevu katika sekta ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunaulinzi shirikishi na katika maeneo mengi yakiwemo haya ya kwake *beach Management Units* zimeanzishwa kama ishara na chombo cha kuwa na ulinzi shirikishi ili raia wema waweze kuwa ndiyo walinzi wa rasilimali hizo za uvuvi.

Lakini lingine Sheria pia ziko wazi, kikosi cha doria kikishirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vimedu na kazi ya kuwakamata hawa watu na kuwashtaki na kuwafungulia mashtaka na wengi wamepewa adhabu ama ya faini ama ya

kifungo kwa sababu ya kukamatwa wakijihusisha na shughuli hizo haramu. (*Makofi*)

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa suala la msingi linazungumzia kuwaondolea umaskini wananchi wanaoishi maeneo ya kandokando ya bahari; na kwa kuwa Mkoa wa Pwani zaidi ya asilimia 45 maeneo yake ni Ukanda wa Bahari na maeneo mengine ni visiwa. Kwa hiyo wananchi wengi wa maeneo hayo wanajishughulisha na biashara za uvuvi.

- (i) Je, Serikali iko tayari kuwasaidia wananchi hao hususan wanawake wanaofanya shughuli za uvuvi na kilimo cha mwani?
- (ii) Je, kwa kuwa Serikali inaonekana haina uwezo, iko tayari kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi ili kundokana na adha hii wanayopata wananchi wote wanaoishi maeneo ya bahari na maziwa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio serikali iko radhi na ipo tayari kuwasaidia akina mama wajipange vizuri na wachangie katika kutatua tatizo zima la umaskini. (*Makofi*)

Lakini tunapokuja kwenye hali halisi, tumewaelekeza kama tulivyotoa mwito kwenye majibu yangu ya swali la msingi kwamba kuna fursa na dirisha katika Benki ya Rasilimali (*TIB*) na tungewaomba akinamama wanaoishi katika ukanda wa pwani, wajipange wawe kwenye vikundi na watafute mikopo huko kwenye vyombo na taasisi za fedha zaidi kuliko kutazamia kupata ruzuku kutoka Serikalini.

Lakini pamoja na kwamba swali ni moja lakini tuko radhi kuchukua mawazo yake na kuyafanyia kazi na natumaini kwamba Mheshimiwa Mbunge atashirikiana na Wizara yangu katika kufanyia kazi pendeleko alilotoa. (*Makofi*)

Vyombo vyatya Habari Kutoa Huduma ya Habari kwa Walemavu wa Kuona na Kusikia

MHE. LUCY F. OWENYA aliuliza:-

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka wazi haki ya kila Mtanzania kupata habari.

Je, ni lini vyombo vyatya habari vya Serikali vitatoa fursa kwa Watanzania wenyewe ulemavu wa kuona na kusikia kupata mahitaji maalum ya habari kama ilivyo kwa Watanzania wengine wasio walemavu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kutoa fursa za kupata habari kwa Watanzania wenyewe ulemavu wa kuona na kusikia kama ilivyo kwa Watanzania wengine wasio na ulemavu kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 18 inatamka wazi kuwa kila raia anayo haki ya kupata habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha haki hiyo ya msingi inapatikana kwa watu wenyewe ulemavu wa kuona na kusikia, Serikali imekamilisha marekebisho ya Kanuni za Maudhui za Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta ambazo zitavitaka vyombo vyatya habari vyote kuwa na wakalimani wa lugha ya ishara. Kukamilika kwa Kanuni hizi kutafanya kuwepo wakalimani hao kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hizo zimeshafanyiwa marekebisho na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, amezisaini na kuziwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya hatua za utekelezaji. (*Makofii*)

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Serikali inatambua umuhimu wa watu wenyewe ulemavu wa kusikia na kuona kupata habari na kwamba Serikali imeshakamilisha na Kanuni na Sheria ya kuvitaka vyombo vya habari viwe na wakalimani kwa ajili ya watu hao wenyewe ulemavu.

Sasa mimi ningependa kupata jibu kutoka kwa Waziri ni lini Serikali itupe *timeframe* ni lini watakamilisha Sheria hiyo ili iweze kutekelezeka na watu hao wenyewe ulemavu waweze kupata habari kama watu wengine?

Swali la pili, kwa kuwa *TBC* ni Televisheni ya Taifa na inatumika kwa walipa kodi Watanzania pamoja na watu wenyewe ulemavu. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri haoni sasa ni wakati mwafaka sasa kwa kuanzia Televisheni ya Taifa iwe na wakalimani ili watu hawa waweze kupata habari? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ni kwamba tayari Sheria hii ya *EPOCA* Waziri mwenye dhamana ambaye ni Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ameshaisaini na amepeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maana ya kuandikwa na kutoa kama tangazo ili zianze kutumika rasmi. Kwa hiyo ni wakati wowote kuanzia sasa Mwanasheria Mkuu anafanya kazi hiyo kwa maana ya kutekeleza kuandika *GN* ili zianze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli *TBC* ni chombo cha taifa na niseme kwamba moja ya matatizo makubwa ambayo yamefanya mpaka sasa kutokuwepo kwa wakalimani katika vipindi mbalimbali ni kutokana na gharama hizo za wakalimani. Lakini *TBC* inatoa nafasi kuna kipindi cha Wape Nafasi ambacho mlemavu ndiye huwa anasimamia kile kipindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri huo lakini pia kuanzishwa kwa Sheria hii na itakapoanza kutumika kila chombo cha habari kinapaswa kuwa na mkalimani wa alama za vidole.

MHE. ALLY K. MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wewe naona ni mpenzi mkubwa wa mchezo wa mpira. Sasa swali kwanini Chama cha Mpira wa Miguu (*TFF*) kila mara Ndugu Michael Wambura, anapoomba uongozi kila mara wanamkatalia?

Ndugu Michael Wambura, kuomba uongozi imekuwa nongwa, akiomba cheo chochote katika uongozi wa Mpira wa Miguu anapigwa chaki, kwa nini? (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy, sasa hilo suala la Wambura linaendana na alama za vidole kwenye televisheni. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufupi hebu mfahamishe Mheshimiwa Keissy lakini yupo nje ya swali kabisa amekuja na ajenda yake mpya.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba Mheshimiwa Mbunge anaguswa sana na suala la Ndugu Michael Wambura, kugombea na kutokuteuliwa na mimi nataka niseme sisi kama Wizara tunaosimamia michezo ipo taasisi ambayo iko huru kabisa ambayo ni *TFF* hao ndiyo wanaochuja wagombea na ambao wanasmamia mambo yote na taratibu zote za michezo.

Kwa hiyo, mimi nataka awasiliane na Ndugu Michael Wambura, ili aendelee kumsaidia na kumshauri ni namna gani anashindwa kupata vigezo ambavyo *TFF* wameviweka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Kheri Khatibu Ameir, Mbunge wa Matemwe na linaenda Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

MHE. KHERI KHATIBU AMEIR: Mheshimiwa MwenyeKITI, naomba kulitoa swali hili kwa sababu ni la muda mrefu sana tangu nililete na kwa muda huu Mkongo umefika. Kwa hiyo naomba kulitoa.

(*Swali Na. 112 liliondolewa na mwuliza swali*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Ameir. Waheshimiwa Wabunge swali hili limeondolewa katika *Order Paper* ya leo na mwuliza swali kwa kuwa amesharidhika na utekelezaji wa Serikali katika eneo hilo. Kwa hali hiyo tutaendelea na swali linalofuata linaloenda Wizara ya Fedha na linaulizwa na Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini.

Na. 113

Ukusanyaji wa Kodi Usioridhisha

MHE. RAMADHANI HAJI SALEH aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo la ukusanyaji wa kodi usioridhisha hapa nchini hali inayopelekea ukosefu wa mapato:-

Je, hatua gani zimechukuliwa ili kutatua tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Haji Seleh, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za Kisheria na Kiutawala za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani mwaka hadi mwaka. Hatua za Kisera zilizochukuliwa ni pamoja na kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi, kwa lengo la kudhibiti na kupunguza misamaha hiyo, kuboresha mfumo wa kodi katika sekta isiyo rasmi na kufanya maboresho ya uwianisho wa Sheria za Kodi.

Hatua za kiutawala ni pamoja na maboresho ya mifumo ya ukusanyaji na usimamiaji wa mapato, kuendelea kupanua uwigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya, kuimarisha uchumi tulivu pamoja na kuweka mazingira bora ya biashara ili kuiwezesha sekta binafsi kukua. Aidha, udhibiti wa upotevu wa mapato umeimarishwa kwa kuanzisha matumizi ya mashine za *electronic* za kutoa stakabadhi za kodi, yaani *electronic fiscal devices*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeimarisha huduma na elimu kwa walipa kodi ili kuongeza ulipaji kodi kwa hiari. Hatua zingine zilizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha usimamiaji wa kodi kwa msingi wa vitalu vya walipa kodi (*Block Management System*), kuongeza ujuzi katika shughuli za ukaguzi na kuweka mfumo wa usimamiaji wa kodi unaozingatia viashiria hatarishi vya upotevu wa mapato (*Enterprise Wide Risk Management System*).

Mamlaka ya Mapato pia inajiandaa kunufaika na mpango wa kuwapatia Wananchi wote Vitambulisho vya Taifa (*National ID*). Zoezi hili ni muhimu sana kwa sababu litasaidia kuhakikisha kila Mwananchi anayepaswa kulipa kodi anafanya hivyo. Hatua nilizozitaja zimeongeza mapato kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na baadhi ya nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara na kukaribia

wastani wa uwiano wa mapato na Pato la Taifa katika eneo hili ambao kwa sasa unafikia 18.1%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu mapato yetu yamekuwa chini ya wastani wa 18.1%, makadirio ya kukusanya shilingi trillioni tisa na mia nane sabini na sita ukijumuisha mapato ya Serikali za Mitaa katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, ni sawa na 18.7% ya Pato la Taifa. (*Makofi*)

MHE. RAMADHANI HAJI SALEH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niulize swali moja tu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kumekuwa na sintafahamu katika ukusanyaji wa mapato katika nchi yetu, hali inayopelekea Watanzania kutoamini kuwa mapato haya yanayopatikana siyo sawa. Je, Serikali inawaambiaje Watanzania kuhusu hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Watanzania wote kwa ujumla kuwa, takwimu tunazozitoa kwa ajili ya kulipa kodi zipo wazi na mahali popote pale ambapo kodi inapokelewa kuna taratibu zake na takwimu zinawekwa. Kwa hiyo, labda kitakachotakiwa ni kuwa zioneshwe kwa uwazi zaidi, sehemu nyingi zaidi, ili Wananchi waamini kama kweli tunapokea hizo kodi kama tunavyotamka na kuwa kodi hizo zinatumika katika maeneo ambayo Serikali imepanga kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mengine zaidi tutajitahidi kadiri iwezekanavyo, kutoa taarifa zaidi mpaka kufikia walengwa wote hadi Wananchi wa Vijijini kujua kama kweli tunakusanya, lakini takwimu hizo ni sahihi na ni rahisi kuzithibitisha.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa baada ya *operation* aliyoifanya Mheshimiwa Mwakyembe pale Bandarini (*TPA*), imeonesha kwamba ni dhahiri mapato mengi ya Serikali yanaingia mifukoni mwa watu binafsi badala ya kuingia Serikalini na kuwanufaisha Watanzania wote. Ninaomba Serikali *in a very serious note* iwaambie Watanzania; itafanya mkakati gani ili mambo yaliyokuwa yakifanyika *TPA* yasifanyike mahali popote na kupoteza mapato ya Watanzania? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Ningependa kuchukua nafasi hii, kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, kwa kazi kubwa na ya ujasiri anayoifanya katika Mamlaka ya Bandari na yamkini katika Wizara nzima ya Uchukuzi. Kwa kupitia juhudi kama hizo za Waheshimiwa Mawaziri na Viongozi wengine wa Serikali, kwani Serikali imejipanga sasa hivi kupambana na vyanzo vyote vya ulaji ambavyo vilikuwa vimejitokeza. Sasa hivi Serikali inajitahidi kwa kadiri iwezekanavyo, kuunganisha nguvu katika Wizara zote ambazo zina suala la kukusanya mapato, zinashirikiana sasa hivi kimkakati kuhakikisha kuwa zile njia zote ambazo zilikuwa zinavujisha mapato ya nchi kuingia katika mifuko isiyostahili zinazibwa. Imeanzia huko, itakwenda Wizara ya Fedha na Wizara zingine zote, mmesikia juhudi ambazo zimefanywa na Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, kila mahali sasa hivi Serikali imejizatiti kuhakikisha kuwa, mapato hayatavuja tena na hatua zitachukuliwa kama inavyostahili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ushirikiano wenu Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wawe na imani na sisi kwa sababu kazi inayofanyika inaonekana.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kuna wafanyabiashara wakubwa na wawekezaji wakubwa ambao wamekuwa wakikwepa kulipa kodi na kubadilisha makampuni yao. Je, Serikali ina mikakati gani kuwadhibiti hawa Wafanyabiashara wakubwa na Wawekezaji wasiolipa kodi kuwachukulia hatua za Kisheria?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafanyabiashara wakubwa, wawekezaji na hata wafanyabiashara wadogo wanaotambulika kuwa wanakwepa kodi, wanapotambulika wanatozwa faini, wanalipishwa kodi inayostahili na Serikali bado iko makini kuhakikisha kuwa wanawafuatilia. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine wote, pale mtakapokuwa mna taarifa au fununu yoyote kuwa kuna mfanyabiashara ambaye halipi kodi, tafadhalii sana milango yetu iko wazi, karibuni mtupe taarifa hizo tutazifanyia utafiti na itakapodhihirika kuwa ni kweli basi tutachukua kodi yetu.

Na. 114

Kukifufua Kiwanda cha Zana za Kilimo (ZZK) Mbeya

MHE. ALIKO N. KIBONA aliuliza:-

Kiwanda cha Zana za Kilimo cha ZZK, Mbeya kilikuwa tegemeo sana kwa Wakulima wa Mbeya na Tanzania kwa ujumla hususan katika zana za kama matoroli, fyeko, majembe, mapanga mashoka na kadhalika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukifufua Kiwanda hiki muhimu sana kwa Uchumi wa Taifa ikiwa pia ni utekelezaji wa Kaulimbiu ya KILIMO KWANZA?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ilaje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali haina mpango wa kukifufua Kiwanda cha Zana za Kilimo cha ZKK Mbeya, ambacho hapo awali kilikuwa tegemeo sana kwa Wakulima wa Mbeya na Tanzania kwa ujumla. Aidha, Kiwanda hiki kilibinafsishwa kwa njia ya ufilisi mwaka 2002 kutokana na mtaji mdogo waliokuwa wamewekeza, utendaji usioridhisha wa kiwanda na deni la Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *CMG Investment*, inayomiliki Kiwanda hiki kwa sasa ilifanya tathmini kwa lengo la kukifufua ili kuendelea kuzalisha zana za kilimo, lakini tathmini iliyofanywa na mwekezaji huyo ilionesha kuwa, faida isingepatikana kama angeendelea kuzalisha zana za kilimo. Hii inatokana na changamoto zilizokuwepo hapo awali, ikiwa ni pamoja na teknolojia kupitwa na wakati, ukosefu wa malighafi, yaani chuma kwa wakati huo, gharama za usafirishaji wa malighafi kutoka Dar es Salaam hadi Mbeya pamoja na ushindani wa biashara hasa baada ya zana nyingi za kilimo kuanza kuingizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya tathmini hiyo, mwekezaji huyo aliomba kibali cha kubadilisha biashara na sasa anatarajia kuanza uzalishaji wa bia aina ya Serengeti. Aidha, mwekezaji huyo ameona kwa kuzalisha bia atawez kutoa ajira nyingi kwa Wakazi wa Mbeya na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Serikali kupitia kodi atakazolipa. (*Makofii*)

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na majibu niliyopewa. Sababu ambazo zimetolewa hapa kwamba, mwekezaji yule ametoa sababu kuwa gharama za kuzalisha vifaa vyta kufanya shughuli za kilimo ni kubwa kwa sababu malighafi haipatikani nchini, na kama ikipatikana kutoka nje gharama ni

kubwa kutoka Dar es salaam kwenda Mbeya siyo za kweli kwa kipindi hiki kwa sababu tayari nchi yetu imepata neema ya kupata chuma kule Liganga Ludewa:-

(i) Je, kwa sababu hizo Serikali ipo tayari sasa kwa kuwa gharama za kuzalisha majembe na vitu vingine ni nafuu, kumkatalia mwekezaji huyu aelekeze kutuzalishia zana za kilimo kama alivyoomba kuwekeza mwanzoni?

(ii) Miaka ya 1985 mpaka 1990 na kuendelea, Watanzania tuliaminishwa kuwa hatuwezi kusimamia viwanda vyetu na Mashirika yetu na kwa hiyo mashirika yetu yaliuzwa kwa wawekezaji ambao wengine wameshindwa kuendeleza. Tunao Watanzania ambao wameonesha wazi kuwa wanaweza kufanya kazi ikaonekana; kwa mfano tuliuona kwa ndugu zetu; Mheshimiwa Mwakyembe aliyefanya kazi kubwa na Watanzania wote wameiona na Mawaziri wengine, orodha ni ndefu. Je, tunaweza sasa kubadilisha au kurejea nyuma ili tuangalie upya Sera yetu ya Uwekezaji maana tayari tunao Watanzania wanaoweza kusimamia Mashirika yetu? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kibona, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, inabidi nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa kufuatilia sana zana za kilimo katika Mkoa wa Mbeya na hususan Tanzania nzima kwa ujumla. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kuwa, hapo awali chuma kilikuwa ni tatizo, kwa hiyo, ndiyo maana kile Kiwanda cha ZKK Mbeya kilikuwa kabisa kwa sababu ya kushindwa kupata malighafi hiyo. Kwa kuwa hivi sasa chuma kimeanza kupatikana na bado hatujaanza kuchimba kule maeneo ya Liganga kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge; kwa sasa tujaribu kuangalia wawekezaji wengine ambao wanaweza wakajitolea kufanya kazi hiyo, kwa sababu chuma sasa kinapatika katika eneo la Liganga, ambalo ninaamini kwamba ni jirani sana na Mbeya kama kilomita 200 hivi, kwa sasa hivi inawezekana. Ushauri

ambao ameutoa kuwa wawekezaji wengine waweze kujitolea, tunauchukua na tunaufanyia kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, unaweza kutusaidia, hoja ya msingi hapa ni kuwa je, tuna uwezo wa kubatilisha hayo matumizi kutoka uzalishaji wa bia kurudi katika uzalishaji wa zana za kilimo? Kwa sababu hicho ndicho kipaumbele chetu, sasa ukilinganisha bia na zana za kilimo, labda Mheshimiwa Waziri wa Viwanda.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swalı lako la nyongeza na kuendeleza majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Suala la msingi hapa ni kwamba, uanzishwaji wa Kiwanda cha Kutengeneza Zana za Kilimo kwa miaka ile ya 1990 na 2000, ulipatikana na matatizo ya ukosefu wa malighafi hasa chuma na kutokana na hali hiyo, Kiwanda hakikuweza kufanya kazi vizuri na ndiyo maana kilishindwa kikawa na madeni na kikafilisiwa. Vilevile mpaka sasa hivi Kiwanda kile hata kama tutakianzisha, maana yake ni kuwa kinahitaji uwekezaji mkubwa kutokana na mabadiliko ya teknolojia yaliyojitekeza wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupata chuma cha Liganga, chuma ambacho mpaka sasa bado hatujaanza kuchimba, maana tunasema kuwa ikiwa chuma kile kitachimbwa na tutakipata, inawezekana ikawa ni malighafi nzuri sana katika Mkoa wa Mbeya katika kuendeleza hicho Kiwanda cha Zana za Kilimo. Sasa hivi yule mwekezaji kwa sababu ya kushindwa kuendeleza uzalishaji wa zana za kilimo, pamoja na sababu tulizotoa, ndiyo maana yeye akaamua kuzalisha bia kwa kushirikiana na Kiwanda cha Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kusema kuwa hiyo ni *priority*, lakini kutokana na changamoto ya malighafi inayohitajika kwa Kiwanda kile na hasa kuitwa kwa teknolojia, ndiyo maana ameamua kufanya hivyo. Hatufanyi kuwa bia ni *priority*, lakini zana za kilimo ni *priority*. Changamoto ni hizo ambazo ni lazima zifanyiwe

kazi na tukipata mwekezaji tuone ni jinsi gani tutaendelea na hasa kwa kutegemea chuma kitachopatikana Liganga na Mchuchuma. (*Makof*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mbeya na Mikoa mingi nchini hasa ya Nyanda za Juu Kusini ni Mikoa ya Kilimo. Kufa kwa Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya kumesababisha vifaa hasa zana za kilimo kuwa na bei kubwa sana. Serikali sasa pamoja na kutuambia kuwa kuna vifaa vingi vya zana za kilimo vinavyoagizwa kutoka nje vya bei nafuu; lakini je, Serikali itakubaliana na mimi kuwa zana za kilimo zimekuwa na bei kubwa na hivyo kuna kila sababu ya kuhakikisha kuwa inaharakisha kujenga viwanda vya kilimo nchini vitakavyozalisha zana za kilimo na kuhakikisha kuwa kinawapa nafuu Wananchi hasa Wakulima katika nchi hii?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoptana na mkakati tuliuweka katika viwanda, mkakati unganishi kwa maana ya *Integrated Industrial Development Strategy*, moja ya eneo lilitiliwa umuhimu sana ni uanzishwaji wa viwanda ambavyo vitaendeleza *value edition* katika nchi. Ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa, moja ya eneo ambalo tunalizingatia na kuli-focus ni lile la kutengeneza zana ambazo zitasaidia katika shughuli zetu hususan shughuli za kilimo.

Na. 115

Hitaji la Umeme - Kata za Kondoa

MHE. MOZA A. SAIDY aliuliza:-

Pamoja na Wilaya ya Kondoa (Mjini) kupata umeme tangu mwaka 1982 bado kuna Kata nydingi tu hazina umeme:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwafikishia Wananchi wa Kata hizo huduma hiyo ili kujipatia maendeleo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa inachangia uharibifu kwa kufanya Wananchi wakate miti ovyo kwa sababu ya kukosa nishati mbadala ya umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa kupeleka umeme kwenye Kata za Wilaya ya Kondoa (Mjini), ikiwa ni pamoja na Wilaya za Mpwapwa, Kiteto na Kongwa, ilifanya juhud ya kutafuta fedha ili kutimiza azma hii. Mradi huu utatekelezwa kupitia Mfumo wa MCC. Mradi huu umekabidhiwa kwa Mkandarasi *PIKE ELECTRIC CO. LTD* kutoka Marekani, ambaye alifanya kazi ya kusambaza umeme. Kazi ya kupeleka umeme kwenye Kata za Kolo, Mnienia, Pahi, Dalai, Mpango na Isusumia za Wilaya ya Kondoa pamoja na Wilaya zilizotajwa hapo juu ilioanza mwezi Juni, 2011 tayari imekamilika na Wananchi zaidi ya 100 wanafaidika na umeme huu. Aidha, Serikali kwa kupitia Wakala ya Nishati Vijiji (*REA*), imeingiza vijiji vifutavyo katika utekelezaji wa Miradi kwa Awamu ya Pili (*REA Turnkey Projects Phase II*): Kelelema Balai, Kingale, Kwadelo, King'ang'a, Iyoli, Haubi, Chungai, Cheke, Filimo, Masange, Kandaga, Itolo, Kisese, Disa, Busi, Itundwi, Jangalo, Mlongia, Itolwa, Mwakisabe, Tandala na Kifulukwa.

Kazi ya kupeleka umeme katika vijiji viliviyotajwa hapo juu inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33, urefu wa kilomita 392.2, njia njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4, urefu wa kilomita 123 na ufungaji wa transfoma hamsini na saba; kumi na nne za kVA 25, ishirini na na moja za kVA 50, kumi na tisa za kVA 100 na nne za kVA 200 ili kuwaunganisha wateja 2,766. Ghrama za Mradi zilikadiriwa kuwa Shilingi za Kitanzania 20,688,650,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni za kupata Wakandarasi kwa ajili ya kutekeleza kazi hizi imetangazwa mwezi Desemba, 2012 kuitia kwa Wakala wa Nishati Vijiji (REA) na ujenzi wa miundombinu ya Mradi huu unaotarajiwa kukamilika ndani ya miezi 24 unatarajiwa kuanza katika robo ya nne ya Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa utunzaji wa mazingira kwa kuwapatia Wananchi huduma ya umeme na ndiyo maana ina mikakati mbalimbali ya kuwafikishia huduma hiyo. Hata hivyo, tumnamwomba Mheshimiwa Mbunge, asaidie katika kuwaelimisha Wananchi wa maeneo ya Jimbo lake, kutunza mazingira hasa kwa utaratibu wa "Kata Mti Panda Mtii" wakati Serikali ikitafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Umeme Wilayani Kondoa.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, nashukuru kwa majibu yenyewe matumaini ya kuweza kuwapatia Wananchi hawa umeme lakini sijafahamu ni lini.

(i) Kwa kuwa Wilaya ya Kondoa ni ya muda mrefu, ina takriban Kata zisizopungua 48 na zilizokuwa na umeme mpaka sasa hivi ni Kata 15 tu labda na hizo zilizopo barabarani au Makao Makuu ya Mji. Hata pale katika Kata ndogo ya Kichangani, kilomita moja, umeme haujafika, kilomita kumi tu mpaka pale Tumbelo hakuna umeme. Je, Waziri unatuambia nini kuhusiana na hizi Kata zingine zote na Wilaya ulizozitaja ni lini basi watapata umeme huu ili wanufaikie kwa ajili ya maendeleo ya nchi yao?

(ii) Kwa niaba ya Watanzania wote na Wananchi wa Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Kondoa, kumekuwepo na malalamiko makubwa mno ya ongezeko la bili za umeme. Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kwenda kuongea na Wananchi hususan wa Wilaya ya

Kondoa ili kuepukana na adha hii nao waone kwamba wanatendewa haki katika malipo ya bili hizo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Naibu Waziri kutoka kuweka umeme mpaka kuangalia masuala ya bili.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini na hususan *TANESCO*, pamoja na Mifuko mbalimbali ikiwemo *REA* na Miradi mbalimbali ya *MCC*, *Electricity Five*, inaendelea kufanya jitihada kubwa za kupeleka umeme maeneo mbalimbali ya nchi hususan kwenye vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi kumsikia Mbunge akitaja Kata na Vijiji, inaonesha ni jinsi gani Wizara imejitahidi sasa kuondoka kwenye ngazi za Wilaya na kwenda kwenye ngazi za Kata na Vijiji. Nimhakikishie tu kama nilivyojibu kwenye swalii msingi, *REA* imekusudia kuanza Mradi huu katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13 na utakamilika ndani ya miezi 24, pindi taratibu zote za utekelezaji wa Mradi zitakapokuwa zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili kuhusu bili za umeme; bili za umeme kwanza zipo *centralized* Makao Makuu ya *TANESCO* na mfumo ni mmoja tu na hakuna bili ambayo ni mahususi kwa Watu wa Kondoa wala bili mahususi kwa Watu wa Shinyanga. Kwa hiyo, ninachoweza kumjibu Mheshimiwa Mbunge ni kuwa, vile viwango vya *tariff* vinatumika maeneo yote ya nchi na kwa maeneo ya Kondoa kama kuna makosa ya kiufundi yanajitokeza, nimuahidi tu sasa tutaagiza Wataalam wetu wachunguze ili kama kuna makosa yoyote ya kiufundi, tuweze kuyarekebisha na Wananchi wasitozwe bili kubwa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swalii linalofuata, muda umekwisha tumbakiwa na dakika tano kama mnavyoona na maswali bado yapo manne. Naomba nimwite sasa Mheshimiwa Donald Kelvin Max.

Kutatua Matatizo ya Wachimbaji Wadogo wa Madini

MHE. DONALD K. MAX aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitoa ahadi nyingi za mara kwa mara za kutatua matatizo ya wachimbaji wadogo wadogo wa madini ili wasilingiliane na wawekezaji wakubwa lakini hadi sasa ni takriban miaka minane na hakuna kinachofanyika zaidi ya Viongozi wa Serikali kuendelea kuwasumbua wachimbaji hao:-

Je, ni lini Serikali itamaliza na kutatua matatizo hayo yanayosababisha migogoro isiyo ya lazima hususan katika Wilaya ya Geita, Kata ya Mgusu na Kijiji cha Nyakabale?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya jitihada za kupatikana maeneo yanayofaa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili kuongeza tija na kujenga mahusiano mazuri na watumiaji wengine wa ardhi, ikiwemo kwenye maeneo yanayozunguka makampuni makubwa ya madini ili kuweka utaratibu wa kuruhusu uchimbaji mdogo kwenye maeneo ya leseni kubwa bila kuathiri wenyе leseni. Aidha, Serikali imetenga maeneo yaliyokwishafanyiwa utafiti wa awali na kurejeshwa na wawekezaji wakubwa na kubainika kuwa mashapo yenye madini kwa shughuli za uchimbaji mdogo na wa kati ili kufanikisha azma hii. Wizara inashirikiana na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili kubainisha maeneo yanayofaa kwa uchimbaji mdogo na wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Sheria mpya ya Madini, Na. 14 ya Mwaka 2010, Kifungu namba 16(a) na (b), Wizara imetenga maeneo na kuwamilikisha Kisheria wachimbaji wadogo wa maeneo husika kadiri wamiliki wa leseni kubwa za utafutaji wa madini watakavyokuwa wakiacha nusu ya maeneo yao wakati wa uhuishaji (*renewals*). Kwa kuzingatia kipengele tajwa hapo juu, Wananchi wa Kijiji cha Nyakabale watapewa kipaumbele pindi maeneo yaliyopendekezwa kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo yatakapotengwa, ambapo jumla ya hekta zipatazo 1358.6 zimependekezwa kwa maeneo ya Kanza, Lwenge na Bukolwa, yaliyopo ndani ya leseni kubwa za utafutaji wa madini zinazomilikiwa na Kampuni ya *Geita Gold Mine Ltd.* Jumla ya hekta 2811.6 zimependekezwa Wilayani Geita ndani ya leseni kubwa za utafutaji za kampuni mbalimbali. Zoezi hili litaendelea kwa maeneo ya Chato, Nyang'hwale, Sengerema na Biharamulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara kwa kutumia Ofisi ya Madini ya eneo husika, inaendelea kutafuta na kumilikisha Wananchi wa Kijiji cha Nyakabale, leseni za kusaga mawe na uchenjuaji wa dhahabu. Jumla ya leseni nne za aina hiyo, kati ya miradi 15, zimetolewa kwa Wananchi na Vikundi mbalimbali Wilayani na Mkoani Geita, vikiwemo Vikundi vya SACCOS za Wachimbaji wa Kata ya Rwanagasa na Nyarugusu, anapotoka Mheshimiwa Bukwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kuwaomba Watanzania wenzangu, Wadau wote hususan wale wa maeneo tajwa kuwa na subira na kuunga mkono juhudzi za Serikali katika kutafuta suluhisho la kudumu, kutatua matatizo yanayojitokeza na hatimaye kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

MHE. DONALD K. MAX: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi tena. Kwa niaba ya Wabunge wenzangu wa Geita na Wakazi wa Mkoa mpya wa Geita na Wilaya ya Geita, hayo matatizo ya uchimbaji madini hayajaanza leo. Kwa sababu kabla hatujapata

Uhuru, wachimbaji wadogo walikuwepo, miaka ya 30, miaka ya 40 miaka ya 50. Sasa kuna matatizo haya madogo madogo ambayo mara nyingi sisi Wabunge ndiyo tunaletewa. Kwa mfano, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikwenda naye Mgusu, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini nilikwenda naye Nayakabale. Mgusu tatizo lake limetatuliwa tulipokwenda na Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini vitalu mpaka leo havijapimwa, bado matatizo yapo pale pale.

Unapokuja kwa hawa wachimbaji wadogo sasa hivi wao wameshakuwa na taratibu mpya za namna ya kusafisha ile dhahabu badala ya kutumia zebaki sasa hivi wanatumia *cyanide* na *carbon*, lakini namna ya kuipata *cyanide* na *carbon* inakuwa ni shida. Matokeo yake wanatumia ujanja kuingia mle migodini, ndiyo maana mifarakano haiishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba, huyu Afisa Madini wa Wilaya au Mkoa apewe utaratibu wa kupata vibali ili hawa wachimbaji wadogo wajue wanaipata wapi *cyanide* na ile *carbon* ili haya matatizo yaishe. Kwa sababu wao wanachodai wanalipa *TMAA* asilimia nne.

MWENYEKITI: Swali Mheshimiwa Max.

MHE. DONALD K. MAX: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, haya matatizo tungakuwa tunapewa picha kwamba, kikomo ni lini kwa sababu haya mambo ya kwenda miaka minane, tisa, kumi inatuchosa? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Max, kama ifuatavyo:-

Nakubali kwamba, kwenye maeneo mengi ya wachimbaji wadogo, kuna migogoro ya hapa na pale ambayo Serikali inafanya jitihada kubwa za kuyashughulikia na kutafuta njia sahihi ya

kushirikiana na wachimbaji wakubwa. Napingana na hoja ya Mbunge ya kusema kwamba, vitalu katika eneo la Mgusu havijatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye madini hatuiti vitalu tunaita leseni na nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara ya Nishati na Madini, baada ya Waziri Mkuu kufanya ziara katika eneo la Mgusu na kuwaahidi kuwapa Wananchi wa Mgusu leseni katika eneo lililokuwa linamilikiwa na Mgodi wa Shanta, Wizara ya Nishati na Madini, iliweza kukabidhi leseni 20 na kukataa leseni moja kati ya maombi 21 ya Wananchi wa Mgusu waliokuwa wameomba Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, vitalu hivyo anavyoviita kwa maana ya leseni kwa Vikundi vya Ushirika vya Mgusu, Serikali imeshatekeleza na tulivikabidhi Geita na vilikabidhiwa kwa Wanakijiji wale na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Kinana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda hili swalii la pili la *cyanide*, teknolojia ya kutumia *cyanide* ni mpya kwa wachimbaji wengi wa Tanzania na Wizara ina mipango ya kuwaelimisha na tunaendelea kuwaelimisha wachimbaji wadogo maeneo mbalimbali ya nchi, namna nzuri ya kutumia *cyanide*, ambayo inaweza kupata dhahabu zaidi ya asilimia sitini ambayo iliachwa kwenye udongo uliosafishwa mara ya kwanza kwa kutumia *mercury*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili linaendelea maeneo mbalimbali, ikiwemo maeneo ya Geita, Shinyanga Kahama, Misungwi, Tarime na hata maeneo ya Chunya kwenye Kituo chetu cha Wizara kwa ajili ya kuwafundishia wachimbaji wadogo cha Matundasi. Tayari mpango huo unaendelea na wachimbaji wadogo wanaendelea kufundishwa matumizi mazuri ya *cyanide* na hasa kwenye kuzingatia utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, tunaendelea na jitihada za kutatua migogoro yote ya wachimbaji wadogo ukiwemo wa Senkenke ambao nitakwenda kesho kuushughulikia.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata, kama nilivyosema muda hauturuhusu.

Waheshimiwa Wabunge, Swali Na. 117 lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na swali hilo lilikuwa linahusu Ulipwaji wa Fidia kwa Wananchi wa Vijiji vya Litapwasi, Mpitimbi na Namatuhi, Muhukuru Barabarani na Nakawale waliopo kwenye Barabara ya Likuyufusi Mkenda kuelekea Msumbiji. Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, ndiye anayeongoza Kikao hiki leo, itakuwa ni maslahi binafsi kusimamia Mheshimiwa Waziri akijibu swali na mwuliza swali ndiye anayesimamia utaratibu wa maswali kujibiwa ndani ya Bunge. Kwa hali hiyo, kwa utaratibu wa Kikanuni na kwa utaratibu wa kawaida na kwa busara ya Kiti chake, ninaomba sana Ofisi ya Bunge, iliondoe swali hili leo na niwaombe radhi Wananchi wangu wasubiri swali hilo litapangiwa tena muda mwingine na Ofisi ya Bunge.

Kwa maana hiyo sasa tutaendelea na swali linalofuata ambalo litafulizwa na Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mbunge wa Viti Maalum.

(Swali Namba 117 liliondolewa na mwuliza swali)

Kupandisha Hadhi Barabara ya Njombe - Iyayi

MHE. NEEMA M. HAMID aliuliza:-

Je, Serikali itaipandisha lini hadhi Barabara ya kutoka Njombe - Iyayi yenye kilometra 71 kutoka Barabara ya Mkoa kuwa Barabara Kuu (*Trunk Road*) kwa kuwa ni kiungo muhimu kati ya Mkoa wa Njombe na Mbeya?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi inayapokea mapendelekezo ya Mheshimiwa Mbunge ya kuipandisha hadhi Barabara ya Njombe - Iyayi, yenye urefu wa kilometra 71 kutoka Barabara ya Mkoa kuwa Barabara Kuu. Hata hivyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge, apitishé mapendelekezo yake kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Njombe, ambayo kulingana na Sheria ya Barabara ndiyo humshauri Waziri wa Ujenzi, barabara zinazopendekezwa kupanda daraja na vigezo husika jinsi vilivyoainishwa kwenye Sheria.

Bodi ya Barabara ya Mkoa ikiridhia na kuyawasilisha mapendelekezo haya Wizarani kwangu, tutayafanyia uchambuzi kwa kuzingatia vigezo na utaratibu ulioainishwa kwenye Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za Mwaka 2009.

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri vile vile kwa ahadi aliyoitoa ya kuipandisha hadhi Barabara hii ya Njombe - Iyayi. Ningependa pia nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, swali dogo la nyongeza:-

Nataka kujua ni lini Serikali itaijenga Barabara hii ya Njombe – lyayi kwa kiwango cha lami ukizingatia kwamba Barabara hii inapitiwa na Vijiji vya Nyumba ya Nitu, Mlovera, Mdandu, Ruduga na lyayi ambavyo vina uzalishaji mkubwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mgaya, kwa kuwa na *interest* na Mkoa wa Njombe. Kwa sababu Mkoa wa Njombe ni Mkoa mpya na Mikoa mingine ambayo ni mipyä, tutaangalia suala la kuiunganisha na Mikoa mingine. Maana Barabara Kuu inaunganisha Barabara ya Mkoa na Mkoa mwengine. Kwa hiyo, Mkoa wa Njombe utakuwa na nafasi ya kuunganishwa na Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Songea na inaweza kukidhi vigezo vya kupandisha hadhi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ni Mkoa wa Ruvuma siyo wa Songea.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma. Kwa hiyo, katika Barabara Kuu zote, tumesema ni *priority* kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara zote zinazounganisha Makao Makuu ya Mkoa mmoja na Mkoa mwengine. Kwa hiyo, najua kabisa itakapopanda daraja barabara hiyo, suala la kujenga barabara ya lami litaangaliwa na Serikali.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la mwisho katika *Order Paper* yetu ya leo na ninaendelea kuwaomba radhi kwa muda, swali hilo linalizwa na Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge Mji Mkongwe. Namwona Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kwa niaba yake.

Wageni wa Kimataifa Kutembelea Zanzibar

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (K.n.y. MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA) aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini Viongozi kama Rais Bush wa Marekani, Rais Hu Jintao wa China, Rais wa Uturuki na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, walipotembelea Tanzania hawakupewa fursa na heshima ya kitembelea Zanzibar kama sehemu ya Muungano?

(b) Utamaduni wa Viongozi wa Nje kutembelea Zanzibar ulikuwepo mara tu baada ya Muungano, ambapo Viongozi wengi kama Rais wa Cuba, Algeria, Afrika Kusini na Waziri Mkuu wa India, walishatembelea Zanzibar; je, ni kitu gani kinaondoa utamaduni huo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ningependa kutoa maelezo ya utangulizi kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ndiye mratibu wa Ziara za Viongozi wa Nchi za Nje wanaotembelea nchini. Zipo aina tatu za ziara za Viongozi ambazo ni Ziara ya Kiserikali (*State Visit*), Ziara ya Kikazi (*Working or Official Visit*) na Ziara Binafsi (*Private Visit*). Katika Ziara za Kiserikali, nchi mbili husika, hupanga maeneo ambayo mgeni atatembelea. Aidha, katika Ziara za Kikazi na Binafsi, Mgeni husika hupanga maeneo ambayo angependa kutembelea akiwa nchini.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya Kiongozi wa Nchi kuwasili Nchini, timu ya awali hutumwa kutoa maelekezo ya maeneo ambayo Kiongozi husika atapenda kutembelea. Katika ziara za kikazi au ziara binafsi, Serikali haina maamuzi juu ya mgeni huyo atembelee wapi au asitembelee wapi. Kwa mantiki hiyo, uamuzi wa Kiongozi kutembelea au kutotembelea Zanzibar, upo mikononi mwa Kiongozi husika. Mfano mzuri, ni ugeni wa hivi karibuni wa mtoto wa Malkia wa Uingereza, ambaye alionesha nia kutembelea Zanzibar na Wizara ikafanya utaratibu husika na ugeni huo kutembelea eneo husika, tofauti na Viongozi wengine waliowahi kutembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugeni wa Rais Bush wa Marekani, Rais Hu Jintao wa China na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Bi Hilary Clinton na Rais wa Uturuki, Abdullah Gul, ulikuwa ni ugeni wa ziara za kikazi na hivyo, Wizara au Serikali, haikuhusikka moja kwa moja na uamuzi wa Viongozi hao kutotembelea Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la sehemu (b) halina tofauti na swali lilitangulia hapo awali. Kimsingi, hakujawahi kuwa na utaratibu na hakuna utaratibu unaomtaka Kiongozi anayezuru Tanzania kulazimika kuzuru na Zanzibar. Uamuzi wa kuzuru au kutozuru Zanzibar, uko mikononi mwa Kiongozi husika.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ambayo yamenipa wasiwasi kidogo, napenda kuuliza maswali mawili yafuatayo:-

(i) Sote ni Watanzania na tumekuwa tukishuhudia kinachoendelea tokea tumefanya Muungano tarehe 26 Aprili, 1964. Viongozi wengi waliokuja hapa katika nchi yetu wamepangiwa kwenda Zanzibar kwa sababu ile ni sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano. Ni sababu ipi sasa iliyosababisha Viongozi hawa hata katika Ziara hizi za Kikazi wasitembelee Zanzibar?

(ii) Hivi ni kweli Serikali yetu haina maamuzi juu ya Kiongozi anayekuja kwenye Ziara ya Kikazi katika nchi yetu wenyewe juu ya maeneo gani atembelee?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la (b), ni kweli taratibu za Kidiplomasia ni kwamba, Kiongozi hasa katika Ziara za Kikazi, anaeleza nia yake ya kutembelea nchi kwamba, ningependa kutembelea Tanzania na sisi tunatuma mwaliko. Tunatuma mwaliko nchi ile, Kiongozi yule anatuma watu wake wanakuja Tanzania, wanakaa wanakuwa wameshaona, kwa kutegemea mahusiano ya hizi nchi mbili, maeneo gani ambayo wangependa kutembelea. Kwa mfano, alipokuja Rais Hu Jintao; yupo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, zilifanyika jitihada za kuomba angalau atembelee Zanzibar lakini wakaomba kwamba, kwa mujibu wa ratiba ilivyo na kwa mujibu wa safari zilizopo ni kwamba, hawataweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi mwenyeji hauwezi kumshurutisha mgeni wako atembelee eneo katika Jamhuri yako ambalo anaona kwa muda wake, kwa mujibu wa ratiba yake, hataweza. Kwa hiyo, ni kweli inafanyika na hata sisi tunapoenda nchi nyiningine katika Ziara za Kikazi, tunakuwa tumeamua tutembelee maeneo gani na wenyehi wetu wanawezesha hiyo safari. Kwa hiyo, ni kweli hilo linatokea na ni utaratibu wa kawaida sana kwenye diplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo sahihi kusema kwamba, Viongozi wakubwa waliowahi kutembelea Tanzania, hawajawahi kwenda Zanzibar. Rekodi ipo kwamba, ni mara nyangi siku za nyuma Viongozi walitembelea Tanzania, pale muda uliporuhusu wameitembelea Zanzibar vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Muungano wetu ni kweli upo na upo imara, utaendelea kuimarika na hautatikisa kutokana na ziara na maamuzi ya Viongozi wa nchi nyingine kuchagua maeneo watakayotembelea katika Jamhuri yetu. Muungano wetu hauwezi kutikisa kutokana na maeneo ambayo wageni wanaamua kutembelea katika Jamhuri yetu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nilishatoa Taarifa muda hauniruhusu. Kama mnavyoona, tayari tunakaribia saa tano na leo ni siku ya kuahirisha Bunge; kwa hiyo, ninaomba tu mkubali tuendelee na ajenda nyingine ili twende na muda.

Nimepokea hapa viji-note kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wengi, wanauliza kwa nini maswali ya nyongeza haujatupa nafasi. Nadhani kama ningetoa hiyo nafasi tungeweza kwenda mpaka saa tano, ni kinyume cha Kanuni. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kuwaomba radhi, ni ushirikiano tu wa pamoja wa Kiti na muda kwa kweli leo haujatutosha.

Sasa, hapa ninayo Matangazo yafuatayo:-

Kwanza, nina Tangazo la Wageni walioko katika Ukumbi wa Bunge. Tunao Wanafunzi 80 na Walimu wanne kutoka Shule ya Msingi Michese Dodoma; ningeomba kama wako humu ndani wasimame. Nadhani labda hawajapata nafasi na watakuwa wamekaa eneo lingine. Basi kama wanatuona, tumetambua uwepo wao.

Tunao Wadau tisa kutoka *Kusini Utalii Festival*, ambao wapo kwa ajili ya kutembelea Bunge. Ningeomba hao wageni tisa kutoka huko Kusini, wasimame kama nao wako kwenye Ukumbi wa Bunge. Ni wale, wako hapo mbele yetu; karibuni sana, tunashukuru kwa kututembelea.

Tunao wanafunzi 60 kutoka *Jordan University, Anti-Corruption Union Morogoro*; ningeomba hawa wageni 60 kutoka *Anti-Corruption Unit Morogoro* kwa pamoja wasimame.

Tunawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri ya kutusaidia kupiga vita rushwa katika nchi yetu na kama vijana, tunawategemea sana. Karibuni sana siku nyingine katika Bunge letu.

Waheshimiwa Wabunge, tunao Wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Maendeleo ya Jamii; sijaambiwa hapa ni Chuo gani, lakini tunawakaribisha sana, maendeleo ya nchi yetu yanategemea sana fani yenu, karibuni sana. Naona hapa Waziri wenu na Naibu wake, wanawashangilia. Inamaanisha wanaelewa umuhimu wenu na sisi sote tunaelewa. Karibuni sana siku nyingine tena mje kushirikiana na sisi. (*Makofi*)

Tunao Wanafunzi watano kutoka Chuo cha Uhasibu Dar-es-Salaam; kama wapo wasimame. Wapo na wao wamekaa maeneo tofauti. Karibuni sana, tunawaona, karibuni sana.

Tunao wageni sita kutoka *Flight Link, Branch* ya Dodoma. Timu ya *Flight Link* kutoka *Branch* ya Dodoma, kama wapo na wao wasimame. Nadhani wamekosa nafasi ndani ya Ukumbi wa Bunge; aah wapo, karibuni sana. Tunatambua uwepo wenu na tunatambua shughuli zenu.

Wageni watano wa Mheshimiwa Augustino Masele, Mbunge wa Mbogwe, ambao ni Madiwani watano wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Wilaya, Mheshimiwa Masanja Maduhu. Ningeomba hawa Madiwani wasimame, wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti, Ndugu Masanja. Basi kama mko katika Viwanja vyetu vya Bunge, mtakuwa mnatusikia, tunaendelea kuwakaribisha katika Bunge letu.

Wageni tisa wa Mheshimiwa Ritta Kabati, wakiongozwa na Ndugu Sith Moto, Mkurugenzi wa *Majembe Auction Mart* na

Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Kilolo, Iringa. Tunaomba Mwenyekiti wa CCM asimame? Karibuni sana, ahsante sana.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Raya Khamis na Mheshimiwa David Silinde, yeye ni Ndugu Deogratius Siale Munisi, Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana CHADEMA; ningeomba asimame. Karibu sana Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana katika Bunge letu. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, huyu ni Mjukuu wake na anaitwa Farid Hamad Shamladi. Ningemwomba huyu Farid Hamid Shamladi asimame, Mjukuu wa Mheshimiwa Kapuya. Simwoni Mheshimiwa Kapuya, sijui ameshaenda Mtera na mjukuu wake. Tunakukaribisha sana Mjukuu wa Mheshimiwa Kapuya; yupo eeh? Aah, karibu sana Mjukuu wa Mheshimiwa Kapuya.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Titus Kamani, ambao ni wanafunzi kumi kutoka Chuo Kikuu cha Bugando Mwanza, wakiongozwa na Ndugu Ndatula Samuel.

Naomba wanafunzi kumi kutoka Chuo Kikuu cha Bugando wasimame, kama mko katika mazingira yetu ya Bunge, tunaendelea kuwakaribisha.

Nichukue nafasi hii kuwakaribisha na Watanzania wengine wote, ambao wanapenda kuona shughuli zetu za Bunge zinavyoendeshwa.

Matangazo ya Kazi Waheshimiwa Wabunge: Tangazo la kwanza, linatoka kwa Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali kuwa, leo tarehe 8 Februari, 2013, kutakuwa na Kikao cha Kamati, kuanzia saa tano kamili asubuhi katika Ukumbi Namba 231 uliopo Ghorofa ya Pili ya Jengo la Utawala.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dokta Augustine Mrema, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwamba, leo baada ya Kipindi cha Maswali na wao watakuwa na Kikao, Ukumbi Namba 227.

Vilevile Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, wakutane leo tarehe 8 Februari, 2013, kutakuwa na Kikao cha Kamati kuanzia saa tatu asubuhi. Nadhani hawa watakuwa wameshaanza hicho Kikao chao, Ukumbi Namba 219.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii na yeye anaomba Wajumbe wa Kamati yake, wakutane leo saa saba mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati, Ukumbi wa Pius Msekwa C. Kwa hiyo, Pius Msekwa C, Mheshimiwa Margaret Sitta na Wajumbe wake, watakutana hapo.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo Tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge; ninaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba, leo tarehe 8 Februari, 2013, kutakuwa na Tafrija ya Wabunge kuuaga Mwaka 2012 na kuukaribisha Mwaka Mpya wa 2013. Kutakuwa na burudani za vionjo mbalimbali, akiwemo Mwanamuziki Mkongwe, Mzee King Kikii. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mjiandae nadhani mambo huko leo yanaweza kuwa yako balaa kabisa.

Ninalo Tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge; nadhani na hili kwa kweli muhimu sana na ratiba ya tangazo hili, nadhani Waheshimiwa Wabunge mtagawiwa. Ninaomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, leo tarehe 8 Februari, 2013, kutakuwa na Uzinduzi wa Vitambulisho vya Taifa katika Ukumbi wa Msekwa, baada ya Kipindi cha Maswali. Nitaomba Waheshimiwa Wabunge, tutaelewana kidogo na Ofisi ya Katibu, kwa sababu kuna ajenda tunaendelea nazo hapa.

Baada ya Uzinduzi wa Vitambulisho vya Taifa, vitatolewa kwa utaratibu ufuataao:-

Vitambulisho hivyo nadhani atapewa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Wenyeviti wote wa Bunge, *Chief Whips* wote; wa Chama Tawala na Upinzani, Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Baraza la Mawaziri pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa hiyo, wote tunakaribishwa ili kuweza kuchukua Vitambulisho vyetu hivyo vya Taifa katika utaratibu uliopangwa.

Kwa kuwa hapa imeandikwa baada ya maswali na bado ratiba yangu inanionesha tunaendelea na kazi, kwa hiyo, Ofisi ya Bunge tutaendelea kuwasiliana nayo tujue kazi tulizonazo na tukio hilo muhimu tunaweza tukafanya saa ngapi na tutaendelea kuwapa taarifa. Niwaombe tu, mfahamu kwamba, tutakuwa na hilo zoezi muhimu sana hapa Bungeni katika siku hii ya leo na itakuwa ni siku ya kumbukumbu nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Selasini, naye ameniomba kwa niaba ya Bunge letu, Waheshimiwa Wabunge wote na kwa niaba ya Wananchi wetu tunaowawakilisha na Wananchi wote wa Tanzania, nitoe pia rambirambi kwa Kifo cha Baba Askofu wa Jimbo la Moshi, aliyefariki huko Nairobi jana alikopelekwa kwa matibabu. Huyu ni Askofu wa Jimbo la Moshi, aitwaye Amedeus Msarikiya, aliquwa Askofu. Kwa hiyo, Taarifa hii pia nimeipokea sasa hivi kutoka kwa Mheshimiwa Selasini. Kama hivyo ndivyo, basi ninaomba nichukue nafasi hii, kutoa pole sana kwa Baraza la Maaskofu Wakatoliki Tanzania, Wakristu wa Jimbo Kuu la Moshi, lakini vilevile na Wananchi wote wa Moshi na Watanzania kwa ujumla, kwa kifo cha huyu Kiongozi mwingine tena wa dini katika nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, hii taarifa nimeipokea hapa Mezani sasa hivi kutoka kwa Mheshimiwa Selasini.

Katibu, tuendelee na ajenda inayofuata.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mwongozo wa Spika.

MHE. MBUNGE FULANI: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wote waliowasha *MIC*, sitawapa nafasi ya kusema, wanakiuka Kanuni Namba 60, ambayo inatoa utaratibu. Aliyebakia ambaye hakukiuka taratibu hiyo ni Mheshimiwa Msigwa peke yake.

Mheshimiwa Msigwa!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68(7): "Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema..."; nadhani Kanuni inaeleweka Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuomba Mwongozo wako. Siku mbili zilizopita, Mheshimiwa Spika, alitangaza hapa kwamba, Hoja Binafsi zimeondolewa na mimi kama Mbunge, nilikuwa nimeandaa Hoja Binafsi, inayohusiana na Ujangili Uliokithiri Hapa Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kupata Mwongozo wako kwamba, hizi Hoja Binafsi, zimeondolewa moja kwa moja au tutaziletea utaratibu mwingine katika Mabunge yanayokuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, ahsante sana. Nafikiri maelekezo ya Spika, aliyoyatoa katika Kikao kilichopita baada ya kushauriwa na Kamati ya Uongozi, kwa mujibu wa Kanuni, ambayo ndiyo yenye wajibu wa kupanga Ratiba. Hoja Binafsi zilizoondolewa ni zile zilizokuwa zimepangwa katika Mkutano huu wa Kumi wa Bunge.

Sasa, katika Mkutano huu Mkuu wa Kumi wa Bunge, sikuona kama Hoja yako ilikuwa mionganini mwa Hoja hizo. Kwa kuwa haikuwa mionganini mwa Hoja hizo, ninaamini kabisa kwamba, utaratibu wa kuzipanga Hoja hizo tena katika Mikutano inayofuata, bado unabaki kwa mujibu wa Kanuni na kwa mujibu wa maelekezo ya Kamati ya Uongozi, ambayo imepewa madaraka ya kuweza kupanga Ratiba za Bunge. Kwa hiyo, sidhani kama una haja ya kuwa na hofu katika hilo, kwa sababu Hoja zilizoondolewa zilisimama kwa mujibu wa Hoja zilizokuwa zimepangwa kwenye Ratiba ya Mkutano huu.

Nimekuona Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Hamisi na mwisho Mheshimiwa Murji, halafu tutaendelea.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), ikisomwa pamoja na Kanuni ya 94, ambayo ninaomba kuisoma: "Ili kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Ibara ya 63(3)(c)..."

MWENYEKITI: Kanuni namba ngapi Mheshimiwa Mnyika?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 94.

MWENYEKITI: 94?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba inasema: "Bunge, litakaa kama Kamati ya Mipango katika Mkutano wake wa mwezi Februari ili kujadili na kushauri kuhusu mapendelekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha unaofuata."

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi tumekabidhiwa Orodha ya Shughuli za Leo, ambayo inaonesha kwamba, shughuli ya mwisho ya siku ya leo ni Kuahirisha Bunge. Katika orodha ya leo na orodha nyingine ya vikao vyote vilivyofuatia kwenye Mkutano huu wa Bunge, hakuna siku yoyote ambayo tumetekeleza matakwa ya Kanuni hii ya 94, ambayo inasema kabisa na imetaja mwezi kabisa kwamba, kwenye Mkutano wa Bunge wa mwezi Februari, Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango, kuishauri Serikali kuhusu Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi tumekuwa na malalamiko kuhusu Miradi ya Maendeleo na tungependa sana kabla Serikali haijakkamilisha Mpango wa Maendeleo ili kuhakikisha kwamba, bajeti inazingatia vipaumbele iwe ni vya maji na mambo mengine, ilipaswa tukae kama Kamati ya Mipango, tuweze kutoa mapendekezo kuhusu Mpango wa Maendeleo. Sasa ningependa kupata mwongozo wako ni kwa nini Kanuni hii ya Bunge imekiukwa na ni lini Kanuni hii itatekelezwa kwa sisi kukaa kama Kamati ya Mipango kutengeneza vipaumbele vya Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa John Mnyika. Mheshimiwa Hasnain Murji.

MHE. HASNAIN M. MURJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) inayosema: "Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika, alilieleza Bunge kwamba, ataunda Kamati Teule ya Bunge ambayo itakwenda Mtwara kuangilia hali halisi ya yaliyotokea huko. Kwa kuwa kulikuwa na Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Mbunge ambaye aliomba suala hili lijadiliwe Bungeni na hoja hiyo kutokupata nafasi, kutokana na kutokupata nafasi hoja hiyo kuzungumzwa Bungeni, Wananchi wa

Mtwara kwa heshima na taadhima, wanaomba bado Kamati Teule iundwe na iende Mtwara ikawasikilize.

Pamoja na kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alienda kama Serikali na Wananchi wanaomba Mhimili mwingine ambao ni Bunge, liende wakasikilizwe Wananchi wa Mtwara na wana matumaini makubwa sana na Bunge. Naona ya kuwa, hali ilivyo ni muhimu Kamati Teule iundwe na iende Mtwara kupata chanzo chote na ukweli wa mambo yote na kuepusha mgogoro mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa leo Bunge linaahirishwa, ningetaka kujua Kamati hiyo itaundwa lini na itakwenda lini kwani Wananchi wa Mtwara wanashubiri kwa hamu sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

MWENYEKITI: Ahsante. Wa mwisho ni Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1), ambayo inasema: "Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno "kuhusu utaratibu", ambapo Mbunge yejote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naitaja Kanuni ambayo ninahisi imekiukwa katika Mkutano huu wa Bunge na hii ni Kanuni ya 63(1) ambayo naomba noisome, fasili ya kwanza inasema: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge yejote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeje

mwenyewe anaamini kuwa ni la ukweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaisoma hii na kutaka Mheshimiwa Mwenyekiti, kulisaidia Bunge kwa kutoa hoja, hapo baadaye nitatoa hoja na nitaomba Waheshimiwa Wabunge, waniunge mkono ya kutaka kumwadhibu Mbunge mwenzetu mmoja kwa mujibu wa Kanuni hiyo hiyo ya 63(9)(a), (b) na (c), ambapo alisema uongo Bungeni na imethibitika kwamba alisema uongo huo. Mbunge huyu nitanukuu maelezo ya *Hansard* ambayo aliyasema: "*This book is written using curriculum developed and approved for the United Republic of Tanzania* ya Mwaka 2005. Naomba wanipe hiyo Mitaala ya Mwaka 2005 waliyoisema kwenye Bunge lako Tukufu iko wapi na wakiweza kuionesha hapa nitajiuzulu Ubunge wangu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia naomba wanipe hiyo mitaala ya mwaka 2005 walioisema kwenye Bunge lako Tukufu iko wapi na wakiweza kuionyesha hapa nitajiuzulu Ubunge wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu, lilipokea kauli hii kutoka kwa Mheshimiwa James Mbatia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, subiri amalize basi bwana.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako lilipokea kauli hii, sisi sote ni mashahidi tulisikia, Watanzania huko nje walisikia na Vyombo vyta Habari huko nje vikanukuu akisema mbele ya Bunge hili kwa kujiamini kwamba, yuko tayari kujiuza Ubunge aliopewa na Mheshimiwa Rais kutokea Ikulu kwamba atajiuzulu. Sasa Mamlaka ya Rais iliyomteua ni kubwa sana, Bunge hili ni kubwa na ni Tukufu sana na linaheshimika mbele ya macho ya Wananchi.

MWENYEKITI: Utaratibu gani sasa umevunjwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla?

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliovunjwa kwa mujibu wa Kanuni ya 63, fasili ya kwanza ni kusema uongo Bungeni na hapa ninasema kwamba imethibitika kwa mujibu wa ile Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Spika juzi. Kwenye Kiti hapo alikuwepo Mheshimiwa Naibu Spika, ikaenda kupitia Mitaala na Mheshimiwa James Mbatia akiwemo kwenye Kamati hiyo. Wakapitia Mitaala iliyowasilishwa kwa Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri na wakathibitisha kwa kusaini kwamba, Mitaala hiyo ilikuwa sahihi.

Kwa maana hiyo basi, imethibitika bila shaka yoyote ile kwamba, Mheshimiwa James Mbatia, alilidanganya Bunge; na kwa kuwa alilidanganya Bunge na akasema kwamba atakuwa tayari kujiuzulu Mitaala hiyo ikiletwa, ninaomba atumie uungwana yeye mwenyewe kusimama katika Bunge hili, aidha, kuwaomba radhi Watanzania kwa kudanganya ama kutimiza wajibu aliousema hapa yeye mwenyewe wa kujiuzulu Ubunge wake ambaa alipewa tu kutokea lkulu. Kama sivyo, basi ninaomba sasa Waheshimiwa Wabunge muwe makini hapa ninatumia Kanuni ya 63, fasili ya tisa, kutoa hoja ya kumtaka Mheshimiwa James Mbatia, aadhibiwe na Bunge hili Tukufu kwa kusema uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza niisome Kanuni yenyewe, hii ni Kanuni ya 63, fasili ya tisa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, sina muda sana nenda *straight*.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Ninasoma kipengele kidogo tu kinasema kwamba: "Endapo Mbunge mwingine ye yeyote ataona kwamba uongo uliosemwa na Mbunge huyo Bungeni ni mkubwa kiasi cha kuathiri heshima ya Bunge, anaweza kutoa hoja kwamba Mbunge huyo:-

(a) Ikiwa ni kosa lake la kwanza, asihudhurie Vikao vya Bunge visivyozidi kumi.

(b) Ikiwa ni kosa lake la pili au zaidi, asihudhurie Vikao vya Bunge visivyozidi ishirini.

(c) Achukuliwe hatua nyingine za kinidhamu zitakazotajwa katika hoja yake."

Mheshimiwa Mwenyekiti, uongo aliousema Mheshimiwa James Mbatia ni mkubwa sana na umeleta madhara. Sasa ninaomba nitoe hoja kwamba, Mheshimiwa James Mbatia, aadhibiwe kwa mujibu wa Kanuni ya 63, fasili ya 9(b), asihudhurie vikao visivyozidi 20 na (c) aombe radhi kwa maandishi kwa Watanzania kwa kusema uongo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Moses Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) ili kuweza kumpa taarifa mzungumzaji aliyemaliza kuzungumza, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, pamoja na Bunge lako Tukufu na Watanzania wote ambao wanatuangalia hivi sasa kwamba, Mheshimiwa James Mbatia, hakuzungumza uongo kutokana na ushahidi ambao hata mimi ninao ulikopitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; Waziri alilitaarifu Bunge hili kwamba, Mitaala ya sasa ambayo inatumika ndani ya nchi yetu ni ya mwaka 2005 na kwa mujibu wa Rasimu ya Mitaala ambayo tunayo sisi inaonesha kwamba, ipo Mitaala miwili ambayo imeandaliwa mwaka 2005, Chapa ya Kwanza mwaka 2012. Jambo ambalo nina-*justify* kwamba baada ya kuulizwa mwaka jana walianza kwenda kutengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; Rasimu hiyo ya Mitaala ambayo imesainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu, Dkt. Paul Mushi, imeandaliwa mwaka 2010 na Chapa ya Kwanza mwaka wa 2012 na ndiyo maana tukasema kitendo kilichofanywa cha kusema kwamba, wangewasilisha Mitaala tarehe 6 ya mwezi huu, ilikuwa ni suala la kwenda kuchakachua, kupika na hicho kilichowasilishwa ndani ya Bunge lako hatukuwa na imani na tuli-*declare* toka mwanzo, kwa sababu tunao Waraka wa Serikali. Kwa kuwa huyu Dkt. Paul Mushi ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Serikali, ambayo inahusika na masuala ya uundaji wa Mitaala ambayo inatumika kuanzia chekechea mpaka Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu, kwa mantiki hiyo hatuna imani na hata alichokuwa anazungumza Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwamba Mheshimiwa James Mbatia amedanganya.

Kwanza, waende wakaadhibiane wao wenye, wakamwadhibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu, kwa kutoa Waraka ambao sisi tunao na ambao bado ni Rasimu. Sasa nani mwongo nani mkweli na kwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa siku ile wakati anajenga hoja hapa alionesa akasema Mitaala hii hapa ilishindwa kuwasilishwa.

MWENYEKITI: Naomba tu kujua sasa unahama kwenye hoja kwenda kwenye hoja nyingine au bado unaendelea na taarifa?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, kwa kuwa siku ile Waziri alionesa ndani ya Bunge letu kwamba, Mitaala hii hapa na alipotakiwa kuiwasilisha alionesa wasiwasi mkubwa na kushindwa kuiwasilisha. Hali iliyopelekea kwamba, alichotuonesha ilikuwa ni usanii mtupu na ndiyo maana tukasema hatuna imani naye. Kwa hiyo, hiki walichokileta ndani ya Bunge letu, hiyo ni Mitaala ya kwake yeye, lakini sisi tunazo *documents* ambazo tunazo siku nyingi na Mtaala ulioletwa hatuna imani nao hata kama umewasilishwa kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaomba apokee taarifa hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla hawezi, hapana, hapana, naomba ukae, Waziri yuko wapi, mwenye taarifa hiyo? Anayetakiwa kujibu ni Waziri, ndiyo anayepewa hiyo taarifa. Waheshimiwa Wabunge mbona mnataka kunichanganya!

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuelewane; nadhani niende sasa moja kwa moja kwenye hii miongozo kusudi tumalize tuendelee na kazi, kwa sababu nikiendelea kuruhusu hapa tunaweza kutoka nje ya shughuli.

Mheshimiwa John Mnyika, umesema jambo la uhakika kwa mujibu wa Kanuni uliyoisoma ni sahihi na huo ndiyo utaratibu tuliojiwekea kwenye Bunge na ni kweli kabisa mwezi huu wa pili tulitakiwa kabisa Wabunge tukae kama Kamati ya Mpango.

Naomba nichukue nafasi hii, kukufahamisha Mheshimiwa John Mnyika, ukiwakilishwa na Viongozi ambao wanahuduria Kamati ya Uongozi wa Bunge, akiwemo Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani; Kamati ya Uongozi sasa hivi imekuwa na kazi ya kupitia mfumo mzima wa bajeti na kuona tunaweza tukarudi vipi na tukawa na utaratibu upi wa bajeti.

Sasa mfumo huo unaojadiliwa sasa hivi na kwa hakika kabisa unavunja Kanuni uliyoisema Mheshimiwa Mnyika na kwa sababu unakwenda kuvunja Kanuni uliyoisema, ninaomba mwongozo huu sasa niuchukue. Nina uhakika kabisa sasa hivi Kikao cha Kamati ya Kanuni kinaendelea na kazi na tutawasiliana nao kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Spika, kujua nini ambacho wanaliongoza Bunge baada ya kutokutekelezeka kwa majadiliano ya Mpango huu.

Niendelee kuwaambia Watanzania na wote wanaonisikiliza pamoja na wewe na Wabunge wote, Mheshimiwa Spika, alishatoa

taarifa siku ya *briefing* kwamba, Bunge letu sasa linakwenda kufanya mapitio ya mfumo mpya wa bajeti. Kwa hiyo, sina shaka kwamba, suala hili limekwenda likiingiliana. Kwa hiyo, maswali hayo ya lini na kwa namna gani, ninaamini kabisa kwamba, hayo yataambatana na maamuzi yanayokwenda kufanywa kwa sasa.

Mheshimiwa Hasnain Murji, suala la kuunda Kamati kwa mujibu wa Kanuni suala ambalo limekwisha kufanyiwa maamuzi katika Kikao cha Bunge hili, haliwezi kufufuliwa mpaka baada ya miezi sita. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika alishafanya maamuzi kwamba, hatounda tena Kamati ya Bunge akiwa hapa Mezani. Kwa hiyo, mimi kwenda kurudia tena suala hilo kwa kufanya maamuzi mengine, nitakuwa nakiuka Kanuni za Bunge, lakini kama unaona kwamba hoja hii bado ni ya msingi kwako, Kanuni zinakuongoza kuileta hoja hii kwa utaratibu mwengine, lakini si kwa maamuzi yaliyokwishafanya hapa mbele na Mheshimiwa Spika, nitakuwa nakiuka Kanuni. Kwa hiyo, nakuomba kama unaona suala hili bado unahitaji lifufuliwe, utatumia Kanuni zetu na utakuja kwa utaratibu mwengine.

Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla na Mheshimiwa Moses Machali, mmeinuka hapa wote mkilumbana jambo moja tu ambalo pia lilihafanyiwa maamuzi humu ndani ya Bunge. Maamuzi yalikwisha kufanyakia, kwa maana ya Spika kuunda Kamati na kuipa kazi Kamati ikafanye kile kilichotumwa na Naibu Spika hapa kwa maana ya Spika mbele ya Kiti, kwenye Kiti hiki na matokeo ya uchunguzi wa Kamati ile yalishawasilishwa ndani ya Bunge na Mheshimiwa James Mbatia, aliomba mwongozo jana akitaka kujua sasa anaweza kuunda hoja hiyo.

Sasa mimi naomba niseme yafuatayo: Kwanza, kwa mwongozo aliouomba Mheshimiwa James Mbatia jana, ye ye aliomba mwongozo na kwa mujibu wa Kanuni ukiomba mwongozo unaomba Kiti kikuongoze, huwezi sasa kutoa hoja ili kile ulichoomba mwongozo halafu kianze kujadiliwa; ni lazima Spika akupe sasa mwongozo wa namna gani hicho kinachokukera ndiyo kiletwe kama hoja ili kiweze kujadiliwa. Kwa hiyo, kwa Mheshimiwa James Mbatia ule mwongozo

uliouomba jana kama unaona una hoja tumia Kanuni, lete hoja hiyo kwa utaratibu sasa wa Kikanuni ili iweze kujadiliwa. Mwongozo uliouomba jana hauwezi kukuruhusu ulivyohitimisha kwa kuomba uungwe mkono ili hoja yako ijadiliwe. Kwa hiyo, hayo ni maamuzi kwa hoja ya Mheshimiwa James Mbatia.

Sasa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, kwenye suala la kujiuzulu Mbunge na hasa Mbunge huyo akiwa alisema yeye mwenyewe ndani ya Bunge, kwa mujibu wa Kanuni hizi hatuna kifungu ambacho kinawaambia Wabunge, huyo Mbunge sasa ajiuzulu. Kwa Kanuni hizi hakuna mahali ambapo panasema Kanuni hii sasa inasema Mbunge aliyetangaza humu ndani sasa ajiuzulu; hatuna, ila Mbunge mwenyewe anapoweka *commitment* ya kujiuzulu, anao uwezo wa kupima kwa haya yaliyojiri yanamfanya aendane na kile ...

(Hapa Wabunge fulani walikuwa wanazungumza)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

Alichokisema kwamba, sasa kwa haya yaliyotokea nijiuzulu ama nisijiuzulu.

Kwa hiyo, ipo mikononi mwa Mbunge mwenyewe, lakini sisi kama Bunge, hatuna mamlaka kwa mujibu wa Kanuni kumwajibisha huyo Mbunge ajiuzulu. Hatuna madaraka ya Kikanuni na wewe umekuja hapa na hoja ya kubadilisha adhabu aliyojtengenezea Mbunge ya kujiuzulu kwenda kwenye adhabu ya kumpa *suspension*. Sasa na wewe pia unakiuka Kanuni, kwa sababu aliyeomba adhabu aliomba kitu kingine na wewe unapendekeza kitu kingine; kwa hiyo, nafikiri Waheshimiwa Wabunge, katika suala hili kwa kuwa lilikwishakuamuliwa mimi nafikiri Mbunge aliyesema ajiuzulu atapima yeye mwenyewe na kama kuna mtu yeyote ana hoja zaidi kuhusu hoja hii ambayo tulikwisha kuifunga, ninaomba ailete kwa utaratibu mwingine, kwa kutumia Kanuni zetu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema haya, nisingependa tupoteze muda, ninaomba nimwite Katibu, tuendelee na kazi za leo.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2012 (*The Written Laws (Miscellaneus Amendments) (No. 3) Act, 2012*)

(*Majadiliano yanaendelea*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na jana tulimaliza mjadala wa Wabunge kwa pamoja, sasa tunampa nafasi Mwanasheria Mkuu, aweze kuhitimisha hoja yake.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba nikupe pongezi kwa maamuzi yako dhahiri, yanayoonesha kwamba, unaweza na wenzako wanaofanana na wewe wanaweza, pamoja na mke wangu pia anaweza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linahitaji maamuzi kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada huu jana. Jumla ya Wabunge 53 wamechangia Muswada huu kwa mawazo mazuri kabisa; Wabunge 20 wamefanya hivyo kwa kusema hapa Bungeni; na Wabunge 33 wamechangia kwa maandishi.

Wabunge waliochangia kwa maandishi naomba niwataje na niwatambue kwa majina. Ni Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mtemi - Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, aliyetoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana - Mwenyekiti wa Katiba,

Sheria na Utawala, Mheshimiwa Abdallah Amour, Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Prof. Anna Kajumlo Tibaijuka, Professa wa Uchumi; Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa John Momose Cheyo, *Doctor* wa binadamu Mheshimiwa Kebwe Stephen Kebwe, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mheshimiwa Subira Khamis Mgatu, Mheshimiwa John Shibuda Magalle, Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Mheshimiwa John John Mnyika na Mheshimiwa William Augustao Mgimwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao ni Wabunge 20 waliosema hapa Bungeni.

Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dkt. Wakili Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Namelok Edward Moringe Sokoine, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkyi, Daktari wa Binadamu na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareoso, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Profesa, Wakili huyu, Peter Mahamudu Msolla; Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Betty Elieza Machangu, Mheshimiwa Athumanji

Rashid Mfutakamba, Mheshimiwa January Yusuf Makamba,
Mheshimiwa Prof. Wakili Juma Athuman Kapuya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri na Wabunge wengine waliongea na mimi ambao hawakuleta michango yao kwa maandishi wala kwa kusema. Kwa kweli mazao yao na ushauri wao ni wa kujenga na kushauri sheria zetu.

Kwanza kabisa, ningependa kuanza kwa kutoa ufanuzi na elimu juu ya hoja iliyotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani wakati alipokuwa anawasilisha hoja kuhusu Muswada huu kwamba umeletwa Bungeni kinyume na kanuni za Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hiyo inadai kwamba uwasilishwaji wa Muswada huu ni ukiukwaji mkubwa wa kanuni 24 ya kanuni za Bunge. Mheshimiwa Msemaji huyo alihoji kama Mwenyekiti wa Kamati amewahi kumjulisha Spika kwa maandishi kwamba Kamati imemaliza kujadili Muswada huu na kwa kweli hili ni sharti la kanuni ya 85(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umefuata masharti yote ya kikanuni, pamoja na Mwenyekiti kumjulisha Spika na Spika kufuata sharti la 85(2) kwa uhakika.

Pili, kanuni ile ya 84 ya kanuni zetu ilifuatwa, barua za mialiko zilipelekwa kwa Taasisi sita. Taasisi ya kwanza ilikuwa ni Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. Barua ya kwanza ilikuwa ni Sheria ya Haki za Binadamu, barua ya pili ilipelekwa kwenye Chama cha Mabenki, yaani *Tanzania Bankers Association*, barua ya tatu ilipelekwa kwenye Chama cha Mawakili wa Tanganyika, Barua ya nne ilipelekwa kwenye Chama cha *NOLA*, barua ya tano ilipelekwa kwenye Kitivo cha Sheria cha Mzumbe, na barua ya sita ilipelekwa kwenye Chama cha Wanasheria Wanawake.

Katika Taasisi hizo, Taasisi iliyotoa majibu ni Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana kwamba kila wakati wamekuwa wakijibу hoja hizi na kutuandikia kuhusu marekebisho ya sheria tunayofanya. Taasisi hii safari hii ilijibу ikikubaliana na marekebisho haya tulioleta na kushauri katika maeneo mengine kwamba yaangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, siyo kweli kwamba Muswada huu uliondolewa Bungeni. Kilichoondolewa Bungeni ilikuwa ni Jedwali la Marekebisho ya Muswada huu ili kuipatia Kamati nafasi tena ya kujadili zaidi eneo la sita linalohusiana na marekebisho katika Sheria ya *Public Audit Act* na jambo hili liliwezesha Kamati kuzingatia ushauri mahsusи wa Mbunge Mheshimiwa Ndassa na Wajumbe wengine walioungana na ushauri huo kwamba kifungo kile kilikuwa hakijakaa sawasawa. Nitalielezea baadaye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, hakuna Kanuni yoyote iliyovunjwa na Mheshimiwa Spika, katika kukubali Muswada huu kuingizwa katika orodha ya shughuli za Serikali, hivyo siyo kweli na ni hoja isiyo na afya kwa kweli kumkashifu au kulaumu kwamba Spika analiendesha Bunge na kutoa maamuzi bila haki wala uadilifu au kwa hila na upendeleo kwa Serikali. Hoja hii haina uadilifu wa kibunge na angekuwepo ningemwangalia machoni hivyo hivyo. Haina msingi wa heshima ya Bunge na haizingatiii madili ya Kibunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Spika, asingeweza kuniamuru mimi mtoa hoja kuiondoa hoja na ndiyo maana Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa kutumia haki yake ya Kibunge ameendelea kujadili hoja ingawa allsema *under protest*. Kwenye kanuni zetu hakuna mahali ambapo Mbunge anaweza kujadili hoja *under protest* na huyu ni Mwanasheria na baada ya kufanya hivyo akatumia nafasi hiyo kwa mujibu wa kanuni ya 100 bila kuzingatia wajibu wake kama Mbunge na kama raia kuanza kukashifu watu wengine na mamlaka nyingine za dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kutoa ufanuzi huo, najizua kuzungumzia watu, nataka nzungumzie hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa ufanuzi huo naomba nianze kwa kujibu hoja za kisera za kijumla, na napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru sana Mawaziri; Mheshimiwa Anna Tibaijuka, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, ambao wamechangia hoja kwa kutoa ufanuzi katika masuala ambayo yaligusa sera zaidi kuliko hoja zenyewe zilizopo hapa. Hii ilitokana na michango iliyotoka kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la tofauti kati ya Mahakama na Mabaraza ya Ardhi nadhani lilliezwa vizuri na Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mheshimiwa Prof. Tibaijuka, Mheshimiwa Shekifu, Mheshimiwa Chana na Mheshimiwa Selasini. Naomba radhi kuwataja kwa jina moja.

Wengine ni Mheshimiwa Kombo na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, walichangia kuhusu eneo hili. Kwa kweli Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi nafikiri hoja hapa ni vizuri kujua, kuna maoni kwamba kuunganisha mifumo ya utoaji wa haki kwamba Mabaraza ya Migogoro ya Ardhi, yale yanayoitwa Mabarabaza na kwamba yanajumuisha pia kwamba Baraza ni Mahakama kimantiki; Mahakama, lile Baraza siyo Mahakama, ila linatoa maamuzi ya kimahakama. Sababu ya kuanzisha hii sheria mtakumbuka kama alivyosema Profesa, ilitungwa kwa lengo kuanzisha mfumo madhubuti wa kushughulikia migogoro ya ardhi nchini baada ya utafiti ule uliofanywa na Prof. Shivji, tumeitumia kwa muda huu. Sisi ni watumiaji wake na ninyi ndio mnafahamu kasoro zake. Ni vizuri, kama Wabunge maoni yenu yanapotolewa tutayazingatia.

Sasa kifungu cha tatu cha sheria hiyo kimeainisha utaratibu wa kushughulikia migogoro ya ardhi kwa kutaja kuanzisha vyombo mahsus i kwa ajili hiyo. Kwa mujibu wa kifungu hicho, vyombo hivyo vyote vinaitwa Mahakama. Neno hilo 'Mahakama' ndiyo msingi wa utata nafikiri uliotokea jana kwa vile kuna mtazamo kwamba Baraza, yaani *tribunal* ni sawa na Mahakama. Neno Mahakama limetafsiriwa katika sheria kumaanisha chombo kilichoanzishwa chini ya sheria yoyote. Pamoja na Mahakama zilizotajwa katika kifungu cha 167 cha Sheria ya Ardhi. Kifungu hicho kinafanana sana na kifungu cha tatu cha Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi, yaani *The Land Tributes Court Act*. Maneno yaliyotumika, "iliyoanzishwa chini ya sheria yoyote", yaliyopo katika fasili ya neno 'Mahakama' yanatupeleka katika Sheria za Mahakama za Mahakimu sura ya 11 ya sheria zetu toleo la 2002 ambayo kimsingi ndiyo iliyoanzishwa Mahakama na kwa mujibu wa sheria hizo, hakuna Mahakama iitwayo Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya au Baraza la Kata. Hivyo, siyo sahihi sana.

Kwa hiyo, ni uelewa tu. Kwa hiyo, naomba nikisema ni uelewa kusema kwamba Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi imeanzisha Mahakama. Kilichofanyika katika sheria hiyo ni kuzitaja Mahakama zilizopo na kuainisha vyombo vipya ambavyo kimsingi siyo vya Mahakama. Vyombo hivyo ni pamoja na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na Baraza la Kata, yaani *District Land and Housing Tribunal, and what tribunal?* Mahakama Kuu na Mahakama za Rufaa zenyewe ni Mahakama kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaani sura ya kwanza ya sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limejitokeza ambalo ni la kijumla, nitalisemea zaidi baadaye, ni kuhusiana na Wazee wa Baraza au Washauri wa Baraza na nimepata maoni ya maandishi, nimepata maoni pia kwa kusema na wengine pia tumezungumza nao jana jioni, wengine leo asubuhi, wengine leo Ofisini kwangu.

Waheshimiwa Wabunge, tunachofanya hapa, hatuwaondoi Wazee wa Baraza kwenye Mahakama, wanaendelea kuwepo. Lakini tunachosema Mheshimiwa Mkosamali, Mheshimiwa Rajab Mohammed, nafasi za Wazee wa Baraza, bado zipo. Marekebisho ambayo tunapendekeza na Waheshimiwa Wabunge ni mapendekezo. Marekebisho tunayopendekeza ni kwamba hawa wazeee waendelee kuwepo, lakini kwenye mashauri. Wahusishwe kwenye mashauri ya kimila, yaani kwenye *Customary Law* na mashauri yale yanayohusiana na dini ya Kiislamu. Ndivyo ilivyo sasa tofauti. Tofauti iliyopo ni kwamba, mapendekezo yetu hivi sasa wazee hao wawili wakitoa maoni yakatofautiana na Hakimu, maoni yanayofuata ni yale ya wazee. Sasa tunachosema, kwanini tunafanya hivyo? Tumefanya maboresho kwenye Mahakama zile, tunaweka Wanasheria ambao naomba mfahamu kwamba, tunao Wabunge wanasheria. Vyuo vyetu Vikuu vinavyofundisha Elimu ya Sheria vinafundisha elimu ya Sheria za Kimila, yaani *Customary Law* na nyiningine zinafundisha *Islamic Law* na wapo watu wamebobeaa katika Elimu ya Kiislam. Wengine ni Waaislam, wengine siyo Waaislam, maprofesa wapo! Sasa tunasema hawa watakapokaa kwenye Mahakama kwa kweli inakuwa taabu, huyu ambaye hana Elimu ya Dini kwa sababu hawa wazee wanavyochaguliwa huwezi kufahamu kwamba ana uelewa mkubwa wa Elimu ya Dini kuliko yule Hakimu, hiyo ndiyo ilikuwa mantiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tutatoa mapendekezo, ninyi ndio watungaji wa sheria, hivyo tunasema kwamba inakuwa taabu sana, Daktari aliyesomea Uduktari kubanwa na maamuzi ya Daktari hao wa kawaida, wanaita sijui *auxiliary doctors*, inakuwa ngumu kidogo sasa. Labda mfano mwingine, kama *engineer* wa umeme abanwe na mtu aliyesoma umeme wa *VETA* au ambaye hakusoma umeme, lakini kwa sababu ya kutenda kazi zile kila siku akawa na elimu ya umeme. Kwa hiyo, hatuna dhamira wazi au hila au *virtual* kutaka kuonyesha kwamba tunaingilia masuala ya Dini ya Kiislam, siyo hapa na tumepeata marekebisho.

Nafikiri nimemsahau jina la Mheshimiwa lakini alisema kwa uchungu, lakini akasema tutaleta machafuko, mimi nikawa natikisa kichwa, siyo kwa sababu napinga hoja yako, mimi sijazoea, hili jambo kwamba watu wapinge kwa sababu tunaleta marekebisho haya, ni afadhali tuyafute kama hayafai. Kwa hiyo, hoja ni hivi, kila Mbunge anayo nafasi kwa kutumia kanuni zetu kuleta mapendekezo. Nimepata mapendekezo mawili kwenye enelo hili, nikiwataja Wabunge wawili, Mheshimiwa Kigwangalla na Mheshimiwa Jafo wameleta mapendekezo, wakati ukifika tutayaangalia. Sisi tumetoa maoni yetu, ni kwamba tulikuwa tunadhani hawa watu ambao wana Elimu ya Chuo Kikuu wanao uelewa na weledi katika masuala ya Sheria za Kimila pamoja na Sheria za Dini ya Kiislamu. Hiyo ndiyo ilikuwa *position* yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kutoa wasiwasi Watanzania wenzangu kutoka Makunduchi mpaka Tarime kwamba, hatuna hila kwa kufanya lolote kuondoa haki za imani za watu kwa kutumia sheria, haitawezekana na haitakuwa. Nia yetu ilikuwa ni hiyo na si nydingine. Mimi mwenyewe lazima nikiri kwamba kuna wakati na mimi nilisoma madrasa, nilisoma sikuendelea kwa sababu nilichokuwa nakitafuta nilikipata. (*Makofii*)

Kwa hiyo, labda niseme kitu kimoja kingine, ilivyo sasa, Hakimu au Jaji na mimi nimekaa na hawa wazee kwenye Mahakama Kuu, unapokaa na hawa wazee wakakushauri, ukitofautiana nao, lazima useme kwanini umetofautina nao. Usiposema, uamuzi wako unaweza kubatilishwa katika rufaa au kwa mapitio. Lazima useme kwanini, na lazima uandike wamesema nini. Labda tuseme kwamba Mheshimiwa Hakimu anayekaa na wazee hawa atatakiwa kutoa maelezo, ni kwanini hakuafikiana na maoni ya Wazee wa Baraza? Utafikiri kwamba mimi kwa maoni yangu Waheshimiwa Wabunge, maoni ya upande wa Serikali na wataalam wangu mahiri wa dini zote tumekubaliana kwamba *safety guard*, yaani ulinzi wa haki hii unabanza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba hili nimeandikiwa na Mwanasheria mahiri, mtaalam wa Dini ya Kiislamu, anasema katika misingi ya haki ya asili, yaani *rule of natural justice* inaelekeza kwamba pale unapotoa maamuzi, lazima utoe sababu ni kwanini umefikia maamuzi hayo? Sasa yako maneno ya kilatini hapa sitaki kuyasema, labda Mheshimiwa Selasini anaweza kuyaelewa na huu ni msingi katika dini zote, mnafahamu hata Mwenyezi Mungu alipotaka kumpa adhabu Hawa/Eva na mwenzake Adamu aliwapa nafasi ya kusikilizwa wakasingiziana, lakini alishawapa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, alipowafukuza Eden, alitoa sababu kwanini anawafukuza. Walisingiziana ni huyu mwanamke uliyenipa; mwingine anasema, ni yule sijui shetani, sijui nini; kwa hiyo, *safety valve* nyingine Waheshimiwa Wabunge, yaani ulinzi mwingine wa haki hii ya kidini ni kwamba ibara ile kifungu cha 20 kifungu kidogo (b) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu kinampa nafasi mtu ambaye hajaridhika na maamuzi kukataa rufaa katika Mahakama ya Wilaya. Kwa hiyo, ni *both ways* hata yule ambaye hataridhika na uamuzi ule unambana Hakimu atakataa rufaa.

Hata huyu ambaye hakuridhika na maamuzi ya Hakimu atakataa rufaa. Kwa hiyo, tunachosema *connection* ni *level*, hivi kweli Mheshimiwa wewe Mbunge unajua Jimbo lako vizuri, halafu anakuja Mwenyekiti wa Kijiji anakwambia mambo ambayo unafikiri wewe akisema basi, atakuwa msemaji wa mwisho. Inaleta taabu kidogo! Nazungumzia Mahakimu wahitimu wa shahada ambao pia wana elimu ya *Customary Law* na wana elimu ya Dini ya Kiislam.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa upande wetu sisi, hatuoni tatizo lolote kwa sababu maamuzi ya Wazee wa Baraza yakimfunga Hakimu, kuna *issue* ya nafasi na kufedheheka kwa Hakimu. Kwamba inakuwaje mnaniwekea sheria ambayo watu ambao siyo wasomi wanatifunga na mambo haya ambayo mnasema mnayaelewa na mimi nimeyasomea? Hiyo ndiyo hoja yetu. Ikiwa hivyo, kama Mheshimiwa Hakimu amefanya maamuzi, uamuzi wake siyo wa mwisho, bado kuna rufaa.

Sasa kuna lingine ambalo napenda kulizungumzia. Tunajizuia kwa sababu jambo hili lilishafika Mahakamani hapa na Mheshimiwa Spika Kaunda Kamati, Kamati ikapewa kazi, bado haijatoa majibu kuhusiana na Majaji wa Mikataba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Celina Kombani, jana amelielezea hili vizuri. Hakuna Majaji wa Mikataba na nam-*challenge* Mheshimiwa Tundu Lissu atuletee Mkataba wowote wa Jaji wa Mahakama Kuu, na ni vizuri afanye hivyo kwa sababu bado wako hai, afanye hivyo kabla hawajafa. Afanye haraka atuletee Mikataba hiyo, kwa sababu kuna tabia imezuka ya kutumia *microphone* ya Bunge kwa ajili ya kufanya siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya Bunge hili kudhalilisha mhimili wa Mahakama ni kubwa, kwa sababu watu wanawaamini mnachosema mpaka wafanye utafiti wajue ni uwongo, athari kubwa imeshatokea. Hakuna Majaji wenye Mikataba. Katiba inaruhusu Mheshimiwa Rais kumruhusu Jaji kuendelea na kazi. Mimi sijatumia neno mwongo kwa sababu mimi ni mstaarabu, mimi ni Jaji, hakutakuwa na tofauti na msema ovyo. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, nije sasa kwenye hoja mahsus. Hoja ya kwanza ni kwenye Sheria ya Udhhibit wa Fedha Haramu. Tunachofanya hapa ni kutafsiri maneno ugaidi. Tumeambiwa kwamba hatukufanya utafiti; hoja yetu haina maana, ni kweli inawezekana. Kwanza, kuleta hoja ya Sheria ya Kudhibiti na Ugaidi kwamba sababu ile tafsiri iliyoko kule inatosha, mimi nasema ni kweli. Mimi kama Mwanasheria, ni sawa, kwa sababu tunachofanya hapa ni kurahisisha usomaji wa sheria kwamba usihitajike kuwe na sheria mbili kama mwenzangu anavyobeba vitabu hapa ili asome sheria kwa aina moja. Kwa hiyo, ukibeba kitabu kimoja, kinatosheleza. Siyo unapakia vitabu kwenye Lori, unakuja navyo Bungeni hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Sheria hii inahusu fedha haramu na Sheria y Ugaidi ina mambo mahsusini yanayohusika kwenye sheria ile. Sasa hapa ni suala la uelewa tu. Ni suala la uelewa na vyema sheria na ndiyo msimamo wa wanasheria waendelevu, ni bora sheria iwe na tafasiri inayolingana na maudhui yake. Kwa hiyo, ndivyo tunavyofanya hapa Mheshimiwa.

Mheshimiwa Pindi Chana ametoa pendekeso zuri kabisa, kwamba tutoe tafsiri ya neno '*financing*', kwenye Sheria ya Ugaidi kwa sababu haipo. Ushauri ni mzuri, lakini hakika ni hivi, kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Ugaidi kinaainisha vitendo ambavyo ni vya kusaidia ugaidi kuwa ni pamoja na kutoa misaada ya kifedha na maana ya kutafsiri haya maneno, unatafsiri maneno yale ambayo ni ya kiufundi na neno '*financing*' liliyo sasa, siyo neno la kifundi. Linatumika katika lugha ya kawaida ya Kiingereza. '*Financing*' siyo neno la kiufundi. Lakini '*Financing Terrorism*' kwenye Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ilivyotafsiriwa, ni *technical*. Ni la kiufundi kwa sababu *terrorism* ni kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mansoor Shanif na Mheshimiwa Margareth Sitta walishauri kuwe na mkakati wa kudhibiti namna ya utumiaji wa fedha kwa njia ya simu. Ni mawazo mazuri sana, tumeyapokea na tunayafanyia kazi. Hili naomba kutoa taarifa kwamba tunafanya mchakato wa kutunga sheria inayohusika na mambo haya, yaani *cyber law*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, suala la tafsiri ya neno '*Ufadhilli wa Ugaidi*' urekebishwe na kupewa tafsiri nyingine. Tunashukuru kwa ushauri, lakini tungependa utuletee tafsiri hiyo. Kwa maoni yetu sisi tunaona tafsiri tuliyotoa inatosheleza.

Mheshimiwa Mnyika amesema maneno mazuri ambayo yanatuhimiza tuwe watu wa kuweza kuona mbele zaidi. Tulitunga sheria hii, hili jambo kwanini tulisahau? Mheshimiwa Mnyika ni vizuri kusema hivyo, lakini utungaji wa sheria ni kama ujenzi wa nyumba na vifaa viendavyo kwa maji, unahitaji ukarabati na ukarafati, ukarafati

kwa vyombo viendavyo majini na ukarabati katika vyombo ambavyo viko nchini. (*Makofii*)

Kwa hiyo, unahitaji kupaka nyumba yako rangi. Wakati fulani unahitaji kutoa tofali bovu na kuweka tofali lingine. Kwenye jambo la sheria hii, siyo Tanzania tu, hii ni sheria ambayo inahitaji kuangaliwa kila wakati, kwa sababu hawa wahalifu wanagundua na kubuni njia nyingine. Kwa hiyo, lazima na wewe uwe haraka. Kwa hiyo, inawezekana katika kufanya ukarafati ukasahau tundu au ukasahau nafasi katika nyumba. Kwa hiyo, tutakuwa tunafanya hivyo mara kwa mara na ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu hili siyo la *Attorney General*. Muswada unapoletwa hapa na wewe pia ni Mbunge na unatunga sheria, kwa hiyo, huwezi kumnyoshea kidole mtu yeyote.

Hii Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Mheshimiwa Tundu Lissu, tunamshukuru, ametembea mwendo mrefu, katika hotuba yake kurasa mbili zinaeleza tunacholeta hapa. Tunacholeta hapa ni kusema kwamba Mamlaka ya Mahakama inayataja hapa iwe ni Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya, ndio hivyo tunavyosema kwamba hizi kesi zinazohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu zisikilizwe na Mahakimu wa Mahakama za Mahakimu Wakazi na Mahakama za Wilaya. Ndicho tunachosema. (*Makofii*)

Sasa anasema hakuna sababu ya kufanya hivyo, kwa sababu Mahakama hizo zimetajwa kwenye sheria nyingine. Wazo ni zuri. Wazo ni zuri kabisa! Narudia, msingi wa marekebisho haya ni kurahisisha matumizi ya sheria ili kufanya rejea kuwa rahisi katika sheria mbalimbali.

Aidha, kile kifungu ambacho Mheshimiwa Tundu Lissu amekitaja cha 165 cha Sheria ya Kanuni na Mwenendo wa Mashitaka, haikuzuia sheria nyingine kutaja Mahakama zitakazohusika na kuamua kesi zinazotokana na sheria hizo, na narudia tena, ni vizuri tubadilishe tabia. Sheria zetu zisomeke kwamba ukisoma hii ukaenda

ukasoma ile, halafu jibu unalipata kwenye sheria ya tatu, unaona mwenyewe. Alizitumia kurasa mbili kutafuta iliko hiyo Mahakama, sisi tunaandika kusudi usitembee na vitabu vingi, utembee na kitabu kimoja tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Masoud Abdallah alisema, makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu hayawezi kutatulika kirahisi kwa sababu mipaka yetu iko wazi na hati za kusafiria hupatikana kwa njia zisizo halali. Ni wazo zuri. Hilo ni suala la utekelezaji. Sisi tunachosema ni kwamba wakikamatwa utekelezaji mzuri ukifanyika, washitakiwe kwenye Mahakama za Mahakimu Wakazi au Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Pindi Chana alisema, Serikali iweke utaratibu mzuri, Sheria ya Kudhibiti Usafirishaji Haramu wa Binadamu kwa njia ya *digital*. Haya, ushauri umepokelewa.

Mheshimiwa Ummy Mwalimu alisema, Mahakama wapatiwe elimu ya kusikiliza kesi za usafirishaji haramu wa binadamu. Ni ushauri mzuri sana. Nitoe taarifa tu kwamba hata mimi nilikuwa nafundisha hilo na nilikwenda Mariutius kwenye mambo ya SADC kwa ajili ya kuonyesha Mahakimu na Majaji namna ya kushughulikia hizi kesi za usafirishaji wa binadamu. (*Makof*)

Tatizo ni kubwa sana. Tatizo ni kubwa kuliko mnavyofikiria nyie, kwa sababu wengine ni watu wazuri, wamevaa suti kama mimi, ni vigumu kuwafahamu. Kwa hiyo, unahitaji mambo ya intelejesia, unahitaji fedha, unahitaji weledi na mambo kama haya.

Mheshimiwa Kombo alisema, makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu hayajapewa uzito na sheria haijaainisha ni Mahakama gani itashughulikia masuala haya. Hili ndilo tatizo tunalofanya. Tunasema, sasa Mahakama itakayofanya hivyo ni Mahakama za Mahakimu wakazi, Mahakama za Wilaya. Lakini tunakubali kwamba hii itakuwa ni vita kubwa.

Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, nakushukuru sana mama yangu. Yeye alisema, Makosa haya ya usafirishaji wa binadamu ni makosa makubwa na ni udhalalishaji wa haki za binadamu, hivyo yashughulikiwe na Mahakama Kuu. Wazo ni zuri sana. Ushauri wetu ni kwamba makosa haya yanaanza katika Mahakama za Wilaya au Mkoa na kwa kuwa zina mamlaka makubwa, wakati mwengine Mahakama hizo huongezewa mamlaka, yaani *extended jurisdiction* na Mahakama Kuu. Vilevile marekebisho haya yanaruhusu fursa ya kukata rufaa Mahakama Kuu, lakini *issue* ni, kwamba unakamatwa Horohoro, una watu unawasafirisha au watu wanakamatwa, sasa uwapeleke Mahakama kuu Kilimanjaro Moshi, ni mbali sana au Tanga ni mbali, lakini pale kuna Mahakama za Wilaya, kuna Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya, wanaweza kusikilizia kesi pale pale. Kwa hiyo, ndiyo maana yake hiyo, kwamba Mahakama zile zina uwezo unaostahili.

Issue nyininge ilikuwa ni Sheria ya Mahakama za Mahakimu. Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Christina Mughwai, Mheshimiwa Pauline, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Saada Salum Rajab na Mheshimiwa Ritta Kabati, wametoa maoni yao pale. Ni maoni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hili na niseme kwa ujumla kwamba Waheshimiwa Wabunge tunafanya marekebisho ya mfumo wa utoaji wa haki katika ngazi ya Mahakimu. Tunasema kwamba ngazi ya kuingia, na namshukuru Mheshimiwa Kombani aliposema jana, ngazi ya kuingilia katika Utumishi wa Mahakama kama Hakimu sasa itakuwa ni Mahakama za Mwanzo, utaanza kama Hakimu Mkazi (*Resident Magistrate*), Mahakimu waliopo na wapo ambao hawana *degree* mnawapeleka wapi? Mna mpango gani wa kuwaengua? Mna utaratibu gani wa kuwaondoa pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Mahakimu, kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma, wataendelea kuwepo na watakuwa *phased out* kama wakistaafu au wakienda kusoma.

Hadi sasa, kwa sasa labda nitoe taarifa hiyo, kuna Vituo vya Mahakama 1105. Hizo ndizo Mahakama za Mwanzo katika Vituo hivyo. Vituo 960 vinafanya kazi na vingine havifanyi kazi kwa kukosa majengo. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kwenye Halmashauri zenu. Sasa kwa ujumla kuna jumla ya Mahakimu 1002 kwa sasa kwa Mahakama za Mwanzo. Kati ya hao, 772 wana Shahada ya Sheria, wamejiendeleza na waliobaki ndio wenyе Cheti na Diploma, yaani wako 630. Kwa hiyo, tunaowazungumzia hapa, labda kwa kutumia tarakimu ni Mahakimu 630, hao ndiyo tunaowazungumzia.

Tunasema hawa hawatafukuzwa kwa sababu tuna mwongozo. Tuna Waraka wa Utumishi namba moja wa 2010. Mahakimu hawa wataendelea kufanya kazi katika Mahakama za Mwanzo hadi watakapostaafu na kuijendeleza.

Liko suala kwamba Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ana elimu kama Jaji Mkuu. Nasikitika! Walimu wa Vyuo Vikuu wanaofundisha Sheria, heshima ya Chuo inatokana na alumni, wale waliosoma katika Chuo kile (*Makofi*)

Kuna wakati nilitaka kurudisha Cheti changu cha Sheria kwenye Kitivo cha Sheria cha Dar es Salaam, kwa sababu niliudhika na jinsi ambavyo Walimu walikuwa wanabaka haki ya kusema. Nikasema, sikihitaji kwa sababu nina kingine. Nilifurahi kwamba Maprofesa wale walikuja tukazungumza, na wameacha. Kwa hiyo, mimi ni alumni wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo cha Sheria. Ninaamini katika heshima ya Chuo hicho, na unapozungumza hapa, Waheshimiwa Wabunge mlio ni Wanasheria humu ndani; umetoka *Open University*, umetoka *Tumaini University*, umetoka Mzumbe. Unapozungumza kama Mwanasheria, angalia sana ulimi wako. (*Makofi*)

Ulimi wa mtu una kalamu anayotumia, una ncha kali kuliko mkuki. Mamlaka za Mahakama haziko kwa mtu, *the court's jurisdiction is not on a person* na kalamu mnaosoma chukua notice, Mamlaka ya Mahakama iko kwenye Taasisi, siyo mtu. (*Makofii*)

Hakuna ugomvi kwamba kwa sababu *Primary Court Magistrate* anaweza akawa na *Masters* ya Sheria, kwa hiyo, maamuzi yake akitoa yatapingana na ya Jaji Mkuu. *What kind of reasoning is that!* Ninasikitika kama nilitoa elimu ambayo haieleweki, lakini Mamlaka ya Mahakama inatokana na Mahakama yenyewe, siyo mtu. Ndiyo maana ukija hapa unainama, humwinamii Spika, unaimamia Mamlaka ya Spika yanayoonyeshwa na hiki chombo ambacho sina hata nafasi ya kukishika. Hili jitu limekaa tu, lakini tumejenga tabia kwamba hii ndiyo ya Spika. Kwa hiyo, ninapozungumza hivi, wanasheria nawaomba, usizungumze kwa vidole, unapomwonyesha Spika hivi, ni utovu wa maadili ya Uwanasheria. (*Makofii*)

Sasa tunasema kwamba katika Mahakama za Mwanzo tuna categories mbili za Mahakimu. Hakimu ambaye hana Cheti, lakini katika utaratibu wa *ku-phase out* na Hakimu Mkazi, ndivyo tunavyosema. Ukienda pale Mahakamani uki-file kesi, kuna mtu anagawa majalada. Jalada halipelekwi kwa Hakimu, kuna mtu anagawa, hili liende kwa fulani, hili liende kwa fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ambayo siwezi kuipuuza kamwe, hoja ya uwakilishi wa Mawakili katika eneo hilo. Mahakama za Mwanzo ziko karibu na wananchi na wale ambao mmesoma vizuri kuhusu suala la *access to justice*, ambayo ni *dimension*, ni mkabala kwamba moja ya *access*, moja ya *dimension* hiyo ni *distance*, umbali kutoka kwa mtu, kwenda Mahakamani. Zile ndiyo Mahakama ziko karibu na watu. Watu wetu ni wanyonge, hawana fedha za kulipa Mawakili! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwambia hizo kesi zenyewe, Wakili atalipwa Shilingi ngapi? Unajua kwa Kanuni zetu sisi, Wakili anayetoza fedha kidogo, kinyume na utaratibu wa zile *schedule of payments*,

anafanya kosa! Siyo yule tu anayetoza sana, hata yule anaye *underrate* wenzake, ni kosa. Sasa tutasema hivi, hii itakuja baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, kwa sababu Mawakili, Mahakama hizi na Sheria ndivyo inavyosema, hazibanwi na mambo ya ufundi, jinsi unavyoleta makaratasi, mashtaka yale unavyoweka, haibanwi kama vile uko kwenye *District Court au Resident Magistrate Court*, unaweza ukaandika tu kwa mkono, hakwambii sivyo. Ukipeleka Mawakili pale, unaleta ufundi na *uta-complicate system*. Kwa sasa nilikuwa naomba Waheshimiwa Wabunge tukubali kwamba, kwa sasa Mawakili wasiende pale. Kwanza ni kwa sababu, sasa itakuwa vigumu kusema kesi hii iende kwa 'X' kwa sababu ana digrii na kesi hii iende kwa 'X' kwa sababu hana digrii.

Pili tuangalie mfumo wa fedha. Ukiwapeleka kule Mawakili, lazima na mimi unipeleke. Lazima! Sasa bado fedha mazonipa ni kidogo sana, lakini siyo ninyi, ni mapato yetu hayajatufikisha mahali ambapo naweza kujidai kupeleka Mawakili kila *Primary Court*, 1002.

Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba Waheshimiwa hivyo, kwamba kwa sasa tukubali mpaka hawa watakapokuwa *phased out*, tufikirie, lakini wazo la kutumia Mawakili kule siyo la kupuuza, ila sababu za kutowatumia zipo. Unaweza usikubaliane nazo, lakini ndivyo ilivyo.

Hili la kuingiza wasomi wenyewe digrii kwenye *Primary Court* haliathiri *hierarchy*, haliathiri mlolongo wa Mahakama. Nafikiri ni vizuri tujue hivyo. Mheshimiwa Moses J. Machali na Mheshimiwa J. Mnyika, hoja zenu mimi nazithamini sana, kwamba tungeweza kufanya wale wenyewe digrii tayari tuwape Mawakili, lakini sababu ninazosema ndiyo hizo, kwamba ukifanya hivyo, Mbunge wangu wa Ubungo na ile barabara yangu ya Kibamba naona inaleta taabu, fanya haraka. Usipofanya haraka itakula kwako. Nilikuwa nadhani kwamba ni vizuri tusubiri kwanza, lakini hoja ni ya msingi.

Hii hoja ya Mheshimiwa Deo K. Sanga ni nzuri, kwamba Serikali iwasomeshe wale ambao hawana hiyo digrii. Tunapokea ushauri na Serikali inafanya hivyo. Mpaka sasa wamekwenda hao 372, ni matokeo hayo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali kuhusu suala la nidhamu, kwamba kwa nini mliwaajiri hawa watu kabla hamjabadilisha sheria? Waliofanya hivyo, kwa nini wasiitwe Mafisadi! Loh! Jibu langu Waheshimiwa Wabunge, taratibu za kuajiri hazitekelezwi na sheria hii tunayoifanyia marekebisho. Kwa hiyo, hapakuwa na haja ya kufanya marekebisho katika sheria hii kwa sababu kwanza hawa wameajiriwa kama Mahakimu Wakazi. Haizui!

Waheshimiwa Wabunge, lakini mfahamu, mnasahau kwamba tumefanya marekebisho kwenye kada ya Mahakimu wa Wilaya; hivi sasa wamebaki sita tu, ni kada inayokufa. Hatukuleta mabadiliko hapa kwa sababu sheria ilikuwa haihitaji. Kwa hiyo, hii ni *process* hiyo hiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakimu hawa sasa wako wapi? Mahakimu hawa wanafanya *orientation* Idara ya Mahakama. Mhimili wa Mahakama umeanzisha utaratibu, na mimi niliufanya kwa wiki mbili. Unapoteuliwa kuwa Hakimu au Jaji, unatakiwa uende ukajifunze mambo fulani ya utaratibu, namna ya kuongea na wenzako, namna ya kuongea na watu wenyewe daawa Mahakamani, namna ya kuwa uliza maswali mashahidi, namna ya kuzungumza na Mawakili. Kwa sababu mkiona hapa tulivyo, mimi nikiwa kama Jaji, siwezi kumwonyesha mtu kidole namna hiyo. *I cannot!*

Kwa hiyo, hiyo ndiyo *orientation* na ninafikiri hata hapa Bungeni tunahitaji. (*Makofii*)

Kwa hiyo, hapa Mahakimu wanafaniwa *orientation*. Ni utaratibu ambao umeanzishwa na Mahakama, wanafanya *orientation* kwenye *District Courts* na kwenye baadhi ya Mahakama za Mwanzo.

Tufahamu pia, kwamba katika hizi Mahakama 1002, siyo zote zitakazopata Mahakimu hao. Kwa hiyo, ndiyo sababu nyingine ya kusema, hhaya mambo ya Mawakili, tusubiri kidogo.

Suala la lugha, tunachosema, hatukiondoi Kiswahili! Mheshimiwa Mkosamali, hatukiondoi Kiswahili. Kiswahili kipo, lakini kitumike na Kiingereza na sidhani kama Watanzania hawajui Kiingereza! Nafikiri Waheshimiwa Kiingereza ni Kiswahili cha Kimataifa. Mimi nafikiri kwamba kwenye Mahakama kuwe na hiyo *opportunity* kwa sababu kuna watu wengine wanakuja pale, lugha zote mbili zinaweza kutumika, lakini Kiswahili kitachukua nafasi kubwa zaidi. (*Makofii*)

Kwenye marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Mheshimiwa alinisaidia lakini rekebisho moja tu tunalofanya ni kuondoa *exclusivity* ya Kitengo cha Ardhi cha Mahakama Kuu, kusikiliza Kesi za Ardhi kusudi kila Jaji aweze kusikiliza, ingawa kuna maoni kwamba, Mheshimiwa Jasson Rweikiza amesema hatuna haja ya kuondoa. Tulishaondoa! Tulishaondoa mamlaka hayo ya *exclusive jurisdiction*, tulisahau tu hayo mengine. Mheshimiwa John Mnyika yuko sawa, labda hakuwa makini wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi itaendelea kuwepo, lakini tunachosema, jamani tupeni ruhusa Mahakama Kuu, Majaji wote waweze kusikiliza kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, sijui kama nitakuwa na muda; Sheria ya Ukaguzi wa Fedha za Umma, tumefanya nini jamani? *Let us have a fair playing fit* kwamba, CAG, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali anapowasilisha ripoti yake hapa, na Serikali iwasilishe majibu yake, kusudi mtakapokuwa mnazungumzia ile ripoti na kutoa madongo majibu yawepo. Ndicho hicho tu kinachofanyika.

Kwa hiyo, siyo kweli Mheshimiwa John Cheyo, mzee wangu, kwamba mimi Jaji, Mwenyezi Mungu kanijalia, Jaji - Mwanasheria Mkuu wa Serikali, niliondolee Bunge mamlaka ya kuhoji mambo ya Serikali! Hapana. Ninachofanya ni kwamba unapohoji, uwe na majibu hapa. Maana nyingine ya hii, ni kubana. Tunataka hawa watu mnaosema wamegoma kutoa majibu, itakuwaje watoe? Sasa tunawabana watoe, wasipotoa, tutamkamata Waziri wa Fedha, maana yake ndiye tuna mamlaka naye, wale hatuna mamlaka nao.

Kwa hiyo, Waziri wa Fedha atakapokuja hapa hana, mshikeni. Lakini nafikiri kuna nia siyo nzuri kwa upande mwingine, kwamba Mheshimiwa unatakiwa uwe na ripoti ya CAG, kusema fedha imeliwa halafu baadaye unasema utakuja kusahihisha, aah! Kumbe ile fedha haikuliwa! Halafu huendi sasa ukasema nilisema uongo. Wananchi wanaichukia Serikali! Sasa tutasema hapana. Tutakuwa na majibu yale, na ukiangalia kifungu kile kilivyorekebishwa, anawasilisha *concurrently*, sasa kama hakupata majibu, itakula kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia maneno hayo, lakini sidhani kama ni ya hakika sana, lakini maana yake ni kwamba atawajibishwa na Bunge. Nikazie kwamba, marekebisho haya yanalipa Bunge kuangalia yale madongo ya Mdhibiti pamoja na majibu ya Serikali kwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho ya Wastaifu, ya Watumishi wa Umma, mapendeleko yale ya Magereza nafikiri ni safi, kwa sababu katika kazi za Jeshi, umri katika kazi ya Jeshi ni muhimu na kazi unayofanya. Ile kada ya kwanza ambayo mmesema iongezwe kutoka miaka 55 mpaka 60, ni kada inayolinda wafungwa. Sasa ukilinda mfungwa lazima uwe na uwezo wa kukimbia kuliko yeye! Kwa sababu anaweza kukutoroka, ndiyo maana tunasema kwamba hiyo miaka tuliyofanya inatosheleza. Vigezo vinavyofanywa ni kwamba, aina ya kazi, afya, uzoefu, elimu, taaluma na uadilifu, hivyo ndivyo vigezo vinavyofanya kuongeza umri.

Kwa nini tusiajiri ajira ya Askari vijana, tunang'ang'ania tu hapa! Kwa kweli, sababu zipo ni kwamba Askari hawa wana uzoefu na ukiajiri wengine inabidi uwafundishe lakini kwa muda huo ni kweli kwamba tulifanya marekebisho kama haya katika sheria nyingine, Sheria ya Polisi na majeshi mengine, na tunachofanya sasa ni kuainisha tulivyofanya. Tayari Bunge lilishafanya hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni la Mheshimiwa Andrew J. Chenge, pamoja na Mheshimiwa Assumpter Mshama na Subira Mgusu. Nawashukuru kwa maoni yao waliyotoa, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria za Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali
wa mwaka 2012, [The Written Laws (Miscellaneous
Amendments) (No. 3) Act, 2012]**

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima ili tuweze kuitisha Muswada huu kifungu kwa kifungu na kuhakikisha kwamba sasa Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali utakwenda kurekebisha sheria zinazohusika.

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 4

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge waangalie kwenye Jedwali la Marekebisho, tunaomba kwamba ile C, ambayo sasa inasomeka: "*Any other Act constituting terrorist financing as provided in the Prevention of Terrorism Act* ambayo iko ukurasa wa nne wa Muswada, sasa kisomeke: "*knowingly solicits support for, or rendering financial support to a terrorist, group or entity which is associated with terrorist acts*".

Sababu ya kufanya marekebisho hayo ni kuondoa upana wa kifungu hicho na kuingiza jambo la msingi kwamba katika kufanya kosa, mambo mawili ambayo Walatini wanasema ni *actus reus* tendo lenyewe na *mens rea*. Kwa hiyo, kinachoingizwa pale, maneno "*knowingly*" yanaingiza dhamira kwamba usimwadhibu kama hakuwa na dhamira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake*)

Ibara ya 5

Ibara ya 6

Ibara ya 7

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 8

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tulichofanya hapa ni kupunguza maneno: "*or Resident*

Magistrate" after the word "Magistrate" appearing in paragraph (a) kwenye sheria inayohusika, yaani the *Magistrates Court Act*.

Kwa hiyo, ukisoma hapa kifungu hicho lazima kisomeke na kifungu cha sita cha Sheria hiyo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 9

MWENYEKITI: Tuanze na Mheshimiwa Selemani Jafo.

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho nimeleta marekebisho katika marekebisho ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ku-add neno "*Customary*" between the word "the", baadaye nikasema *remove the full stop and add the following words: "but, shall bound to conform with the opinion of the Islamic assessors on matter relating on marriage, divorce and inheritance."*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeleta mapendelekezo hayo? Ni kwamba, tunapozungumza suala la kisheria hasa katika dini ya Kiislamu ina taratibu zake. Sasa kitendo cha dini ya Kiislam, kuna watu wanatoa maoni yao kwa mujibu wa dini, halafu Hakimu aongoze maamuzi yake, lakini yasibanwe na utaratibu ambao dini imeshaeleza kwa mujibu wa sheria unasemaje. Naona hapa siyo sawa kabisa na ndiyo maana nimeleta marekebisho hayo kiasi kwamba watakapotoa mawazo yao kwa mujibu wa dini, sheria ile inatakiwa ifuatwe kwa mujibu wa waliota ushauri kwa mujibu wa dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nafikiri nimeelewaka, lakini hili suala ni nyeti, linahusu imani za watu, lakini tukubali kwamba tunatunga sheria. Sasa ilivyo kwenye mapendekezo ya Mheshimiwa Selemani Said Jafo, ni ubunifu, lakini matokeo yake ni kwamba utakuwa unatunga Sheria ya Kibaguzi, kwa maana kwamba kwenye mila hawabanwi, lakini kwenye mambo ya dini wanabanwa.

Sasa wale ambao sio Waislamu na sio Wakristo, bali wanafuata mila na wenyewe sijui kama wapo humu? Lakini na wenyewe watakuwa na songombingo. Mimi nafikiri kwamba Mheshimwa Jafo kama unasema ibaki hivyo hivyo kwamba wawe *bound* ni *better* kuliko hivi ulivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maelezo yangu ni kama nilivyoeleza kwamba mabadiliko haya, au hawa wazee wa Baraza ujuzi wao na uelewa wao wa dini ya Kiislamu inawezekana ukawa mdogo kuliko wa Hakimu. Mimi nasema kwamba situngi sheria, lakini natoa pendekezo tu na ninawashawishi, siwatongozi, ninawashawishi kwamba mkubaliane na mapendekezo ya Serikali kwa msingi kwamba tunatunga Sheria ambazo kila mtu atazifuata. Halafu jamani, unajua tugeuke, hali hii ya kudhani kwamba yule mzee atakuwa anajua *Quran* zaidi ya Hakimu kwenye masuala haya inawezekana ikawa taabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri na nawaomba Waheshimiwa Wabunge mkubaliane na mapendekezo ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo!

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapo ni makosa makubwa sana ambayo yapo na yanaendelea mpaka hivi sasa, na tuna kila sababu kusema kwamba kuna malalamiko ambayo watu kila siku wanayazungumza, ni malalamiko ya kweli. Mimi siamini eti kwamba Hakimu anaweza akajua vizuri Sheria ya Dini ambayo wakati mwingine haguswi na imani yake.

Lazima *a hundred percent* hapo kuna upungufu mkubwa sana na katika hili naomba tuelewe wazi kwamba tunapotengeneza Sheria, tunaitengeneza nchi yenyewe. Kuna masuala mengine yako very sensitive na umesikia watu wote wakitoa malalamiko kuhusu Mahakama ya Kadhi kwa sababu wanajua na hii sheria itawagusa Waislamu wenyewe, sio mtu mwininge nje ya Muislam. Sijaona Mwanasheria Mkuu anakwazika na nini katika hilo! (*Makof!*)

Naomba hoja yangu ibaki kama ilivyo! Ahsante!

MWENYEKITI: Mwanasheria Mkuu mara ya mwisho!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Nasita sana kugombana na Ndugu yangu Jafo, nasita sana na ninaona haya! Lakini kama ndivyo, kama ndivyo kwenye *drafting* ni afadhali tuchukue ile ya Mheshimiwa Kigwangwalla ili kuondoa huu ubaguzi wa Sheria za Mila na Sheria za Dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nasoma Sheria za Zanzibar, maamuzi ya Mahakama Zanzibar kwenye suala hili *authorities* au mamlaka zinazoheshimika ni zile zilizoamuliwa na watu ambao hawakuwa na imani hii na zinafuatwa.

Kwa hiyo, nakubali, lakini najua huu ni mchakato kwamba badala ya kukubali hii labda tuchukue ile ya Mheshimiwa Kigwangwalla. Nafikiri itakuwa *compromise* nzuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* nimekuona, lakini nitakupa nafasi kwa mujibu wa kanuni Na. 5 inayokipa mamlaka Kiti kufanya maamuzi kwa kuzingatia uzoefu wa maamuzi na Mabunge mengine. Naomba sasa nitumie mamlaka hayo kuruhusu sasa na hii *version* ya mabadiliko iliyoletwa na Mheshimiwa Kigwangalla niiruhusu isemwe hapa, halafu tutakapofanya maamuzi sasa tunaweza kufanya maamuzi tukiwa tupo sahihi zaidi.

Kwa hiyo, naomba hapa niwaarifu kwamba natumia kanuni Na. 5 inayonipa madaraka hayo na hatutaamua kwanza Hoja ya Mheshimiwa Jafo mpaka tuone tunapata *consensus* ya namna gani tukianza kuzungumza na ile ya Mheshimiwa Jafo.

Sasa nitamwita Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ili aseme ile ya kwake ya mabadiliko, anamaanisha nini. Pia nilimwona Mheshimiwa *Engineer Manyanya* anataka kuchangia na kama kuna mwingine mmoja au wawili nitawapa nafasi ili tuone namna gani tunaweza kwenda na AG kama anavyoshauri.

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla!

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Ya kwangu kwenye kipengele hicho...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Waheshimiwa Wabunge wengi tunafahamu vizuri lugha ya Kiingereza. Hebu isome kwa Kiingereza, halafu kwa manufaa ya Watanzania wanaotusikiliza nadhani pia inapendeza kama wakisikia kwa Kiswahili ni nini tunamaanisha.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Ya kwangu inasema kwamba:

"(7) In any proceeding in a Magistrates' Court in which any rule of Customary or Islamic Law is in issue or relevant, the Court shall, (kwa hiyo hapa nimeongeza neno shall) and when directed by an appropriate judicial authority, sit with an assessor or assessors, and every such assessor shall be required, before judgement, to give his opinion as to all questions relating to Customary or Islamic Law in issue, or relevant to the proceeding; and that in determining the

proceeding the Court shall be bound to conform with the opinion of the accessor.

Kwa hiyo, utaona tofauti yangu hapa *basically* ni *wording*. Kwenye hii *version* ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali anasema kwamba, "save that", lakini mimi nimetoa ile "save that" nimesema sasa: "it shall", nikimaanisha kwamba katika hukumu ya Hakimu kutafsiri ni taabu sana, katika hukumu ya Hakimu Mkazi ambapo jambo lolote lile la Kanuni za Kimila ama za Sheria za Kiislamu kama linahusika, Mahakama itaamua na kama itaelekezwa na mamlaka ya Kimahakama iliyo juu yake. Itakaa pamoja na *assessor* kwa maana ya Wazee wa Baraza na Wazee hawa wa Baraza watatakiwa kutoa maoni yao kuhusiana na jambo lolote lile lililopo katika Mahakama hiyo linalohusiana na tamaduni ama na mila za Kiislamu ambazo zinahusika na kwamba maamuzi yao yatachukuliwa kama uamuzi sahihi wa Mahakama husika. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Hamisi, tayari?

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta mapendekezo haya kwa kuzingatia sana uhalisia kwamba Mahakama inatakiwa ichukue pia mila na desturi za watu wa maeneo husika katika kufanya maamuzi yake. Sasa haiwezekani Hakimu akawa wa Kinyamwezi akazijua mila za Wayao katika maeneo yao na pengine zile mila za Wayao katika eneo lao ni sheria kwa pale kwao.

Vilevile inahusisha na sheria za Kiislamu. Hakimu ambaye hafuati mila na desturi za Kiislamu au hazijui Sheria za Kiislamu akaenda sehemu ambapo kuna Waislamu na wao wana sheria zao ambazo wanazifuata, akafika pale akatoa maamuzi yanayohusiana na Sheria za Kiislamu, inatia shaka sana kama atatoa maamuzi ambayo ni sahihi kwa sababu pengine hafahamu sheria za watu wale.

Kwa hiyo sasa, kuliko kwenda tu kuiga utaratibu wa Sheria za Kimagharibi ambapo hata kule kwao wanaziheshimu sheria za kimila, ni vizuri tukaiacha kama ilivyo, Wazee wa Baraza wakaachwa wakawepo na Mahakama zikaendelea kuwa kama zilivyo na hilo ndiyo kusudio la wasilisho langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Manyanya!

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwa mujibu wa michango inayoendelea na mapendekezo yanayoletwa, kwa heshima, kwa unyenyekevu na kwa hofu kubwa naomba nilichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo la kujua kwa nini wenzetu Waislamu wangependa isomeke hivyo. Lakini ninakuwa na hofu kwa sababu kwa mujibu wa Katiba iliyopo pale tumesema kwamba nchi haina dini, ila watu wake wana imani. Vilevile ninaanza kuona kwamba sasa kama tutakuwa tunaona tuiingize *Islamic Law*, naona Wakristo, hususan Wakatoliki tunazo sheria za aina hiyo, pengine nazo itabidi ziingie na pengine wakati katika kulitafakari hili suala kwa mapana, yavezekana ikawa haitoshi sana.

Lakini la pili, najaribu kuona katika mwingiliano tulionao sasa hivi, katika masuala ya ndoa, mimi ni shuhuda kwamba nimeshaona kuna watu wanaishi mume Mkristo au Muislamu na mke Muislamu au Mkristo na michanganyiko ya aina mbalimbali....

WAJUMBE: Aaaaaah!

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Naomba mnisikilize ili mu-argue vizuri baadaye.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Manyanya ongea na Kiti tu!

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mazingira kama hayo, nahofia kwa mfano inapotokea kuna suala linalowahukumu watu wenyewe mchanganyiko kama huo watachagua lipi? Kwa hali hiyo, nafikiria kwamba kwa sababu Katiba yetu inaturuhusu sisi tunapokuwa katika masuala ya imani zetu kwenda katika vyombo vinyo yohusiana na imani zetu na kwa sababu masuala hayo huwa yanaheshimiwa kufuatana na maamuzi yanayokuwa yametokana na vyombo vya imani yetu, nashauri kwamba ni vyema tukabakia kama ambavyo Mwanasheria Mkuu alikuwa ameileta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Rajab halafu Mheshimiwa Cheyo!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwanza nataka nimkumbushe dada yangu kwamba nchi hii inafuata sheria tatu, yaani za kimila, Kiislamu na zile za India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa AG kaonyesha lengo la kutaka au kukubaliana na hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla, nami nakubaliana nalo hili na ninampongeza sana Mheshimiwa AG kwa kulikubali hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *assessors*, awe wa kimila au wa kidini huyu wa Kidini hana ulazima wa kuwa na *PhD* wala kuwa na *Masters*, lakini kinachotakiwa hapa ni ule uelewa wake wa Sheria ya Kiislamu, Hadithi za Mtume na kujua *Quran* Tukufu yenyewe kuitafsiri kwa sababu tayari sheria zote za dini ya Kiislamu zipo, kinachotakiwa ni kufuatwa. Lah, kama Wabunge wenzetu mnahisi kwamba hii sheria na mapendekezo aliyojatoa Mheshimiwa Kigwangalla yana

matatizo, tuitoeni yote, tukubali kurejesha Mahakama ya Kadhi. *What is wrong?* Serikali mnagwayagwaya kitu gani? Turejesheeni Mahakama ya Kadhi tu, hili suala lote linakwisha kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cheyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Missanga na msemaji wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Machali.

Waheshimiwa Wabunge, tunatakiwa tufanye maamuzi!

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mimi tatizo nililonalo ambalo nilifikiri Mwanasheria Mkuu angetuongoza miaka yote na sasa tuna miaka 51, yule aliye kwenye Kiti ambaye ndiye Jaji na yeye ndiye anachukua majukumu yote ya uamuzi na wale *assessors* ni Wasaidizi wake. Sasa tukimfunga hapa kwamba analazimika kufuata yanayosemwa na *assessors*, sasa tumwondoeni *Magistrate* tumweke pemberi ili hili liwe Baraza la *Accessors* hata ukienda kufanya *appeal* waliokosea ni *assessors* na siyo Jaji ambaye yuko kwenye Kiti. *To me, tukileta haya mambo, it is extremely dangerous katika judiciary system yote.*

Hivyo basi, naomba busara itumike, miaka yote Jaji aliye kwenye Kiti ndiye mwamuzi. Tuendelee na utaratibu huo na umetufikisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii *subject* tukiigeuza tutakuwa tunawatendea watu mambo ambayo siyo haki.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Kwanza, nataka nimfahamishe Mheshimiwa Cheyo kwamba sheria ya sasa kama ilivyo katika Mahakama pale panapozungumzwa jambo katika Mahakama ya Mwanzo, *assessors*

wawili walikuwa wakikubaliana, lazima Hakimu au Jaji akubaliane nao. Hivi ndivyo ilivyo sasa na sivyo kama anavyosema Mheshimiwa Cheyo kwamba kwa miaka 51, Jaji ndiyo amekuwa akitoa maamuzi, hapana! Hivyo ndivyo ilivyo sasa ndiyo inataka kubadilishwa, ni kwamba pale ambapo ma-assessors wawili wanakubaliana, wanakuwa na msimamo mmoja, yule anakuwa *bound* kuwafuata hawa ma-assessor wawili. *This is how it is as at now for the last 51 years.* Nataka nimfahamishe hilo kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu jambo hili mbona Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameliona ni jambo nyeti ambalo linahitaji kutumia busara na ametuelekeza kwamba pengine tukubaliane na mawazo ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, ameona. Hivi sasa tuna mtafaruku mkubwa wa mambo ya kidini. Jambo hili ambalo ni dogo tena tunataka tuongeze kidonda au tuweke sijui msumari kwenye kidonda wakati ambapo hata hakuna sababu yoyote? Kwa miaka 51, sheria imefanya kazi vizuri wala hakuna sababu za msingi zilizolezwa hapa kwamba hawa ma-assessor wamevuruga kiasi gani katika kufanya kazi yao hiyo. Hilo la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu, mimi kama Serikali ingekuja hapa na mabadiliko ya sheria ya kusema kwamba sasa tunawaondoa ma-assessor angalau hilo lingezungumzwa vingine, ili mradi sheria bado inaendelea kuwatambua hawa ma-assessor maana yake wana umuhimu kuwepo pale. Sasa huwezi kusema kwamba kuna umuhimu wa kuwa na assessors halafu yale maoni yao wanayoyatoa yawe hayana maana, haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unaona mawazo yao hayana maana futilia mbali. Kama Serikali itakuja baadaye kusema kwamba jamani kwa sababu sasa tuna Mahakimu wasomi tunawaondoa ma-assessors hao kwa sababu hawakusoma, hilo litakuwa jambo linguine lakini maadam sheria bado inawatambua wako ma-assessors, kitendo cha kutambua kwamba kuna hitaji la kuwa na ma-assessors maana yake mchango wao ni muhimu. Kwa ajili hiyo, hatuwezi tena

kuji-contradict kusema kwamba tunawatambua wawepo lakini tusitambue yale mawazo yao, hiyo itakuwa ni *contradiction*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kama hoja ni Wazee wa Baraza hawakusoma, si tumeambiwa hapa tunakwenda kwenye mpito wa kuondoa Mahakimu ambao hawakusoma na kadhalika na kadhalika. Huko twendako Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa mstaafu, yule anaweza akawa Mzee wa Baraza. Mheshimiwa Chenge pale atastaafu, atakuwa Mzee wa Baraza, sijui Mheshimiwa nani huyu, Mwenyekiti wangu wa *UDP* pale, atakuwa Mzee wa Baraza. Kwa hiyo, suala la kusema kwamba wale Wazee wa Baraza hawakusoma, ni suala la mpito tu litakwenda kama *mnavyo-phase out* hawa wengine, huko twendako, Wazee wa Baraza watakuwa ni sisi ambao tunajua mambo hayo, pamoja na wewe Mheshimiwa Jenista, samahani, unaweza kuwa Mzee wa Baraza. Kwa hiyo, hilo haliingii kichwani la kusema kwamba tufanye kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na hoja ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwamba Hakimu yule anajua dini ya Kiislam kuliko yule *Assessor* ambaye ni Sheikh, haiwezekani! Hatusemi Missanga kama Mohamed, tunamzungumzia Sheikh, Maalim aliyebobea katika masuala ya dini ya Kiislamu, haiwezekani yeye awe hajui yule Hakimu anajua!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuipeleke nchi yetu hii katika utulivu na amani kama tunavyoambiwa siku zote, hili ni jambo dogo sana lisivuruge amani yetu sisi. Naomba tukubaliane na hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwamba ibaki kama ilivyo sasa. Hivyo anavyosema Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ndivyo sheria ilivyo sasa. Kwa hiyo, ibaki vilevile kwamba maadam Serikali inaona kwamba upo umuhimu wa kuwa na ma-assessors basi maoni yao nayo yawe *bound* kwa yule Mwanasheria.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, nchi yetu haina dini na wala haina ukabila. Napata wasiwasi mkubwa sana kwa nchi yetu ambayo ina madhehebu mbalimbali, ina makabila mengi, kuna Wabudha katika nchi yetu, kuna Wakristo wengi katika nchi yetu, kuna Waislam wengi katika nchi yetu na kuna Wapagani, watu ambao hawana imani. Sasa inapokuja *concept* ya kusema kwamba dhehebu fulani lionekane kwenye masuala ya kuendesha Serikali, kwenye chombo cha kutoa haki, tunaenda kuligawa Taifa letu. Mimi nasema na naomba *ni-declare*, ningependa labda pengine mwisho na sisi Wakristo wakati mwingine tuanze kudai mambo ya Wakatoliki yaingie huko, tutaligawa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watakuja Wabudha nao watataka kudai haki yao, watakuja Wahindu na *denominations* mbalimbali, Wakristo unajua kuna madhehebu mengi, kila mmoja ataanza kudai haki yake tuingize huko, tunaligawa Taifa letu. Watakuja Wapagani nao watakuja na imani zao wataanza kudai haki zao. Nashauri jambo lolote ambalo linahusiana na masuala ya kidini lisiingizwe kwenye masuala ya kisheria. Tuache Mahakimu, Majaji wafanye kazi zao kwa mujibu wa taaluma zao, wafanye kazi kwa mujibu wa sheria zilizotungwa na Bunge ambazo zina-*promote* misingi ya usawa bila ya kujali dini, kabila na bila kujali itikadi za vyama wala misingi yoyote ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tukiingiza kipengele hiki kwamba ma-assessor wa Kiislam waingie katika kutoa ushauri wakati wa kufanya maamuzi kwenye Mahakama zetu, kesho wataibuka Wakristo watakuja kudai haki hiyo, tulete tena mabadiliko hapa. Watakuja Wapagani tunazidi kugawanyika. Niombe kabisa kwa dhamira njema na kwa nia safi kama hakuna kitu kilicho jificha, suala hili utaratibu uwepo tu kwamba ubaki kama ilivyokuwa huko nyuma. Hakuna sababu hapa tutagawanyika, tutaanza kudai haki zetu na nyingine tutaanza kuzidai hapahapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba niishie hapo kwa kweli udini ukikua ni mbaya. Ni vyema tukaheshimiana tu kwamba tufanye mambo haya vizuri. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ileile ya 5 na kwa hali ya hoja yenyewe ilivyo, kwa heshima na taadhima, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aweze kuzungumza kwa niaba ya Serikali halafu tuweze kufanya maamuzi. Mheshimiwa Waziri Mkuu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa mujibu wa Katiba, nchi hii tumeweka misingi mizuri sana ya kuitambua Serikali kutokuwa na dini lakini mtu mmoja mmoja atakuwa na dini yake. Lakini kwa hili, nataka niseme tu kwamba hatuna sababu sana ya kuvutana sana juu ya jambo hili. Kwa mfumo ulivyo sasa, Serikali kupitia sheria zake, kwa makusudi imeweka utaratibu wa wazee hawa ambao tunawaita *assessors*. Utaona mara nyingi wamejikita kwenye maeneo ya kimila na maeneo yale yanayogusa imani ya dini ya Kiislam. Hili jambo ni la kihistoria na lina misingi yake. Hatuwezi leo kusema kwamba hawa wazee hawana nafasi katika kumsaidia Jaji ama Hakimu kufikia hukumu ambayo ni ya haki. Ndio maana utaratibu huu uliwekwa. Wale ambao tulipata nafasi ya kuwa kwenye nafasi za *State Attorney* (Mawakili wa Serikali), nimeuona utaratibu huu ukitumika na umekuwa na manufaa mazuri sana kwa sababu yako maeneo ambayo kwa misingi ya dini, kwa mfano ya Kiislam unapoanza kuzungumza mambo ya ndoa, unazungumza mirathi, wakfu, unazungumza nini, wako watu ambao wanaweza kuisaidia Mahakama vizuri zaidi katika kutenda haki, ndio maana mfumo ukaruhusu jambo hili liwepo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nataka niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge, mjadala unaweza ukawa mkubwa, mkaukuza, ukaonekana kama vile tumefika mahali sasa hii ajenda ni kubwa ya kutugawa, hapana, tusifike huko. Ama turudi kwenye utaratibu ulivyo sasa ambao unakubali jambo hili liwepo kumsaidia Jaji ama Hakimu na mara zote imekuwa ni kwamba wakishakuwa ni

wengi lazima Hakimu au Jaji akubaliane na ule uamuzi kwa sababu linagusa mila, linagusa desturi ambayo kwa misingi yetu hatuwezi kulikimbia kwa sababu sio eneo ambalo tumebobea kwa sababu (*it is not just law*), si suala la sheria tu, viko vitu vingine mle ndani ambavyo unahitaji zaidi mila zile na desturi zao zinasema nini. Kwa hiyo, ama tuchukue hoja ile ya *Comrade Kigwangalla* ambayo kwa kweli ana *modify* tu utaratibu wa sasa, lakini kimsingi ni uleule. Kama itaonekana kwa busara zako unaona lina ugumu basi bora Serikali turudi tukalitazame, tuje na pendekezo zuri zaidi lakini kwa maana ileile ambayo tutakuwa tumeiweka vizuri zaidi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wangu umekwisha, naomba Bunge lirejee ili tuongeze muda ili turudi tena kwenye Kamati tuweze kuhitimisha hoja hii. Kwa hiyo, Bunge linarejea ili tuweze kuongeza muda halafu tutaendelea.

(*Bunge lilitrudia*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, namwita sasa Waziri wa Nchi, aweze kutoa hoja katika misingi ifuatayo, kwa mujibu wa Kanuni zetu aturuhusu tuweze kuendelea na ajenda hii kwa kuongeza muda. Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 150 ya Kanuni za Bunge, naomba Kanuni ya 28(2) itenguliwe ili badala ya Bunge kumaliza kazi zake saa 7.00 mchana liendelee mpaka Muswada unaojadiliwa utakapomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa kwa mujibu wa Kanuni na imeungwa mkono, sasa nitakwenda kulihoji Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

(Hoja ya kutengua Kanuni ya kuahirisha Bunge saa 7.00 mchana na badala yake Bunge liendelee mpaka Muswada unaojadiliwa utakamalizika ilikubaliwa na Bunge)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria
Mbalimbali wa mwaka 2012 [The Written
Laws (Miscellaneous Amendments)
(No.3) Act, 2012]**

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo na naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutumia nafasi yake ya kiti ndani ya Bunge ili kutuwezesha kutupa mwelekeo wa kuhitimisha hoja hii. Sasa nitamwita mtoa hoja ili aseme maneno mafupi ili niweze kuwahoji.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa ajili hiyo, ninaomba kuondoa mabadiliko yaliyotegemewa kufanywa kwenye Ibara ya 7 cha sheria hiyo, kwa hiyo, kufuta Ibara ya 9 yote kama inavyoonekana kwenye jedwali, sio yote ile 7 lakini ile 10 nilikuwa nafikiri bado ibaki, 11, 12 na 13 pia ibaki, pamoja na (D), (E) na (F) mpaka (H) ambazo zinafanya marekebisho kwenye maeneo mengine. Kwa hiyo, mantiki ya haya ni kwamba ile Ibara ya 9 ya Muswada iondoke kama ilivyo, lakini zile sehemu za (C), Ibara ya 10 na kuendelea zibaki.

MWENYEKITI: Haya! Waheshimiwa Wabunge, mmepokea hayo baada ya kumsikiliza Waziri Mkuu na mtoa hoja, sasa kwa mujibu wa maelezo aliyoyatoa haya hapa anakwenda kufuta ile Ibara ya 9. Lakini katika sehemu hiyo, zile nyingine zinazobaki 10, 11 na 12 zinaendelea kubaki. Sasa nawahoji.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kitu kidogo. Wakati AG anawasilisha, aliwasilisha ile Ibara ya 9 peke yake, hii Ibara ya 10 hakuiwasilisha. Kwa hiyo, je, ataiwasilisha, inahusu lugha?

MWENYEKITI: Kwa sababu tunakwenda kifungu kwa kifungu Mheshimiwa Mnyika...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Tutakwenda?

MWENYEKITI: Tulikuwa tunajua hiyo Ibara ya 9 tu ndiyo ilioleta mjadala hapa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Haya!

MWENYEKITI: Kwa hiyo, sasa ndio tunakwenda kuifuta hiyo Ibara ya 9 kwa maelezo ya Mwanasheria, lakini pia kwa maelekezo tuliyoyapokea kutoka kwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge sasa nakwenda kuwahoji.

(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)

Ibara ya 10

MWENYEKITI: Ibara ya 10, ina marekebisho ya Mwanasheria Mkuu. Sasa tuanze na Mheshimiwa Mnyika, huna marekebisho ila una ushauri.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani tayari Mwanasheria amewasilisha, nitautoa ushauri baada ya Mwanasheria kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho yake.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ilivyo sasa ni kwamba lugha ya Mahakama ya Mwanzo ni Kiswahili lakini kwa kuwa tunawaingiza sasa Mahakimu ambao ni Hakimu Wakazi, tunapendekeza kuongeza pamoja na Kiingereza. Kwa hiyo, kama tulivyofanya kwenye *Schedule of Amendment* ni kwamba lugha iwe aidha Kiswahili au Kiswahili au Kiingereza.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kwa mara nyingine tena, sijaridhika na majibu ya AG kwamba tayari kuna watu wengi wenyewe kujua Kiingereza na kwa kuwa wakati tunajadili hapa Mkataba wa Sheria ya Afrika Mashariki tulionyesha wote kwa pamoja, pande zote dhamira ya kukipa kipaumbele Kiswahili katika Mahakama zetu kwenye ngazi mbalimbali, sasa ni ajabu kwenye Mahakama za Mwanzo ambazo zinawagusa wananchi wengi sana ikiwemo huko vijijini, Sheria ilisharuhusu kiwe Kiswahili, sasa tunataka kuweka chaguo ambalo kwa namna yoyote ile Hakimu atakapoamua kuchagua Kiingereza atamwathiri yule mwanachi wa kawaida ambaye hata haki ya kutetewa amenyimwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nashauri AG akubaliane na ushauri ambao umetolewa kwa nyakati mbalimbali, aiache Sheria kama ilivyokuwa, Mahakama za Mwanzo ziendeshwe kwa lugha ya Kiswahili. (*Makofi*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nimwombe kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali akubaliane kama tulivyoshauri tangu jana na kama Mheshimiwa Mnyika alivyomaliza kusema. Ni ukweli usiopingika, Watanzania wangapi ambao wanajua au wanaumilisi wa lugha hii ya Kiingereza? Ni wachache! Watanzania wengi wanajua lugha ya Kiswahili tena kuna wengine hata hiki Kiswahili tunachozungumza

huko, vijiji bado ni matatizo. Kwa hiyo, matumizi ya lugha ya Kiingereza kwamba Hakimu atakuwa anaamua kwamba atumie lugha ya Kiswahili au Kiingereza itatoa fursa ya kumnyima haki mwananchi huyu wa kawaida ambaye haielewi lugha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile wakati tunazungumzia kuridhia lile Azimio la Afrika Mashariki kama alivyosema, tumepata kushauri hapa ni vyema hata hizi Mahakama nyingine nazo tufikirie suala la matumizi ya Kiswahili katika Mahakama nyingine. Sioni tatizo kwamba hivi sasa pengine labda tuna uhaba wa istilahi maalum kwa ajili ya kutumia kwenye suala la kuandika hukumu na kufanya maamuzi mbalimbali. Hivi sasa Kiswahili kina misamiati ya kutosha; ni tofauti na miaka kumi, ishirini au thelathini iliyopita. Nimwombe Mwanasheria Mkuu, nikuombe uridhie utaratibu ubaki vilevile na twende hata kwenye Mahakama nyingine tutumie lugha ya Kiswahili, ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tujali muda.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nikiungana na Waheshimiwa Wabunge waliopita kuzungumza, kimsingi hivi karibuni nilifanya ziara katika maeneo ya magereza na kwa kweli kulikuwa na malalamiko makubwa sana kutoka kwa wafungwa wakilalamikia lugha ya Kiingereza na hususan walikuwa wakijaribu kuonyesha kwamba hata wanapotakiwa kukata rufaa sasa kwenye Mahakama za Wilaya na Mahakama za Juu, inabidi wakate rufaa hizo kwa Kiingereza na hivyo kulazimika kumtafuta mtu ambaye atamwandikia na pengine akaandika tofauti na alichokuwa anamaanisha. Sasa kwa mazingira hayo, kama mtoa hoja alivyozungumza kwamba kwenye Mahakama za Mwanzo hatulazimiki kupeleka hawa Mawakili kutokana na kurahisisha mazingira ya kuwafikia wadau wengi zaidi, basi ningeshauri lugha ya Kiswahili iendelee kutumika kama *compulsory language*, kama lugha stahiki katika Mahakama za Mwanzo lakini vilevile wafikirie kuileta Sheria ya kurekebisha lugha ya Kiswahili

kutumika katika Mahakama zinazofuata huko juu ili Watanzania wapate uhuru zaidi.

MWENYEKITI: Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Wabunge waliozungumzia jambo hili kwa hisia. Nakumbuka katika Bunge liliopita, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anahitimisha alisema maneno ambayo yapo katika kitabu cha msanii maarufu Shaban Robert kuhusiana na Lugha ya Kiswahili kwamba "*Titi la mama litamu hata kama ni la mbwa*" na mimi kwa kweli nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba tuendelee na Kiswahili. Kwa hiyo, kwa maneno hayo na ni vizuri kusema kwamba kinachosemwa hapa ni matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kuweka kumbukumbu za Mahakama lakini msemaji aliyejita Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, rekodi hizo ndizo pia zinatumika kuandaa rufaa. Kwa hiyo, nakubali kwamba tutumie Kiswahili kwenye Mahakama za Mwanzo na hivyo ninaomba kuondoa Ibara hiyo ya 10 katika Muswada wa Marekebisho. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ahsante. Kwa hiyo, unapoondoa ina maana Sheria inabaki ikisisitiza matumizi ya Kiswahili kwenye Mahakama zile za chini? Kwa sababu lazima tuelewane hapo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Ndiyo!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo baada ya hoja hizo kujengwa na Waheshimiwa Wabunge na Mwanasheria Mkuu kuona umuhimu wa suala hili na sisi wote kusikiliza kwa makini, sasa naomba kuwahoji.

*(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilifutwa na Kamati
ya Bunge Zima)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara Zilizotajwa Hapo Juu Zilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara Iliyotajwa Hapo Juu Ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara Zilizotajwa Hapo Juu Zilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hiyo tunafanya marekebisho makubwa kwenye kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:-

"For the purpose of preparation of a consolidated report referred to under subsection (1)- the Accounting Officers shall prepare an action plan of the intended remedial actions for submission to the Paymaster General."

Sasa baada ya hapo tunampa Paymaster General mamlaka ya ku-*consolidate*, kuziweka zile taarifa pamoja na kuzipeleka kwa Waziri na Waziri anatakiwa aziweke Mezani Bungeni kwenye (b)(i). Halafu ampe pia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali nakala ya taarifa za

majibu ya Maafisa Uhaisbu kuhusiana na ripoti hiyo. Kwa hiyo, ripoti hiyo ni kwamba kwenye (3) tunasema, *the report of the Minister*, ile taarifa ya Waziri ambayo tumeirejea hapo juu itawekwa Mezani Bungeni pamoja yaani *concurrently* na taarifa ile ya *Controller and Auditor General* ili kuwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge kuangalia majibu ya Maafisa Masuuli hawa kwenye taarifa zile za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ambazo zilikuwa ni hoja. Tunafikiria kwamba hiyo itakuwa ni nafasi nzuri ya kusikiliza pande zote kabla ya maamuzi hayajafanywa.

MWENYEKITI: Ahsante. Hayo ni marekebisho ya AG. Tunaanza na Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami pia nilileta marekebisho yangu katika hoja hiyohiyo na madadiliko yangu yalikuwa yanapendekeza mabadiliko haya yote yaliyoletwa yafutwe kwa sababu zifuatazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tukiangalia hii Sheria ya *Public Audit Act, 2008*, utakuta vipengele vyote ambavyo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu amevileta.

MWENYEKITI: Samahani kidogo Mheshimiwa Halima Mdee. Kwenye hii *amendment* yako niliyonayo hapa inasema *deleting the entire clause 19 as amended*, sasa Ibara ya 19 hatujafika bado.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni ya pili. Zipo mbili.

MWENYEKITI: Ibara ya 15 Tumeshaipita.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ibara ya 15 ilikuwa kwenye *main Act*, akaja akaleta madabiliko nadhani jana lakini *concept* ni hiyohiyo moja.

MWENYEKITI: Basi usi-concentrate na Ibara ya 15 kwa sababu nilishahoji. Nadhani u-concentrate na hii sasa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ibara ya 15 inazungumzia hoja hiihii, katika *original Act* ya *Miscellaneous Amendment* ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa Ibara ya 15, kwa sababu alileta mabadiliko mengine kwa hiyo namba zimesogea mbele lakini hoja ni hiihii moja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, ngoja tuelewe, naomba uketi. Sasa hivi *concentration* yetu iko *clause 18* ambayo mwanzo ilikuwa ni Ibara ya 15. Sasa wewe *amendment* niliyonayo hapa inakwenda kuzungumzia ku-delete *clause 19*. Hebu ngoja naona ziko mbili hapa. Kwa hiyo, unayo nyingine ambayo umei-submit ina *delete the entire clause 15 of the Act* ambayo ni Ibara ya 18 sasa hivi. Kwa hiyo, *you are right*, naomba uendelee.

Waheshimiwa Wabunge, samahani, kwa kweli haya mambo lazima kujiridhisha kwanza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimependekeza mapendekezo yafutwe kwa sababu, kwanza ukiangalia hii Sheria ya *Public Audit Act, 2008*, hizi hoja zote ambazo anazisema Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu zipo. Ukiangalia kipengele cha 38 kinatoa mamlaka kwa *Committee za Bunge* kujadili hoja ambayo imeletwa na Waziri mwenye dhamama kutokana na ile Ripoti ya CAG iliyokuwa *tabled*. Vilevile inatoa maelekezo kwa Kamati husika kuleta taarifa zake mbele ya Bunge kwa ajili ya kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kipengele cha 40 cha Sheria hii kimeenda mbele zaidi na kusema kwamba Afisa Masuuli anatakiwa aandae Mpango Mkakati na hatua ambazo atazichukua na kuzipeleka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusiana na hayo mapungufu ambayo yameonekana. Kingine kinasema kabisa kwamba huyu Mlipaji Mkuu (*Paymaster General*) baada ya kupata hizo *response* na *action plans*, ata-submit kwa Waziri ambaye

anatakiwa *a-lay before the National Assembly* lakini vilevile CAG atapewa nakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kipengele kinakwenda mbele zaidi kwa kusema kwamba CAG sasa kwa hizo taarifa ambazo atakuwa amezipata kutoka kwa Afisa Masuuli na kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, atazijumlisha katika taarifa yake nyingine ya mwaka unaofuata. Kwa hiyo, hapa hakuna kitu tofauti, kitu ambacho kinataka kuingizwa kiujanja ni kusema kwamba Bunge lisijadili Taarifa za Kamati za Bunge bila maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua michakato ya *auditing* ikoje? CAG anafanya kazi na Maafisa Masuuli kutaka kupata uthibitisho wa matumizi ya fedha ambazo tunawapatia. Baada ya hapo Kamati za Bunge ambazo zina mamlaka kikatiba na kikanuni zinawaita wahusika na kuwahoji CAG amesema hivi, mna mujibu gani? Sasa kama katika mazingira yote mawili...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Naomba dakika moja nimalizie ili nijengeta hoja yangu nieleweke.

MWENYEKITI: Kuna watu wataendelea ku-*support*.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama katika mazingira...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, naomba uketi. Unajua Waheshimiwa Wabunge, ninafahamu kabisa kama nitaachia kila mtu afanye anachotaka ndani ya Bunge, kwa mujibu wa Kanuni itakuwa si utaratibu, naomba uketi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja nimalizie.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima naomba uketi chini. Kanuni ikishanisimamisha Kiongozi Mezani, Mbunge yejote anayezungumza ni lazima aketi na watu wote wasikilize ninachokisema. Mheshimiwa Halima Mdee, Kanuni zetu ziko wazi.

Mheshimiwa Mdee, ninafahamu kwamba una hoja ambayo kweli ulitaka kuijenga. Niwaombe Wabunge wengine, kama una hoja, jitahidi kupanga maneno kwa muda tuliopewa Kikanuni lakini ukipanga maneno yanazidi muda halafu unamwambia Mwenyekiti nipe dakika moja na mwingine akisimama nisipompa dakika moja, hiki Kiti sasa kitakuwa hakiongozwi kwa utaratibu. Kwa hiyo, ninajua kwamba Mheshimiwa Halima umeweka hoja yako na *amendment* umeweka na wewe ndiyo mtoa hoja na utapata muda mwingine ili uizungumzie hoja hiyo.

Sasa nawaruhusu wale wengine ambao wanataka kusema maneno juu ya hoja yako na baadaye nitakupa nafasi wewe utazungumza tena lakini siwezi kuvunja Kanuni, niongeze muda tu kwa kila Mbunge hapa nitakuwa sitendei haki Kanuni wala uongozi wangu hapa kama Mwenyekiti. Naomba nimwite Mheshimiwa Mnyika halafu Mheshimiwa Cheyo na atafuatia Mheshimiwa Subira Mgali.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono mapendelekezo ya mabadiliko yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Halima Mdee ya kuondoa haya marekebisho yaliyopendelekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba jambo hili lilizuka wakati wa Mkutano wa Bunge mwaka jana 2012, Bunge lilipozungumza kwa ukali sana kuhusu Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutaka Mawaziri wajiu zuru na hatimaye yalifanyika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri. Sasa kwa sababu ya yaliyotokea wakati ule, kunataka kuletwe mapendelekezo ya marekebisho ya kuminya hali ile ya Bunge kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naunga mkono mapendekezo haya yaondolewe, Serikali ikajipange upya, kwa sababu tukija kwenye Katiba ya nchi, Ibara ya 143(4) inasema, Mdhibiti wa Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa kwa Rais na Rais anatakiwa kwa mujibu wa Katiba, ndani ya siku saba toka kuanza kwa Mkutano wa Bunge toka alipopokea ile taarifa; taarifa ile iingie ndani ya Bunge na Rais asipoleta, Katiba inasema Spika au Naibu Spika kama Spika hayupo anaileta Bungeni moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja inayoletwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali hapa kwenye mapendekezo yake, hiki kipengele cha (3) cha mapendekezo yake kinasema:-

"The report of the Minister under subsection (2)...shall be laid before the National Assembly concurrently with the report of the Controller and Auditor-General".

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa *laid* vipi *concurrently* kama Rais akishaipokea tu hiyo ripoti ndani ya siku saba inatakiwa iingie Bungeni, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba ripoti ile itakuwa inapelekwa kabla na mambo yatakuwa yanakwenda kufanyika kabla wakati ambapo ripoti ikija hapa Bungeni moja kwa moja Wabunge tuna haki ya kupewa nakala na tuna haki ya kuijadili na kuishughulikia kabla hata ya kushughulikiwa na Kamati za Bunge!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nasisitiza na namuunga Mkono Mheshimiwa Halima Mdee kwamba utaratibu uliokuwepo mwanzoni ubaki uleule kwa sababu tukiubadilisha, tutalinda uzembe wa Maafisa Masuuli, wanapewa nafasi ya kutoa *management responses* wakati *CAG anapo-audit*, wanafanya uzembe au wanakuwa hawana majibu. Mambo yakiibuka Bungeni, kukiwa na zogo kubwa ama wanakwenda kuchakachukua *responses* wakati walikuwa wana nafasi ya kuyafanya hayo na hawakuyafanya. Kwa hiyo, mimi nadhani hapa mapendekezo yangeondolewa.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono pendekezo la Mheshimiwa Mdee kwa sababu Sheria kwa sasa hivi, ndiyo haya mambo nilizungumzia na pia ukiunganisha na ile ripoti pamoja na *response* ya *Paymaster General*, yule *CAG* hana *control* ya *Paymaster General* kwamba lini ripoti itakuwa tayari au vipi. Mpaka hivi sasa nazungumza kwa uzoefu, kuna ripoti nyingi ambazo bado tunawadai hawajaweza kuleta. Kwa hiyo, sisi twende na utaratibu ambao uko ndani ya Katiba, tarehe fulani na sisi tunaweza tukajisifu dunia nzima, *our CAG is on time, every year* analeta ripoti yake hapa. Kwa hiyo, naona tusiambatanishe na jambo lingine lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka tu kushauri kwa Mwanasheria Mkuu, kama anafikiri kwamba kufanya hivi eti kutakuwa na majibu, hakuna majibu kwa sababu ripoti inayowekwa pale ni ya mwaka mpya, ndiyo unaokaguliwa, ripoti ya *Paymaster General*, ni ya mwaka uliopita. Kwa hiyo, hutakuwa na majibu ya ripoti iliyoko mbele ya *National Assembly* kwa wakati huo. Kwa hiyo, mimi naona ni afadhali tuache kama ilivyo sasa.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa na mimi nichangie hoja hii. Ninaomba nichangie kwa kuzingatia uzoefu wangu mdogo. Jambo hili linalopendekezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, siyo jipya, kwa sababu kwenye zile *individual reports* zinazokwenda Wizarani na kwenye Halmashauri zetu, kunakuwepo na majibu, kunakuwepo na *comments* za *Auditors* na majibu ya *management* na baadaye *Auditor* ana-verify anasema nini. Kinachowasilishwa Bungeni, ni ile *general report*, inakuwa inakosa majibu kwa kuwa inakuwa ni *summary* ya *findings*. Kwa hiyo, kuipa fursa Serikali kuwasilisha majibu na kwa sababu ripoti inayowasilishwa inakuwa ni ya *public*, ni vema Serikali pia ikapata fursa ikawasilisha majibu kwamba *public* inapojadili, inajadili na majibu ya Serikali. Kwa kuwa Bunge limepewa mamlaka ya kuishauri na kuisimamia Serikali, sioni sababu kwa nini tunahofia fursa ambayo inapata Serikali ya kuwasilisha majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi, kwa sababu nimefanya kazi kwenye ofisi ya CAG ndani ya miaka 10 na ndiyo utaratibu tunaoufanya kwenye *exit conference*. Wanajibu na kama jibu hulikubali, CAG anaandika kuwa jibu siyo sawasawa na ndiyo ilikuwa inawasilishwa ndani ya Bunge, tunapata nafasi ya kujadili. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa AG kabla ya Mheshimiwa Halima halafu ndio Mheshimiwa Halima atahitimisha hoja yake.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda sitatoa elimu kwa suala hili hapa, tunachozungumza ni kwamba, unapoamua kitu mbele ya mtu mwingine, kwa sababu Sheria ilivyo kama alivyosema Mheshimiwa Mnyika, mamlaka ya kuwasilisha Hesabu za Serikali yanatokana na Katiba na amesema vizuri lakini sasa nisichofahamu ni kwamba CAG akiwasilisha hapa ripoti yake, yale "madongo yake" hayana majibu. Kwa sababu kama ametupa nafasi ya kusema, wewe unaona taabu gani kumwajibisha Waziri wa Fedha kuleta hizo *comments* Bungeni!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatusemi kuwa ripoti ya CAG haiwezi kujadiliwa bila ripoti ya Serikali, hatusemi, kwa sababu utaratibu niliosema huko ni kwamba Ibara ile ya 143, iliyosemwa na ninajua kichwani, Ibara ndogo ya pili (2), inasema kuwa siku saba Rais atawasilisha kwa Spika. Akishawasilisha hapa, hiyo haibanwi na mambo ya ku-*discuss* ripoti ya Serikali, ni kwamba utakapokuwa una-*discuss*, unapokuwa unaenda Ubungo unasema fedha ya Serikali imeliwa na mafisadi, majibu yapo kuwa kumbe haikuliwa!

MBUNGE FULANI: Yes!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Hiyo ndiyo maana yake. Kwa hiyo, kwa kweli ni upotoshaji na ninasikitika ni upotoshaji mkubwa na siyo vyema kwamba sasa unaona utakosa kitu cha kwenda kuwaambia watu, cha uwongo... (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninafikiri kuwa utaratibu huu ni utaratibu mzuri kabisa, unaleta haki kwa Serikali pia. (*Makofii*)

TAARIFA

WABUNGE FULANI: Taarifa!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, katika kipindi hiki sitaruhusu taarifa, ninaomba nimrudishie mtoa hoja, ninaomba Mheshimiwa Cheyo na Mheshimiwa Machali mtulie katika viti vyenu nimrudishie mtoa hoja ili tuweze kufanya maamuzi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona Mwanasheria Mkuu wa Serikali anataka ku-*dilly-dally* ili kuepuka hoja. Hoja hapa iko kwenye iliyokuwa Ibara ya zamani ya 15 ambayo na yeze pia ameiletea mabadiliko. Ibara ya 15 kama nilivyosema iko kwenye Sheria ya *Audit* ya mwaka 2008, lakini walichoongeza ni kuwa taarifa za Kamati wanazozileta Bungeni haziwezi kujadiliwa mpaka kuwe na taarifa nyingine ya Serikali. Hiyo imeelezwa kwenye mabadiliko yake lakini vilevile haiwezi kujadiliwa, lazima zijdiliwe pamoja, iko kwenye Ibara ya 15 ya zamani na iko kwenye Ibara ya 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunachokisema ni kwamba *Auditor* anafanya kazi mwaka mmoja na Maafisa Masuuli kuchunguza uhalifu, taarifa inaenda kwenye Kamati za Bunge, Kamati za Bunge zinawaita Maafisa Masuuli kutoa maelezo yao kwenye Kamati za Fedha na zingine. Baada ya hapo, Kamati za Bunge zinakuja na taarifa yake ya mwaka. Katika taarifa hiyo inatoa taarifa *recently* baada ya kuwahoji na baada ya maelezo ya CAG katika ripoti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu viwili, kuna ripoti za Kamati na kuna ripoti ya baadaye ya CAG. Sasa mabadiliko yangu mengine yanahusu ripoti ya baadaye ya CAG kunyimwa kujadiliwa, sasa hiyo hatujafika huko. Hoja yangu hapa ni kwamba Sheria ilivyo sasa haina tatizo, hakuna haja ya Wabunge kuambiwa hizi taarifa za Kamati

mkijadili lazima mjadili hii, wakati Sheria ya zamani iko wazi kwamba Waziri anatakiwa a- *lay before the National Assembly*, yale masuala ambayo Maafisa Masuuli na walipaji ama Mlipaji Mkuu wa Serikali ametoa *observation* zake na mipango mikakati yake kutokana na ubadhilifu uliofanyika.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa ninakwenda kuwahoji kuhusiana na hoja hii ilivoletwa na Mheshimiwa Halima Mdee inayokwenda kufanya mabadiliko haya na kuondoa kifungu hicho chote. Walioafiki wameshinda, walioafiki hoja hiyo isibadilishwe kwa mujibu wa Halima Mdee wameshinda, ndiyo maana yangu Waheshimiwa Wabunge. Tunapokuwa na utata katika maamuzi lazima nisimame ili niwaeleze vizuri, eeh! Ninaomba nirudie kusema hivi, kwa lugha nyepesi sasa ya Kibunge, waliokataa hoja ya mabadiliko ya Mheshimiwa Halima Mdee wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitakwenda kuwahoji kwenye hoja ya mabadiliko ilivoletwa na Mwanasheria Mkuu ikiwa na zingatio la Ibara ya 15, sasa ni Ibara ya 18.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko ya Serikali bila mabadiliko ya Mheshimiwa Halima J. Mdee)

MWENYEKITI: Katibu, tunaendelea.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Ibara hiyo ya 19, ina marekebisheso ya Mheshimiwa Mdee na marekebisheso ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Mwanasheria Mkoo wa Serikali halafu Mheshimiwa Mdee.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 39, inafanya mabadiliko kwanza kwenye *Schedule of Amendment*, ukurasa wa tatu, pale tunakifanyia mabadiliko kwa kuandika 39(1), baada ya hapo, tunaongeza Kifungu kipya ambacho kinasema kuwa, zile taarifa ambazo ni *public document* zitajadiliwa na Bunge baada ya kuwa zimejadiliwa na *Parliamentary Oversight Committees*, kama tulivyoonyesha kwenye Ibara ya 38(5) iliyopitishwa sasa na kufuata masharti ambayo yametolewa na Kanuni za Bunge.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamesimama kuomba nafasi ya kuchangia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa mnakwenda kuchangia hoja ya Mwanasheria Mkoo, eeh! Mheshimiwa Cheyo na Mheshimiwa Mnyika mnataka kuchangia hoja ya Mwanasheria Mkoo?

WABUNGE FULANI: Ndiyo!

MWENYEKITI: Haya na Mheshimiwa Mdee nitakuita, wewe una hoja ya mabadiliko, hawa wanachangia kwanza hoja ya Mheshimiwa AG.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii ukiisoma vizuri, unaona wazi kabisa Bunge linajitungia Sheria kupunguza madaraka yake, yaani ni kama mtu unachukua mkuki unajichoma wewe mwenyewe. Ibara ya 64 ya Katiba inasema kuwa kazi ya Bunge ni *oversighting*, kuisimamia Serikali. Jambo limefika hapa, ripoti mpya imekuja na inasema kuwa DC wa Muheza ameiba shilingi milioni 100, ripoti iko hapa, Sheria hii inasema kuwa Bunge halitajadili yaani tumwache huyu mwizi aendelee kwa mwaka

mmoja mpaka *PAC* ilete ripoti ndiyo tujadili! Mheshimiwa, *what are we doing for ourselves?* Yaani tuache ubadhifuru uendelee halafu ndiyo tujadili na hili *document* linaloletwa hapa na Mheshimiwa CAG ni *public document* wale kule watakuwa wanapiga kelele *DC* wa Muheza ameiba shilingi milioni 100 na Bunge limefungwa mdomo, limejifunga lenyewe mdomo lisizungumze.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda
wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cheyo muda.

MHE. JOHN M. CHEYO: Kwa hiyo, mimi ninasema kusema kweli hili...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cheyo, muda umepita, ninamwita Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN M. CHEYO: Haya!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya yaliyoletwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanapaswa kuondolewa kwa sababu ni kurudisha nyuma na kupunguza ukuu wa Bunge kwa Ibara ya 63, wa kuishauri na kuisimamia Serikali. Kuna tofauti kati ya Bunge na Kamati ya Bunge, kitendo cha kutunga Sheria ya kulifunga mikono Bunge mpaka kwanza Kamati za Bunge zifanye kazi, mimi nilisema mwanzoni kuwa masuala haya yaliibuka mwaka jana wakati ripoti za CAG ilipoianika Serikali hadharani kuititia Bunge hili, sasa inatafutwa namna ya kupunguza haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Ibara ikipitishwa ni Ibara inayochelewesha kuchukua hatua dhidi ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Maeleo yanayotolewa na Serikali unaweza kudhani kuwa ni matamu sana kwamba ku-buy time Kamati zipitie, Maafisa Masuuli waleti maeleo yao kwa mujibu wa Sheria tuliyonayo hivi sasa ya Ukaguzi, hawa Maafisa Masuuli wanapewa

hiyo nafasi kwenye Ukaguzi mpaka CAG aandike *audit query* maana yake ni kuwa njia za kawaida katika hatua zingine zimeshindikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ajabu sana kama Rais amepewa ripoti na Rais ameikabidhi kwa Spika, Katiba ya nchi inasema, siku saba toka kuanza kwa Kikao, toka Rais akabidhiwe ripoti, ikiwekwa Mezani inakuwa ni ripoti ya umma, halafu tunatunga Sheria kuwa Wabunge hatuwezi kujadili mpaka kui-refer kwanza iende kwenye Kamati za Bunge ishughulikiwe ndiyo tuletewe ripoti. Hii Ibara haiwezi kukubalika kwa namna yoyote ile. Kwa hiyo, kama mtatumia wingi tena katika kupiga kura kukubali, mkubali lakini siyo sahihi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa AG, halafu nitakuita Mheshimiwa Halima uje na hoja yako hapa, nitakuita, anamalizia kabla sijahoji nitakuita kwa sababu wote mko kwenye kifungu hichohicho.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja inayojengwa hapa mimi ninaishangaa kwa sababu Ibara inasema kwamba *documents* zinazowekwa Mezani ni *public document*, kwa hiyo, *document* ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inakuwa ni *public document* na ile ambayo inawasilishwa ile tulioikubali ni *public document*. Mabadiliko hayo ni kwamba katika utaratibu wa kufanya kazi, Wabunge tunafanya kazi kwa mujibu wa Kanuni, kwamba ziko *Oversight Committees*, ziko tatu kwa sasa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa AG, ninadhani kwa faida ya Watanzania maana ya *Oversight Committees* ni nini?

TAARIFA

WABUNGE FULANI: Taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge anayetumia *mike* kwa kuvunja Kanuni ya 60, ninaomba awe mtulivu, Mheshimiwa AG endelea.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni, Kamati ni za kisera zile, eeh? Kuna Kamati kwa ajili ya kusimamia Fedha za Serikali, tunaziita *POAC* au *PAC*, zile ndiyo *Oversight Committees* za Bunge na zile zinafanya kazi kwa niaba ya Bunge. Ndiyo utaratibu wa Kanuni. Sasa tunachosema hapa ni hivi, ripoti zile ambazo zitajadiliwa na *Oversight Committees* za Bunge, sasa unasema Bunge linajadilije taarifa hizi lazima kuna Kanuni na hapa sisi hatujavunja Kanuni yoyote na kusema kwamba hii ni njia ya kujihami ya Serikali, ninafikiri ni kupiga ngumi chini ya kitovu, ninaomba marekebisho hayo yakubalike.

TAARIFA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, taarifa jamani kipindi cha Kamati, Eeh haya! Taarifa unampa AG!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge ziliyyo hivi sasa, Kanuni ya 37(4) inasema kwamba Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja wakati wowote hati yoyote ikiwekwa Mezani kwamba hati hiyo ijadiliwe. Sasa kama tunatunga Sheria inayosema kuwa hati hata kama ikiwekwa Mezani haiwezi kujadiliwa mpaka kwanza iende kwenye Kamati, tunatunga Kanuni ambayo inakwenda kukiuka Kanuni za Bunge. Sasa kwa nini tufanye yote hayo? Kuna nini ambacho kiko nyuma ya pazia kinachosukuma yote haya?

MWENYEKITI: AG, taarifa hiyo unaipokea?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mantiki na mawanda, kuamka tu na kusema ili upate nafasi ya kupiga madongo, hiyo ni lazima tuiangalie kuwa...

WABUNGE FULANI: Aaah!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, *order, order*, tuwe na uvumilivu ndani ya Bunge.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado ninasema Ibara hiyo ni nzuri na ibaki kwenye Sheria yetu, ninaomba Bunge likipitishe.

TAARIFA

WABUNGE FULANI: Taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee, ninaomba nifunge taarifa tuendelee na mjadala kwa sababu kuna watu wenye hoja za mabadiliko. Tukianza kusikiliza hizi taarifa, tunaondoka kabisa kwenye hoja. Mheshimiwa Halima Mdee, una hoja yako ya mabadiliko.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nisikitike kuwa Bunge letu linatunga Sheria ya kujivua au kuji-*limit* madaraka yake. Ninasema hivi kwa sababu ukiangalia hii Sheria ilivyo toka mwanzo, Ibara ya 39 ilisema kwamba taarifa ya CAG ni *public document*. Mabadiliko ya Serikali yanasema taarifa ya CAG haiwezi kujadiliwa mpaka pale itakapopita kwenye Kamati za Bunge na hiyo imetokana na ukweli kwamba Wabunge wakati tukijadili taarifa za *Oversight Committees* na kwa kuwa kipindi hicho CAG ana-*lay* ripoti mpya, tumekuwa tukifanya *reference* ya madudu yanayojirudiarudia, ambayo CAG analalamika katika taarifa yake mpya, ni makosa kwa Wabunge kujiveka uwigo wa kujadili masuala yake, nitatoa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia taarifa ya CAG hii iliyopita mfano anasema Ofisi za Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zimekuwa na maendeleo mazuri katika utekelezaji wa masuala ya kaguzi za nyuma. Hata hivyo, katika mwaka huo wa ukaguzi, Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa 58 zilikuwa hazijashughulikia masuala

ya miaka ya nyuma yenyeye jumla ya thamani ya shilingi billioni 543. Tukipitisha hii Ibara kama ilivyo, CAG aki-lay ripoti yake hapo, sisi tunafungwa mdomo mwaka mzima wakati watu hawajatekeleza majukumu yao miaka yote iliyopita kusubiri taarifa za Kamati za Fedha zije ndiyo tuanze kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, mwisho wa siku nyie mko wengi, mnaweza kuamua kuzika nguvu ya Bunge lakini mimi niwahakikishie, mtahukumiwa kwa hiki mnachokifanya, hamsaidii Taifa ila lengo ni kuilinda Serikali kwa sababu itakuwa inaonekana zembe kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni yangu na ninaungana sana na mapendekezo ya Mnyika na maoni ya Mheshimiwa Cheyo, lengo ni jema kuokoa nchi yetu.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Shekifu, Mheshimiwa Makamba na Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi ningependa ku-declare kwamba nimekuwepo Bungeni hapa kuanzia mwaka 1995, ninavyoolewa utaratibu wa kujadili mahesabu au kujadili jambo lolote katika Bunge unaletwa na Kamati za Bunge, ni vibaya au ni kukiuka Kanuni kwa jambo lolote likajadiliwa ambalo halikupita kwenye Kamati, kinachotakiwa hapa kwa Serikali ambacho tunakiomba siyo kupunguza nguvu lakini ni kukiri na kukubali kuwa itawajibika kwa kuhakikisha kuwa ukaguzi unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa hapa kwa Serikali ambacho tunakiomba siyo kupunguza nguvu lakini sasa ni kukiri na kukubali kwamba itawajibika kuhakikisha kwamba ukaguzi unafanyika kwa wakati, taarifa zinapelekwa kwenye Kamati kwa wakati na zinajadiliwa na Kamati kwa uhuru baada ya kupata maeleo ya kutosha. Kilichokuwa kinafanyika huko nyuma, ikishawekwa ripoti, mtu ye yeyote anaijadili, kumbe Kamati hazijajadili na kupata ukweli wa ndani. Maana kwenye Bunge tunapewa dakika mbili, tatu lakini kwenye Kamati tunahoji kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafkiri tukubaliane na mawazo ya Serikali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Peter Serukamba na Msemaji wa mwisho atakuwa Mheshimiwa January Makamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtu ambaye anajua *auditing*, ukishafanya *auditing*, ukatoa ripoti yako, ukafanya *audit conference*, kinachotakiwa unaweza ukasema hii ni *query* lakini baada ya muda inawezekana ikawa kuna *document* haionekani, mtu anakuja anaileta inakuwa hakuna *query*, lakini *by the time* anaileta ninyi mmeshajadili, mmeshamuua mtu, huku kesho siyo kweli, *what is this?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maana ya kuanzisha Kamati hizi ni hizi Kamati zifanye kazi vizuri. Ningombwa kwa kweli Bunge tuhakikishe Kamati zetu zinafanya kazi vizuri na zinaleta Bungeni kama kuna suala la ubadhirifu Kamati itasema na Bunge litachukua hatua yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na mawazo yaliyoletwa na Serikali kwamba ripoti *thoroughly* ziende kwenye Kamati, zijadiliwe vizuri na Kamati zilete mapendekezo hapa Bungeni, Bunge litafanya kazi yake kulingana na Katiba na Kanuni ambayo tumepewa na Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna anayeondoa nguvu za Bunge hapa, bado Kamati ni sehemu ya Bunge letu. (*Makofi*)

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba iwe kwenye rekodi kwamba uhuru huu ambao Bunge sasa linao na mamlaka makubwa ambayo linayo yametokana na utashi wa Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Wenyeviti wa hizi Kamati za *Oversight*, ni Wabunge wa Vyama vya Upinzani na wao sheria hii sasa inawapa mamlaka wakiwa kwenye viti kuhakikisha kwamba ripoti hizo zinajadiliwa kwa mapana na kwa kina na kuwasilishwa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoona hapa, kungekuwa kwenye Kamati kule kuna kamera za *TV*, tusingekuwa na mjadala tulionao hii leo.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Kama mtu unafanya jambo *with good faith*, huu mjadala tusingekuwa nao leo. Sielewi hata chembe, mtu anaogopa nini kujadili *document* ambayo ina pande zote za *story*? Unaogopa nini kujadili *document* ambayo ina maelezo ya upande mmoja na ina majibu ya upande wa pili? Sielewi leo kabisa, kwamba Mbunge anadiriki kusema kwamba Kamati ya Bunge si Bunge yaani anaona shida kutoa heshima kwa Kamati ya Bunge ambayo inatokana na Wabunge kwa ajili tu haipo kwenye televisheni. (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Aaah!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makamba, muda umekwisha.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda mapendekezo ya Serikali yapite.

MWENYEKITI: Sasa nitawahoji kuhusiana na mabadiliko ya Mheshimiwa Halima Mdee, muda umekwisha.

(*Hoja itolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kukataliwa*)

MWENYEKITI: Sasa nitawahoji mabadiliko yaliyofanywa na Serikali.

*(Hoja itolewa iamuliwe)
(Hoja illamuliwa na Kuafikiwa)*

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko ya Serikali)

Ibara ya 20

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 21

Ibara ya 22

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 26

Ibara ya 27

Ibara ya 28

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, taarifa!

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria
Mbalimbali Na.3 wa mwaka 2012 (*The Written
Laws (Miscellaneous Amendments)*
(No.3) Act, 2012)**

(Kusomwa Mara ya Tatu)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kwa heshima na taadhima kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya mwaka 2012 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Act, 2012*), kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya marekebisho ya Sheria mbalimbali, Na. 3 ya mwaka 2012, (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Act, 2012*) kama ulivyorekebishwa sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA
UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nitakwenda kulihoji Bunge na kabla ya kulihoji Bunge nitamwita Katibu ili aweze kusoma Muswada huu sasa kwa mara ya mwisho.

*(Hoja itolewa iamuliwe)
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulsomwa Mara ya Tatu
na Kupitishwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kuwapongeza wote, Wajumbe wa Kamati lakini Wabunge, kwa mijadala yenu na kwa kweli niwapongeze sana kwa jinsi tulivyo tumia Bunge letu leo kupingana kwa hoja tena kwa utulivu mkubwa. Hii inapendeza sana na inatusaidia kuwapa Watanzania nafasi ya kila mtu kusikiliza, aliyekuwa anapinga anasema nini na aliyekuwa ana-*support* anasema nini. Utaratibu huu ni mzuri sana, Watanzania wanatusikia kwa utulivu wote na wana uwezo wa kufanya maamuzi baada ya kutusikia tukipingana kwa hoja na siyo kwa vurugu, kwa kweli nawapongeza sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitaomba nimwite Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ili aweze kutoa hoja kwa kuwa Bunge letu leo litarejea katika muda ambao siyo muda rasmi wa shughuli za Bunge, Waziri wa Nchi!

KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 150 ya Kanuni za Bunge, kutengua Kanuni ya 28(2) ambayo inataka Bunge kuahirishwa mpaka saa 11 jioni na badala yake liahirishwe mpaka saa 10 kwa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA, Mkutano wa Kumi wa Bunge unaoendelea umepangwa kumalizika leo tarehe 8 Februari, 2013;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kanuni ya 28 fasili ya (2), Bunge linakutana hadi saa saba mchana na kuahirishwa mpaka saa kumi na moja jioni ili kumwezesha Waziri Mkuu kupata muda wa kutosha wa kutoa hoja ya kuahirisha Bunge, inabidi Bunge litengue Kanuni ya 28(2).

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kumi, Kanuni ya 28(2) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(2) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Bunge litakutana hadi saa saba mchana ambapo Spika ataahirisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa kumi na moja jioni itenguliwe na badala yake Bunge likutane hadi saa saba mchana ambapo Spika ataahirisha shughuli hadi saa kumi jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, lakini kabla sijawahoji nitakwenda kubadilisha maneno kidogo katika hoja ya Waziri. Katika kila eneo lilitamkwa ataahirisha, ninabadilisha na kuweka atasitisha. Kwa sababu shughuli za mchana zinaposimama tunasitisha shughuli za Bunge na tunapomaliza kabisa jioni tunazahirisha. Kwa hiyo, ninaomba kufanya mabadiliko katika maeneo yote yaliyokuwa yanasmeka ataahirisha na kuweka neno atasitisha ili niweze kusitisha shughuli za Bunge hili na tuweze kukutana tena saa kumi jioni kwa mujibu wa hoja ya Waziri ili tuweze kwenda kwenye hoja ya kuahirisha Bunge.

Baada ya kutoa marekebisho hayo kwa mujibu wa Kanuni ya 5 ya mamlaka yangu, sasa nitalihoji Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, anapenda kuonana na Wabunge wote wa Zanzibar wa Majimbo leo jioni mara tu baada ya kuahirishwa Bunge katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya shughuli hizo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi leo jioni.

(Saa 7.55 Bunge lilitishwa mpaka saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia)

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka niliyopewa na Kanuni ya 152(3), nimezifanyia marekebisho Kamati zote kwa kuziongezea majukumu, kuzipunguzia majukumu, kuzifuta baadhi ya Kamati, halikadhalika kuunda Kamati mpya tatu. Yafuatayo ni maboresho yanayohusu muundo na majukumu ya baadhi ya Kamati za Bunge. Hivyo basi, dondo za mabadiliko haya ni kama ifuatavyo:-

Kamati zifuatazo zimefanyiwa mabadiliko katika muundo na majukumu yake; Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Viwanda na Biashara, Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Kamati ya Sheria Ndogo na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Kamati tatu zimeundwa; Kamati ya Bajeti, Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Tathmini ya Mfumo wa Kamati uliopo; lengo la kuwepo Kamati za Kudumu za Bunge, ni kurahisisha utekelezaji wa Madaraka ya Bunge, kama yalivyoainishwa na Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kuhusu kusimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake kwa niaba ya wananchi. Aidha, Ibara ya 96(1) ya Katiba, inalipa mamlaka Bunge, kuunda Kamati zake kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka ya Bunge.

Kwa sasa kuna baadhi ya Kamati zinazosimamia Wizara moja moja ambazo shughuli zake si nyingi ikilinganishwa na Kamati nyingine ambazo zinasimamia Wizara zaidi ya moja, zikiwa na shughuli nyingi. Vivyo hivyo, kuna Wizara zinazohusika na kutunga Sera, lakini kwa kiasi kikubwa Sera hizo zinatekelezwa na Wizara nyingine hadi ngazi za chini.

Mfumo huu husababisha baadhi ya Kamati za Bunge, kutoweza kufuatilia vizuri utekelezaji wa shughuli za Serikali, kinyume na matakwa ya Ibara ya 63(3) ya Katiba na majukumu ya Kamati, yalivyoainishwa na Kanuni za Bunge. Kwa mfano, Kamati ya Huduma za Jamii, imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera na shughuli zote za Wizara ya Afya, hususan huduma za Afya, kuanzia ngazi ya Zahanati hadi ngazi ya Hospitali ya Rufaa. Lakini baadhi ya shughuli za afya, zinatekelezwa chini ya usimamizi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuanzia Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya na Hospitali za Mikoa.

Aidha, kwa upande wa huduma za elimu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, chini ya usimamizi wa Kamati ya Huduma za Jamii, inahusika na Sera ya Elimu kuanzia ngazi ya Elimu ya Msingi hadi Vyuo vya Elimu ya Juu. Lakini utekelezaji wa Sera uko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, kwa upande wa Elimu ya Juu, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Ufundı – VETA.

Aidha, TAMISEMI inahusika katika kusimamia utoaji wa Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari. Kwa hiyo, TAMISEMI iliyopewa jukumu la kutekeleza Sera ya Elimu ngazi ya Awali, Msingi na Sekondari, inasimamiwa na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa ujumla TAMISEMI kwa mfumo wa sasa wa Serikali, imepewa madaraka ya kutekeleza majukumu ya sekta mbalimbali za umma kuanzia ngazi ya Vijiji na Mitaa.

Usimamizi wa Wizara nyingi au moja kwa mfumo wa sasa wa Kamati za Bunge, umeleta changamoto zifuatazo:-

Baadhi ya shughuli za Serikali, kutofuatiliwa ipasavyo na Kamati za Bunge. Kwa mfano, Kamati ya Huduma za Jamii, inaishia kwenye kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara zilizo chini yake na kushindwa kupata utaratibu wa kufuatilia utekelezaji unaofanyika chini ya mamlaka ya TAMISEMI inayosimamiwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Kamati ya Miundombinu; inapofuatilia utekelezaji wa Serikali katika ujenzi wa miundombinu ambao, huishia katika ufuatiliaji wa miundombinu iliyoko chini ya Wizara ya Ujenzi tu kwa kukosa nguvu za Kikanuni za kufuatilia utekelezaji wa miradi ya barabara ambayo ipo chini ya usimamizi wa TAMISEMI. Wakati wa bajeti, baadhi ya Kamati za Bunge, za sekta, huwa na Mafungu mengi ya kuchambua ikilinganishwa na muda uliotengwa kwa ajili hiyo. Mfano ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ambayo huwajibika kuchambua Mafungu 50. Maana ni Mafungu yote ya Mikoa, Mafungu ya zile Wizara kubwa, basi yanakuwa ni zaidi ya 50 na hiyo inafanyika ndani ya majuma mawili, wakati kuna Kamati zinazosimamia Fungu moja tu. Mfano wa Kamati iliyokuwa inasimamia Fungu moja ni Kamati ya Viwanda na Biashara, imekuwa ikisimamia Fungu Moja tu.

Hali hii imesababisha baadhi ya Kamati, kutokuwa na kazi za kutosha na hivyo kulazimika kurudiarudia kukutana na Asasi na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara yao. Aidha, kwa upande wa Serikali, Watendaji wa Wizara hizo wamekuwa wakitumia muda mwingi kujishughulisha na masuala ya Kamati za Bunge na hivyo kupunguza muda wa kushughulikia kazi za Wizara.

Majukumu ya Kamati zilizofanyiwa marekebisho na zilizoundwa; Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inaainisha Kamati 18 za Kudumu za Bunge na kueleza kuhusu muundo wa majukumu ya Kamati hizo. Mabadiliko yanahusu Muundo na Majukumu ya Kamati, kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge, kama ifuatavyo:-

Tuna Kamati mpya ya Bajeti; Kamati hii inaundwa ili kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya Serikali (*Micro Budget*) na Sera za Fedha. Kuainisha na kupendekeza vyanzo vyta mapato ya Serikali na kufuatilia mwenendo wa uchumi. Aidha, Kamati itakuwa na jukumu la kushauri Kamati zingine zote kuhusu bajeti kwa sababu, itakuwa na Wataalam wengi zaidi.

Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara; kutokana na kuundwa kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti, ambayo itakuwa na jukumu la kufuatilia masuala ya bajeti na fedha, hivyo basi, Kamati ya Fedha na Uchumi, inabadilishiwa majukumu na hivyo, sasa itasimamia masuala ya uchumi, mitaji, uwekezaji, maendeleo ya viwanda na shughuli za biashara.

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala; kutokana na Kamati hii kukabiliwa na jukumu la kusimamia Wizara zenye Idara na Asasi nyingi za Serikali, ili kuleta ufanisi majukumu ya Kamati hii yamegawanywa katika Kamati mbili kama ifuatavyo:-

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala; Kamati hii itakuwa na jukumu la kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake na Wizara ya Katiba na Sheria.

Kamati nyingine ni Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Kamati hii itasimamia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mikoa na Halmashauri zote nchini pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri. Kwa maana hiyo, Kamati ya Sheria Ndogo, imevunjwa, shughuli zake zitafanywa na Kamati hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Kamati ya Huduma za Jamii; Kamati hii itakuwa na jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis kwa ngazi ya Elimu ya Juu, Vyuo vya Ualimu na Elimu ya Ufundis – VETA na Taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, vikiwemo Vyuo vya

Elimu ya Juu ya Umma, Baraza la Mitihani, Taasisi ya Kukuza Mitaala na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Kamati itaendelea na jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Wizara hii, hususan huduma za afya kwa ngazi za Hospitali za Rufaa, Kanda na Hospitali ya Rufaa ya Taifa – Muhimbili, Bohari Kuu ya Madawa, Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii, Vyuo vya Ustawi wa Jamii, Wauguzi na masuala yote ya Ustawi wa Jamii kwa ujumla.

Kamati ya Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevy; Kamati ya Masuala ya UKIMWI, inaongezewa jukumu la kufuatilia masuala ya matumizi ya dawa za kulevy.

Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; nimeunda Kamati ya Kufuatilia Utekelezaji wa Sera za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Hii imetokana na ukweli kwamba, Serikali yenye sasa ina Diplomasia ya Kiuchumi katika mambo yetu ya nje. Kwa hiyo, tumeona kazi hii mpaka sasa ilikuwa kidogo haijafanyika vizuri, sasa inabidi wafanye hivyo, pamoja na mambo ya Afrika Mashariki.

Tulitamani sana kuwa na Kamati ya Afrika Mashariki, lakini baada ya kujifunza sana, ikaonekana kwamba, ikiwa peke yake itakuwa haina nguvu, isipokuwa tumeondoa mambo ya ulinzi na usalama katika Kamati hii. Kwa hiyo, Kamati hii inakuwa ni ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, pamoja na Mambo ya Afrika Mashariki.

Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*), itaendelea na jukumu lake la msingi la kuchambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*) kwa Wizara na Idara za Serikali pamoja na Mashirika ya Umma, kama inavyotambuliwa Kimataifa. Kimataifa, Kamati ya Mashirika ya Umma haipo na sasa hivi tuko tumeingia katika Mfumo wa Kimataifa wa kuangalia Kamati zetu, kwa hiyo, Kamati ya Mashirika ya Umma haipo popote. Hata tulipojaribu kulazimisha i-fit

humo ikawa haiwezi ku-fit; kwa hiyo, imebidi tubakie na Kamati inayofahamika mahali pote, Kamati ya Hesabu za Serikali, itaongezewa tu idadi ya watu kwa sababu ya majukumu yake. Uamuzi huu unaondoa mwingiliano wa majukumu kati ya Kamati ya Kisekta ya Hesabu za Mashirika ya Umma.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, orodha mpya ya Kamati za Kudumu za Bunge, ni kama ifuatavyo:-

- (1) Kamati ya Uongozi;
- (2) Kamati ya Kanuni za Bunge;
- (3) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge;
- (4) Kamati ya Bajeti;
- (5) Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara;
- (6) Kamati ya Nishati na Madini;
- (7) Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala;
- (8) Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- (9) Kamati ya Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya;
- (10) Kamati ya Huduma za Jamii;
- (11) Kamati ya Maendeleo ya Jamii;
- (12) Kamati ya Miundombinu;
- (13) Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira;

- (14) Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji;
- (15) Kamati ya Ulinzi na Usalama;
- (16) Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa;
- (17) Kamati ya Hesabu za Serikali; na
- (18) Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mabadiliko haya yanaanza kutumika sasa na nimewagiza Katibu wa Bunge, agawe fomu za maombi ya kujiunga na Kamati ambazo kila Mbunge, anaweza kuchagua, kama atakavyozipendekeza kwa Spika. Hizo fomu zinatakiwa kutolewa leo hii kusudi muweze kujaza upesi, halafu tuweze kuona namna tutakavyopanga Kamati kadiri itakavyokuwa inafaa.

Baada ya taarifa yangu hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Ngwilizi kutoa taarifa yake.

TAARIFA KUHUSU FUJO ZILIZOTOKEA BUNGENI WAKATI WA MJADALA WA HOJA YA MHESHIMIWA JOHN J. MNYIKA

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI – MWENYEKITI WA KAMATI
YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni Taarifa ya uchunguzi wa Kamati, kuhusiana na vurugu zilizojitokeza Bungeni, wakati wa mjadala wa Hoja ya Mheshimiwa John Mnyika, kuhusiana na kuboresha upatikanaji wa maji safi na ushughulikiaji maji taka katika Jiji la Dar es Salaam, iliyowasilishwa Bungeni, tarehe 4 Februari, 2013.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ni mionganini mwa Kamati za Bunge ambazo zipo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la

2007. Majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Nyongeza ya 8(4), Kanuni hizo kuwa ni:-

- (i) Kuchunguza masuala yote yahusuyo haki, kinga na madaraka ya Bunge yanayopelekwa kwake na Spika.
- (ii) Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge na kujadili jambo lingine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Ni kutokana na matakwa haya ya Kanuni, Mheshimiwa Spika, baada ya kushauriana na Kamati ya Uongozi, kupitia kikao chake cha tarehe 4 Februari, 2013 aliiagiza Kamati kushughulikia suala la vurugu zilizojitokeza tarehe 4 Februari, 2013 wakati wa mjadala wa Hoja ya Mheshimiwa John Mnyika, iliyohusu Kuboresha Upatikanaji wa Majisafi na Ushughulikiwaji wa Majitaka katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ili Kamati iweze kutimiza majukumu ulioipatia, ulitoa hadidu za rejea za kuzingatiwa kuwa ni:-

- (i) Kubainisha mazingira yaliyopelekea kujitokeza kwa ukiukwaji wa Kanuni.
- (ii) Kuwabaini Wabunge waliohusika na namna walivyohusika.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekozo ya Kamati; ili kutimiza jukumu hilo Kamati ilizingatia nyaraka zifuatazo:-

- (a) Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge za kikao cha tarehe 4 Februari, 2013.

(b) Ushahidi wa tukio zima uliorekodiwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC footage*).

(c) Uamuzi wa Kiti.

Mheshimiwa Spika, ili kupata picha halisi ya kile kilichotokea Bungeni, Kamati ilianza kazi kwa kujikita katika kupitia kwa kina Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge za Kikao cha tarehe 4 Februari, 2013, kipindi cha jioni, ambazo zilitoa mwelekeo mzima wa namna kikao hicho kilivyofanyika. Pia Kamati ilipitia kwa kina Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za kikao cha Tarehe 5 Februari, 2013 ambazo zilikuwa na uamuzi uliotolewa na Spika, kuhusiana na fujo zilizojitokeza katika kikao kilichotangulia ikiwa ni pamoja na kulileta suala hili katika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili iweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati iliweza kupata *CD* yenye picha za *video* ambazo zilirekodiwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) ili iweze kuona hali halisi ilivyokuwa wakati vurugu hizo zinatokea sambamba na kuwatambua Wabunge waliohusika na tukio hilo. Baada ya Kamati kupitia mkanda wa *video* na Taarifa Rasmi ya Bunge, iliridhika na kuweza kufanya majadiliano.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupitia vielelezo hivyo kwa lengo la kupata uelewa wa kile ambacho kinapaswa kukifanyia kazi ilianza kupitia hadidu za rejea moja baada ya nyingine.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, Kamati hii uliipa hadidu za rejea ambazo zilitoa mwongozo wa namna ambavyo Kamati itatekeleza jambo hili. Kamati ilifanya kazi kwa kuzingatia hadidu za rejea hizo kwa utaratibu ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni mazingira yaliyopelekea kujitokeza kwa ukiukwaji wa kanuni. Muda wa kuwasilisha hoja. Jambo la kwanza ambalo Kamati ilibainisha kuwa lilsababisha ukiukwaji wa Kanuni ni suala la tafsiri ya muda uliotumiwa na

Mheshimiwa Waziri wa Maji wakati akichangia hoja ya mabadiliko kuhusiana na hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa John Mnyika. Kanuni ya 62(1)(b) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 53(6)(c) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, inatoa muda wa dakika zisizozidi thelathini kwa Mheshimiwa Waziri kuwasilisha hoja yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utaratibu unaoelezwa na Kanuni hii mtoa hoja ya mabadiliko ambaye ni Mheshimiwa Waziri alichangia hoja hii kwa muda uliokuwa unatakiwa. Hatua ya Mheshimiwa Tundu Lissu kuhoji uhalali wa Waziri kuchangia kwa zaidi ya dakika 15 ilijikita katika Kanuni ya 62(1)(b) ambayo inatamka kuwa:

"Kila Mbunge anayejadili hoja ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 15." Kwa tafsiri ya Mbunge huyu, alimchukulia Waziri kama vile Mbunge mwingine anavyochangia. Kwa mantiki hiyo, hakuona uhalali wa Mheshimiwa Waziri kupewa muda wa zaidi ya dakika kumi na tano.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, jambo ambalo Mheshimiwa Tundu Lissu hakulizingatia ni kwamba ili kupata uhalali wa Waziri kuchangia hoja iliyoko mbele ya Bunge kwa dakika thelathini alipaswa kusoma Kanuni ya 53(6)(c), 62(1) zikisomwa pamoja na Kanuni ya tano (5). Ni dhahiri kuwa tafsiri zinazotokana na Kanuni hizi zilitoa fursa kwa Mheshimiwa Waziri kuwasilisha hoja yake katika muda unaoelekezwa.

Mheshimiwa Spika, ingawa Mheshimiwa Naibu Spika baada ya kutakiwa kutoa ufanuzi juu ya muda huo alikiri kuwa Makatibu Mezani walipitiwa. Kamati imejiridhisha kuwa katika hili Kiti hakikuzingatia Kanuni ya 53(6)(c). Hivyo ilikuwa halali kwa Mheshimiwa Tundu Lissu akiwa kama Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kutimiza wajibu wa kuhahakikisha kuwa Kanuni za Bunge zinazingatiwa katika uendeshaji wa shughuli za Bunge.

Hivyo, hatua aliyochukua ya kukihoji Kiti na kutaka Waziri aketi chini kwa kuwa muda wake wa kuchangia hoja husika ulikuwa umekwisha haikuwa sahihi kwani ilikuwa ni kukiamrisha Kiti kinyume cha Kanuni. Kwa hiyo, hoja na dhana kwamba Kiti kilitoa upendeleo kwa Mheshimiwa Waziri haikuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, pili, utovu wa nidhamu mionganoni mwa Waheshimiwa Wabunge. Nidhamu ni jambo ambalo linapaswa kuzingatiwa wakati wote wa shughuli za Bunge ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake na wajibu wake katika hali ya utulivu na amani. Ili kuzingatiwa kwa nidhamu, Kanuni ya 60 ambayo inaelezwa kuwa ndiyo "Roho ya nidhamu" katika Bunge inapaswa kuzingatiwa sambamba na Kanuni ya 68.

Mheshimiwa Spika, wakati Kanuni ya 60(1) (a) – (c) ikieleza jinsi ambavyo Mbunge atapata nafasi ya kusema Bungeni na pia kuhakikisha kuwa mzungumzaji anakuwa mmoja wakati wote, Kanuni ya 68 inatoa utaratibu wa namna Mbunge anavyoweza kuomba nafasi ya kutoa taarifa kuhusu utaratibu na kuomba mwongozo.

Mheshimiwa Spika, katika kuchunguza iwapo kulikuwa na utovu wa nidhamu katika vurugu zilizotokea, Kamati ilibaini kuwa Kanuni hizi hazikuzingatiwa ipasavyo na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Ni dhahiri kuwa ukiukwaji wa kanuni hizi ndio ultawala katika tukio hilo. Mfano halisi ni Kanuni ya 60(2) inayomtaka Mbunge kutozungumza hadi hapo atakapoitwa na Spika ambapo ataruhusiwa kuzungumza akielekeza maneno yake kwa Spika. Kanuni hii haikuzingatiwa kwani baadhi ya Wabunge walismama na kuwashaa vipaza sauti bila ruhusa ya Kiti, hali illyosababisha kuwepo kwa majibizano na malumbano baina ya Wabunge hao na kitin.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ilibaini kutozingatiwa kwa Kanuni ya 67(1) inayomtaka Mbunge anayezungumza kwa wakati huo kuketi mahali pake mara Spika anapokuwa amesimama wakati wa mjadala, na kuanza kuzungumza. Hatua hii inalenga kuleta hali

ya utulivu ndani ya Bunge na kumwezesha Spika kutoa maelekezo au taarifa yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa ushahidi wa Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge pamoja na picha za *video* ambazo Kamati ilizitazama, Mheshimiwa John Mnyika alionekana kusimama mara kadhaa akisisitiza kwa kusema "Kuhusu utaratibu" hata wakati Naibu Spika alipokuwa amesimama. Pamoja na Kiti kutoruhusu ombi lake, Mheshimiwa John Mnyika aliendelea kusisitiza kwa kutamka maneno "Kuhusu utaratibu" hatua ambayo inabainisha utovu wa nidhamu uliofanywa na Mheshimiwa Mbunge dhidi ya Kiti.

Mheshimiwa Spika, suala la utovu wa nidhamu lillijidhihirisha pia kwa Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Joshua Nassari na Mheshimiwa Pauline Gekul ambao walionekana kuongea kwa jazba, bila ya ruksa ya Kiti huku wakitamka maneno "Kanuni zifuatwe," "Mnatuburuza," maneno ambayo hayakustahili kuongelewa kwani yaliamsha ari kwa Wabunge wengine nao kuanza kurusha maneno kwa Kiti hali iliyochochaea vurugu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua ya Mheshimiwa Joshua Nassari kukishambulia Kiti kwa kutamka maneno "Mheshimiwa Naibu Spika hayo ni matusi," "Mheshimiwa Naibu Spika umebaka Kanuni" inaonesha wazi utovu wa nidhamu na dharau vilivyoonyeshwa na Mheshimiwa Mbunge dhidi ya Kiti.

Mheshimiwa Spika, kitendo kilichofanywa na Mheshimiwa Joshua Nassari cha kujibizana na Kiti hakikuwa sahihi kwani kwa mujibu wa Kanuni ya 5(4) Mbunge ye yote ambaye haridhishwi na uamuzi wa Spika anaweza kuelezea kutoridhishwa kwake kwa kumwandikia Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika ambaye atapeleka jambo hilo kwenye Kamati ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya Waziri kutaka kuondoa hoja ya Mheshimiwa John Mnyika; wakati wa uwasilishaji wa hoja yake Mheshimiwa Waziri alinukuu Kanuni ya 57(1)(c) ambayo ilimruhusu kupendekeza mabadiliko katika Hoja Binafsi iliyowasilishwa na Mheshimiwa John Mnyika. Katika mchango wake huo nanukuu:-

"Kwa kuwa hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu ni kuitaka Serikali kuchukua hatua za haraka kuboresha huduma za Majisafi na uondoaji wa Majitaka katika Jiji la Dar es Salaam ambao tayari unatekeleza mpango maalum uliotengewa fedha nyingi na Serikali ya Chama cha Mapinduzi na kuzingatia kwamba utekelezaji wa mpango huo unaendelea vizuri sana, hivyo basi, napendekeza hoja hiyo iondolewe." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, maneno ya Mheshimiwa Waziri yaliibua hisia tofauti miongoni mwa Wabunge kiasi cha kutaka kufahamu Kanuni au utaratibu unaomwezesha Waziri kuleta hoja ya mapendekezo ya kuondoa hoja badala ya kubadilisha hoja ya msingi iliyokuwa imewasilishwa na Mheshimiwa John Mnyika.

Mheshimiwa Spika, Kimsingi hoja inaweza kuondolewa na mtoa hoja pekee kwa kuomba ruhusa Bungeni. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 58(5). Hivyo hivyo, dhana kwamba, Waziri alitoa hoja inayolenga kuondoa hoja ya Mheshimiwa Mnyika haikuwa sahihi kwa kuwa hakuna Kanuni yoyote inayoruhusu jambo hili kufanyika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kanuni hiyo hiyo katika Fasili ya nne (4) inazuia kufanyika kwa badiliko lolote ambalo kwa maoni ya Spika linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa. Kwa mantiki hiyo, iwapo hoja ya Mheshimiwa Waziri ilikuwa inalenga kubadili msingi wa hoja ya Mheshimiwa Mnyika ni wazi kwamba Kiti kisingeruhusu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Kanuni za Bunge hazifafanui kuhusu maneno gani hasa yatumike katika kuongeza au kupunguza maneno mapya wakati wa kuifanyia mabadiliko hoja

iliyowasilishwa, Kamati imejiridhisha kuwa, jambo hili lilitokea kutokana na upungufu wa Kanuni.

Mheshimiwa Spika, ili kuepuka uwepo wa tafsiri tofauti miongoni mwa Wabunge kuhusiana na maneno yapi yanapaswa kuingizwa au kuongezwa wakati wa kuifanyia hoja mabadiliko, Kamati inashauri kuwa ni vema Kanuni ya 57(1)(c) itamke wazi muktadha wa maneno ambayo yanaweza kutumika katika kuingiza au kuongeza maneno mapya.

Mheshimiwa Spika, kufuatia Kanuni hiyo kutokuwa wazi, Kamati imebainisha kuwa hoja iliyotolewa na Mheshimiwa John Mnyika ililenga katika kulitaka Bunge liazimie kwamba, Serikali ichukue hatua haraka zaidi za kuboresha upatikanaji wa maji safi na ushughulikiaji wa maji taka katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa kuzingatia hoja hiyo na azimio la Mheshimiwa Waziri ambalo lilikuwa linabainisha kwamba, tayari Serikali iko katika utekelezaji wa hoja ilijoibuliwa na Mheshimiwa John Mnyika, hivyo azimio la Mheshimiwa Waziri lilikuwa ni kulitaka Bunge likubaliane na utekelezaji unaofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 58(5) ambayo inaeleza wazi kuwa hoja inaweza kuondolewa na Bunge, baada ya mwenye hoja kutoa pendekemo ni dhahiri kwamba, hoja ya Waziri haikulenga kuondoa hoja ya Mheshimiwa John Mnyika kwa sababu hakuwa mwenye hoja isipokuwa kuliomba Bunge lizingatie azimio jipya ambalo lilitolewa kupitia hoja ya Mheshimiwa Waziri. Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni 57(1)(c) Mheshimiwa Waziri hakuondoa hoja bali alitumia Kanuni hii kuongeza maneno kwa kuweka azimio jipya alilolitoa na kuomba Bunge liweze kuamua hoja yake.

Mheshimiwa Spika, hatua ya Naibu Spika kulihoji Bunge juu ya kuondoa hoja bila kufanyika kwa mjadala:-

Mheshimiwa Spika, baada ya mawasiliano yaliyofanywa na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa mwongozo wa namna ya kuchangia hoja hiyo. Kwa mujibu wa Kumbukumbu za

Taarifa Rasmi za Bunge, wapo Waheshimiwa kadhaa ambao walijitokeza kwa lengo la kuchangia hoja hiyo kama ilivyoelekezwa na Kiti. Hata hivyo, ni mchangiaji mmoja tu ndiye alisimama kwa lengo la kuchangia, lakini mara tu alipoanza kutoa mchango wake ziliibuka fujo zilizomfanya ashindwe kuendelea na uchangiaji.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kwa fujo hizo na kukosekana hali ya utulivu ndani ya Bunge ambayo kulisababisha kukiukwa kwa Kanuni ya 60(2) inayomtaka Mbunge kutozungumza hadi aitwe na Spika kwa kutajwa jina au wadhifa wake na Kanuni ya 60(12) inayowataka Wabunge kukaa chini wakati wote Spika anaposimama kutaka kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kanuni ya 72(1) inampa Spika wajibu wa kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatwa Bungeni na uamuzi wake kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho. Hivyo basi, uamuzi uliochukuliwa na Kiti wa kusitisha mjadala na kulihoji Bunge juu ya hoja husika ulikuwa sahihi kwa mujibu wa Kanuni ya 76(1) inayoelekeza juu ya udhibiti wa fujo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na madai iwapo hoja ya Waziri iliondolewa bila kuchangiwa, Kamati imejiridhisha kuwa, hakuna Kanuni inayotaja idadi ya wachangiaji wanaotakiwa ili kuweza kuhitimisha hoja, isipokuwa mamlaka hayo yapo mikononi mwa Kiti na kwa kuzingatia mazingira na muda uliopo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa hoja ilifikia hatua ya kujadiliwa na kulikuwa na dhamira hiyo kwani Kiti kilikuwa kimeorodhesha majina ya wachangiaji kadhaa, lakini kilichokwamisha utekelezaji wa hatua hiyo ni mtoa hoja kufanya fujo na kukosekana kwa hali ya utulivu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, suala la amani na utulivu Bungeni ni jambo la muhimu katika kuhakikisha shughuli za Bunge zinaendeshwa ipasavyo. Kamati inapata tafsiri kuwa uamuzi uliochukuliwa na Naibu Spika katika kuhitimisha hoja ya Mheshimiwa Mnyika kabla ya hoja ya Mheshimiwa Waziri ililenga kuzingatia kanuni ya 72(1) ambayo inampa Spika mamlaka ya kusimamia utaratibu. Aidha, uamuzi huo

ulilenga kuzingatia Kanuni ya 76(1) inayompa Spika mamlaka ya kudhibiti fujo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, iwapo kulikuwa na malalamiko kwamba, hatua ya Kiti haikufuata utaratibu katika kufanya maamuzi hayo, bado Kanuni zinamruhusu Mbunge ambaye hakuridhika na maamuzi ya Kiti kukata rufaa kwenye Kamati ya Kanuni za Bunge, hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 5(4).

Mheshimiwa Spika, kutojadiliwa kwa hoja za mabadiliko zilizowasilishwa na Wabunge wengine:-

Mheshimiwa Spika, suala la kutokujadiliwa kwa hoja za mabadiliko zilizowasilishwa na Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Susan A.J. Lyimo na Mheshimiwa Peter S. Msigwa ilikuwa ni mionganini mwa mambo yaliyosababisha kujitokeza kwa mazingira ya ukiukwaji wa Kanuni. Kanuni ya 58 ya Kanuni za Bunge imeweka masharti ya namna ya kushughulikia mapendekezo ya mabadiliko yote kwenye hoja ya msingi na Spika amepewa mamlaka ya kuamua mpangilio atakaouona unafaa.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi uamuzi wa Kiti kuamua kushughulikia kwanza hoja ya mabadiliko iliyowasilishwa na Waziri kabla ya kutoa nafasi kwa hoja zingine za mabadiliko ulikuwa sahihi kwa mujibu wa Kanuni ya 58(2). Aidha, uwasilishwaji wa hoja uliofanywa na waziri ulizingatia Kanuni ya 53(6)(c) inayotoa fursa kwa msemaji wa Serikali kuwa mchangiaji wa kwanza kwa hoja ambayo sio ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuzingatiwa kwa Kanuni hizo uchangiaji wa hoja hizo haukufikiwa kutokana na vurugu zilizokuwa zimejitokeza. Kamati imejiridhisha kuwa kilichokwamisha hoja hizo kutojadiliwa ni kukosekana na hali ya utulivu na sio ukiukwaji wa Kanuni kama ilivyodaiwa na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mpaka hapo ndiyo uchunguzi wa Kamati umefikia na naomba kuwasilisha taarifa hii. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa maana ya haki za binadamu, wale ambao walionekana kama wao ndiyo walifanya uchochezi, hawajapata nafasi ya kuitwa wao wenyewe wakaongea. Kwa sababu hiyo tu ni kwamba, wasingefika kwenye kiwango cha kutoa adhabu kwa sababu hao walioonekana kama ni wanachochaea, hawakupata nafasi ya kukutana na Kamati. Kwa hiyo, mpaka watakafanya hivyo tutaangalia adhabu wanazostahili. Ndiyo sababu wamefanya uchambuzi kwa sababu uchambuzi ulikuwa rahisi kwa sababu *TBC* inayo kila kitu na watu mliona, lakini kufikia pale wahusika hawakupata nafasi ya kuulizwa, ndiyo maana tumefikia hapa.

KUAHIRISHA BUNGE

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, tumekuwepo hapa Bungeni, Dodoma kwa takriban siku 11 ambapo leo tunahitimisha shughuli zilizopangwa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge lako Tukufu. Nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa Rehema kwa kutufikisha salama siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao katika ajali mbalimbali zilizotokea hapa nchini, ikiwemo ajali ya Jahazi la *Sunrise* iliyotokea Wangwi katika Bahari ya Hindi na ajali ya lori kule Mbarali ambapo watu wamepoteza maisha na kupata majeraha.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunawapa pole majeruhi wote na abiria waliopoteza mali katika ajali hizo. Kwa kipekee kabisa napenda kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa Askofu Thomas Laiser wa KKKT, Dayosisi ya Kaskazini Kati – Arusha, ambaye amefariki jana jioni na Askofu Mstaafu Amedeus Msarikie wa Kanisa

Katoliki, Jimbo la Moshi ambaye amefariki usiku wa kuamkia leo huko Nairobi alikokuwa anapata matibabu. Wote tunawapa pole sana.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu jumla ya Maswali 116 ya Msingi na 286 ya nyongeza yalipatiwa majibu. Vile vile, Maswali sita yaliulizwa na kujibiwa kwa utaratibu wa Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Miswada ifuatayo ilisomwa kwa mara ya Kwanza:

- (a) Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2013 (*The Cooperative Societies Bill, 2013*); na
- (b) Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2013 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments, Bill 2013*).

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2012 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Act, 2012*) ulisomwa kwa mara ya Pili na kupitia ngazi zake zote.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, pia Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kuwasilisha Hoja Binafsi kama ifuatavyo:-

- (1) Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Mwigulu L. Nchomba, Mbunge wa Iramba Magharibi ya kuitaka Serikali iwasilishe Bungeni Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Elimu ya Juu (*The Higher Education Fund Act*);
- (2) Hoja Binafsi ya Mheshimiwa James F. Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa kuhusu udhaifu ulioko katika Sekta ya Elimu Nchini;
- (3) Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla, Mbunge wa Nzega ya kuitaka Serikali ianzishe Mpango Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana na kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya

Vyama wanaowekeza kwenye Kilimo na Viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na Kilimo; na

- (4) Hoja Binafsi ya Mheshimiwa John J. Mnyika, Mbunge wa Ubungo juu ya Kuboresha Upatikanaji wa Maji Safi na ushughulikiaji wa Maji Taka katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge waliweza kujadili na kupitisha Maazimio Mawili yafuatayo:-

- (i) Azimio la Bunge la Kujinga na Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhali fu Dhidi ya Watu wenyé Kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia (*Convention on The Prevention and Punishment of Crimes Against Internationally Protected Persons Including Diplomatic Agents 1973*); na
- (ii) Azimio la Bunge la Kujinga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia (*International Convention for Suppression of Act of Nuclear Terrorism, 2009*).

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kukamilisha Mijadala hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee Taifa letu limejaliwa na Mwenyezi Mungu kutimiza miaka zaidi ya 51 ya Uhuru likiwa bado linaendelea kudumisha Umoja wa Kitaifa. Umoja huu wa Kitaifa umejengwa kwenye nguzo na misingi imara ya amani, utulivu na mshikamano. Mimi naamini sote tunapaswa kujivunia Umoja huu wa Kitaifa ambao ni Tunu kubwa na nguzo muhimu ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, msingi mkubwa wa Umoja wa Kitaifa tunaoshuhudia leo uliwekwa na malezi mazuri ya Waasisi wa Taifa hili wakiongozwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Abeid Amani Karume. Aidha, Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania inasisitiza, pamoja na mambo mengine, kujenga jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na amani. Ni jukumu la kila Mwananchi kulinda Umoja huu ambao hauna mbadala.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina Makabila zaidi ya 120 ambayo kwa Mujibu wa Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 yamefikisha idadi ya watu milioni 44.929. Aidha, hivi sasa tuna Madhehebu ya Dini yaliyoandikishwa takriban 885 na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zaidi ya 6,675 na tumejenga Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa ambapo hadi sasa tuna Vyama vya Siasa 19 ambavyo vimepata Usajili wa Kudumu.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa idadi kubwa ya watu wa Makabila tofauti yenye desturi mbalimbali na makundi mbalimbali ya Madhehebu ya Dini, Itikadi za Kisiasa na watu wenye rangi mbalimbali, bado tunajivunia kwamba tunaheshimiana na hatubaguani kwa namna yoyote ile. Hali hii ya amani imeipatia nchi yetu sifa Kitaifa na Kimataifa na mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na demokrasia pana iliyopo, wananchi wetu wana uhuru mkubwa wa kutoa maoni, kuanzisha na kuijunga na Vyama vya Siasa pamoja na kushiriki katika kuchagua Viongozi wa Chama chochote wanachokipenda kwa kuzingatia misingi ya Katiba na Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Serikali imetoa uhuru mkubwa wa kupata na kutoa habari kwa uwazi bila vikwazo vyovoyote kwa kuzingatia Katiba, Sheria na Kanuni mbalimbali na Maadili ya Vyombo vya Habari. Kutokana na uhuru huo, idadi ya Vyombo vya Habari imeongezeka sana ambapo hadi sasa idadi ya Vituo 86 vya Redio vimepewa Leseni na vinafanya kazi, Vituo vya Televisheni 26 na Magazeti 768 yaliyoandikishwa na yanayotolewa na Taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo yanayodhishirika wazi, hivi karibuni kumekuwepo na dalili za kupoteza sifa yetu nzuri ya umoja wa Kitaifa na amani ambayo imedumu kwa miaka mingi. Tumeshuhudia wananchi mmoja mmoja wakishindwa kuvumiliana, japo kwa tatizo dogo tu mionganini mwao. Aidha, tumeshuhudia Vyama vya Siasa vikiongesha dalili ya kuhamasisha Wanachama wao kuingia kwenye malumbano ya siasa baina yao wenyewe kwa wenyewe au baina ya Chama kimoja cha Siasa na Chama kingine. Baadhi ya Wanachama wameshikana mashati na kujeruhiana.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwaasa Viongozi wa Vyama vya Siasa kuepuka kutumia majukwaa ya siasa kuvuruga amani yetu na utulivu uliopo. Waepuke matamko ya vitisho na kuhamasisha Wanachama wao kuendeleza vitendo vya uvunjifu wa amani na kujenga chuki na uhasama mionganini mwa Jamii na kwa Serikali halali iliyopo madarakani. Pamoja na kutofautiana kwa mawazo na Sera za Vyama vya Siasa, ni muhimu tujenge mazingira ya kuvumiliana kwa hali ya juu katika kujenga Demokrasia ya kweli hapa nchini. Viongozi wa Vyama wanatakiwa kueleza Sera zao badala ya kutukanana, kubezana, kushutumiana na kuzomeana. Tujenge nchi yetu kwa amani na utulivu ndipo tutapata maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia pia kuibuka kwa migogoro ya Kidini. Baadhi ya Waumini wa Dini wamekuwa wakikashifu Dini nyingine kwa kejeli na vitendo vingine visivyostahili. Naomba kusitiza kwa Madhehebu ya Dini yana nafasi kubwa ya kujenga umoja wa Kitaifa, amani na mshikamano. Nawaomba viongozi wa Madhehebu ya Dini, kutatua kwa amani migogoro iliyopo na kuelimisha waumini wao kuthamini, kujenga na kuenzi amani na utulivu uliopo nchini. Serikali imetoea uhuru wa wananchi wake kuabudu, kila mtu kwa Dini anayoitaka. Hivyo, hakuna sababu ya Dini moja kukashifu Dini nyingine. Aidha, tupinge kwa nguvu zetu zote chokochoko za Kidini ambazo zimeanza kujitokeza katika sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Napenda kusisitiza kuwa kama ilivyokuwa kwa Vyombo vingine, yana jukumu kubwa la kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujenga umoja wa Kitaifa. Viongozi ya Mashirika haya wasaidie Taifa kuendelea kulinda amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari kwa upande mwingine, vina wajibu mkubwa wa kuelimisha umma na kuhabarisha kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo. Aidha, Vyombo hivi vina fursa nzuri ya kutumia uhuru uliopo kudumisha amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizopo za baadhi ya watu waotaka kubomoa umoja wa Taifa letu na kuhatarisha amani na utulivu nchini, sisi kama Taifa hatuna budi kufanya yafuatayo:-

- (i) Serikali, wananchi na Wadau wote ikiwemo Vyama vya Siasa, Madhehebu ya Dini, Vyombo vya Habari, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kadhalika tunapaswa tukae chini tuzungumze na kutafakari kuhusu hali hii, kwa njia ya majadiliano;
- (ii) Tunapaswa kwa namna zote tuvumiliane na kuheshimiana kwa kuzingatia Utamaduni wa Kitanzania na misingi ya amani na utulivu tuliojjijengea kwa muda mrefu; na
- (iii) Wananchi wote tuzingatie na kuheshimu Utawala Bora wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwaomba sana wananchi na Watanzania wenzangu kuendeleza umoja na mshikamano wa Kitaifa ili kudumisha amani na utulivu uliopo nchini. Ni vyema kutambua kuwa, amani na utulivu uliopo nchini ni mazingira wezeshi ya kusaidia kila mmoja wetu kufanya shughuli zake

za kijamii na kiuchumi na kujiletea maendeleo. Bila amani na utulivu hakuna maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali itahakikisha kwamba, umoja tulioijengea unadumishwa. Taasisi mbalimbali za Serikali, zikiwemo Vyombo vya Dola ni lazima zihakikishe kwamba, wananchi wanaishi kwa amani na utulivu. Vile vile, kuhakikisha kuwa, umoja wa Kitaifa tulioujenga kwa miaka mingi haupotei. Naziomba Taasisi zote zinazohusika na kusimamia amani na usalama kuhakikisha kuwa, pamoja na changamoto zilizopo, umoja wa Kitaifa ni lazima adumishwe kwa gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanyika hivi karibuni juu ya upatikanaji wa chakula nchini na athari za mvua zinazoendelea kunyesha, inaonesha kuwa maeneo mengi hasa, yale yanayopata mvua za msimu kama vile Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Iringa, Tabora na Mtwara mazao mengi yapo katika hatua mbalimbali za ukuaji na yanaendelea vizuri. Inatarajiwa kwamba, endapo mvua hizi zitaendelea vema, upatikanaji wa chakula katika maeneo hayo utakuwa mzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hiyo ya hewa, tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe iliyofanyika mwezi Januari, 2013 inaonesha upungufu wa chakula katika Wilaya 47 zilizoko katika Mikoa 15 ambazo zitahitaji msaada wa chakula katika vipindi tofauti. Inakadiriwa kuwa jumla ya watu 1,615,445 watahitaji chakula jumla ya tani 32,870 katika vipindi hivyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matarajio hayo ya uhaba wa chakula, Serikali itahakikisha kuwa Kitengo cha Hifadhi ya Chakula cha Taifa (kinaendelea kusambaza mahindi katika maeneo yenye uhaba wa chakula). Hadi sasa jumla ya tani 20,000 zilishatolewa kwa Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Dodoma, Singida, Morogoro, Lindi, Tanga, Mtwara, Pwani, Dar es Salaam, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara na Tabora.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kitengo hicho kitaendelea kununua nafaka mapema baada ya mavuno ili kuhakikisha kuwa Serikali ina hifadhi ya kutosha ya chakula kwa ajili ya kusambaza katika maeneo yatakayokuwa na uhaba wa chakula. Hadi tarehe 6 Februari, 2013 Ghala la Taifa la Chakula lilikuwa na jumla ya tani 68,712.9 za mahindi pamoja na tani 3,335.989 za mtama.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya upatikanaji wa chakula nchini na kuhakikisha kuwa hakuna mwananchi atakayepoteza maisha kutokana na njaa. Nitoe wito kwa wananchi kuendelea kuweka utaratibu wa kuhifadhi sehemu ya mavuno yao baada ya kuvuna kwa ajili ya akiba ya baadaye badala ya kuuza mavuno yao yote.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inayo changamoto kubwa ya kukabiliana na magonjwa makubwa duniani, yakiwemo Malaria, Kifua Kikuu, UKIMWI, Saratani na kadhalika. Niruhusu leo katika Hotuba yangu nizungumzie kidogo kuhusu ugonjwa wa Malaria. Ugonjwa wa Malaria bado unaongoza kuwa sababu kubwa za wagonjwa wengi wanaohudhuria katika Vituo vya Huduma za Afya nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, ugonjwa huu unaongoza kwa kusababisha vifo, hasa kwa Watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Takwimu kutoka Vituo vya kutolea huduma ya Afya nchini zinaonesha kuwa, takriban wagonjwa milioni 11 hadi 12 huhudhuria katika Vituo vya Huduma za Afya kwa sababu ya ugonjwa wa *Malaria*. Vilevile, tafiti zilizofanyika katika Jamii (*Tanzania HIV/Malaria Indicator Survey 2011/2012*) zinaonesha kuwa asilimia 10 ya watoto katika kaya wana maambukizi ya vimelea vya ugonjwa wa *Malaria*.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo hili katika kuhakikisha wananchi wanaendelea kujikinga na maambukizi dhidi ya ugonjwa wa *Malaria*, Serikali imefanya mambo muhimu yafuatayo:-

- (1) Kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Mapambano Dhidi ya Ugonjwa wa Malaria wa Miaka Mitano, 2008-2013; ambao una lengo la kupunguza vifo kwa Asilimia 80 ifikapo mwaka 2013 mwishoni. Utekelezaji wa Mpango huu unafanyika kwa kushirikiana na Mikoa, Wilaya na Wadau mbalimbali hadi katika ngazi ya Jamii;
- (2) Kusambaza na kuongeza matumizi ya vyandarua vyenye viuatilifu vya muda mrefu katika Kaya. Hadi sasa zaidi ya vyandarua milioni 26 vimesambazwa kupitia Kampeni iliyolenga Watoto wenyewe umri chini ya miaka mitano;
- (3) Kutekeleza Mpango wa Hati Punguzo unaolenga kuhakikisha akinamama wajawazito na watoto wanaozaliwa wanaendelea kupata vyandarua hivyo na kujikinga dhidi ya ugonjwa wa *Malaria*;
- (4) Kuendeleza Mpango wa kunyunyizia dawa ya ukoko majumbani ili kutokomeza mazalia ya mbu. Mpango huo unaendelea kutekelezwa katika Mikoa ya Kagera, Mwanza na Mara ambapo zaidi ya Kaya 1,440,000 sawa na asilimia 90 katika Wilaya za Mikoa hiyo zitanyunyiziwa viuatilifu. Kutokana na Mpango huo, zaidi ya watu 6,500,000 wameendelea kukingwa dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa Malaria;
- (5) Kuendeleza Mpango wa kuangamiza viluwiluwi vya Mbu kwa kutumia njia za Kibaiolojia. Mpango huu ambao unafanywa na Serikali kwa ushirikiano na Serikali ya nchi ya Cuba unatekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam kuanzia mwaka 2011;
- (6) Kutumia Mwongozo wa kutibu ugonjwa wa Malaria isiyo kali kwa kutumia Dawa ya Mseto ya *ALU*. Mwongozo huu unaendelea kutumika katika Vituo vyote vya Umma vya kutolea huduma za Afya; na

- (7) Kusambaza kipimo cha haraka cha kutambua na kuthibitisha uwepo wa vimelea vya Malaria kwenye damu katika Vituo vyote vya Umma vya kutoa huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa yaliyopatikana, bado kuna changamoto ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi. Changamoto hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- (a) Kujitokeza kwa usugu wa mbu dhidi ya viuatilifu vya aina ya *pyrethroids* vinavyotumika katika vyandarua na unyuziaji dawa ya ukoko majumbani;
- (b) Kupata vyanzo zaidi vya fedha za ndani za kuendeleza mkakati wa unyunyiziaji dawa ya ukoko majumbani;
- (c) Uwezo mdogo wa uzalishaji wa dawa za kuangamiza viluwiluwi vya mbu na kuanza kuangamiza viluwiluwi hivyo katika Jiji la Dar es Salaam; na
- (d) Kuendeleza uhamasishaji wananchi kutumia nyenzo na kushiriki katika mikakati iliyopo, hasa inayohitaji ushiriki wao wa moja kwa moja, kama kuharibu mazalia ya mbu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kupambana na Malaria Duniani, Shirika la *Roll Back Malaria Partnership* wakishirikiana na Wizara ya Afya ya Afrika Kusini wanatarajia kufanya Mkutano mkubwa unaohusu mapambano dhidi ya Malaria kwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*) kuanzia tarehe 9 - 11 mwezi huu. Mkutano huo unatarajia kukutanisha Viongozi wa ngazi ya juu kutoka Nchi za *SADC* ikiwa ni pamoja na baadhi ya Marais, Mawaziri Wakuu, Mawaziri wa Afya na Mawaziri wa Michezo katika nchi hizo. Mkutano huo pia utajumuisha Viongozi wa juu wa Makampuni mbalimbali ya Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, lengo la Mkutano huo ni kukutanisha Viongozi mbalimbali kwa lengo la kuendesha mjadala kuhusu janga la Malaria katika Nchi za Afrika; ikizingatiwa kuwa ufadhili wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali unazidi kupungua. Mkutano huo unategemewa kuwa chachu kwa Viongozi kuongeza Bajeti za udhibiti wa Malaria nchini mwao na kuongeza ushirikiano na Sekta Binafsi pamoja na Sekta ya Michezo, hasa katika Mpira wa Miguu katika dhana nzima ya Mpango wa *Safe Companies*. Aidha, Mkutano huo unatarajiwa kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa, Mkutano huo utakuwa wa mafanikio makubwa kwa Nchi za Kusini mwa Afrika katika vita dhidi ya ugonjwa wa Malaria. Vile vile, utatupatia uzoefu kwa nchi yetu katika kupambana na ugonjwa huu wa Malaria.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kupambana na *Malaria* nchini, Muungano wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walianzisha Asasi inayojulikana kama *Tanzania Parliamentary Against Malaria (TAPAMA)*. Lengo la kuanzishwa kwa Asasi hii ni kuongeza utashi wa Kisiasa katika kushiriki na kutekeleza Mpango na Sera ya Taifa ya kutokomeza Ugonjwa wa *Malaria* nchini. Asasi hii ilisajiliwa mwaka 2008 na hadi sasa imetekeliza masuala mbalimbali katika jitihada zake za kupambana na *Malaria* nchini kama ifuatavyo:-

(a) Ugawaji wa vyandarua kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi kwa Mikoa ya Ruvuma, Kilimanjaro na Mwanza ambapo zaidi ya watoto 2,500 walifaidika na huduma hiyo;

(b) Kufanya mazungumzo na Wawakilishi wa Bunge la Jumuiya ya Ulaya mwaka 2009 waliotembelea Tanzania na kuona uwezekano wa Jumuiya ya Ulaya kusaidia zaidi Mapambano dhidi ya Malaria Tanzania. Aidha, walifanya mazungumzo na Viongozi na Wawakilishi wa Asasi ya Malaria No More ya Marekani, ambao waliongozwa na

Balozi Mark Green na kuwezesha kuanza kwa Mradi wa Zinduka, Malaria Haikubaliki;

(c) Kushiriki Kikao cha Nchi za Jumuiya ya Ulaya nchini Ufaransa mwaka 2009 ili kujadili juhudzi za Viongozi wa Kisiasa katika Kupambana na Malaria nchini; na

(d) Kushiriki kutayarisha Mwongozo (Advocacy Guideline) utakaotumiwa na Wabunge, Madiwani na Viongozi wengine wa Kisiasa na Kijamii katika Utekelezaji na ushawishi wao katika kutokomeza Malaria Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Wajumbe wote wa *TAPAMA* chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge wa Viti Maalum kwa juhudzi zao za kuhakikisha kuwa wanaungana na Wadau wengine nchini na duniani katika kutokomeza ugonjwa wa Malaria. Nazipongeza pia Taasisi Zisizo za Kiserikali kwa ujumla wao ambazo zimejitokeza katika mapambano dhidi ya magonjwa mbalimbali, yakiwemo UKIMWI, Kifua Kikuu, Saratani na kadhalika. Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge zaidi wazidi kujejunga na Asasi za aina hii na hasa magonjwa ili kuweka hamasa kwa wananchi katika kupambana na maradhi hayo.

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa wito kwa wananchi wote kwa ujumla kuunganisha nguvu za kupambana na ugonjwa huu wa *Malaria* ili kunusuru nguvukazi ya Watanzania. Suala kubwa ni kuzingatia masharti ya Wataalam kuanzia katika kutunza mazingira yetu na kutumia Vyandarua kama kinga iliyo ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imetangaza kumaliza kazi ya kukusanya maoni binafsi ya wananchi mmoja mmoja kama mchango wao kwa ajili ya kuandika Katiba Mpya. Aidha, imekamilisha kazi ya kukutana na Makundi Maalum, Viongozi wa Kitaifa Wastaifu na Viongozi wa Kitaifa waliopo Madarakani.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, Tume sasa imekamilisha kazi ya ukusanyaji maoni kama ilivyopangwa. Hivi sasa Tume inaendelea na kazi za uchambuzi wa maoni yaliyotolewa na wananchi na yale yaliyotolewa na makundi mbalimbali ili baadaye kutayarisha Rasimu ya Katiba ambayo itawasilishwa katika Mabaraza ya Katiba yatakayoitishwa na Tume nchini kote.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Ratiba, Mikutano ya Mabaraza ya Katiba itafanyika kuanzia mwezi Juni, 2013 na itajumuisha Wajumbe watakaochaguliwa na wananchi wenyewe kuanzia ngazi ya Kijiji. Wajumbe hao ndio watapaswa kuwasilisha maoni ya wananchi katika Mikutano ya Mabaraza.

Mheshimiwa Spika, nimearifiwa kuwa Tume imeandaa Rasimu ya Mwongozo wa namna bora na ya Kidemokrasia ya kuwapata Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ambao unaendelea kusambazwa nchi nzima. Mwongozo huo tayari umetangazwa katika Vyombo vya Habari ili wananchi waufahamu na kutoa maoni kuhusu namna ya kuuboresha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Rasimu hiyo ya Mwongozo, katika Mikoa ya Tanzania Bara ukiondoa Mkoa wa Dar es Salaam, kila Kata itawakilishwa na Wajumbe wanne (4) watakaochaguliwa kutoka mionganini mwa wakazi wa Vijiji vilivyopo kwenye Kata ambao wataungana na Madiwani wa Kata na Madiwani wa Viti Maalum kuunda Baraza la Katiba la Wilaya. Mkoa wa Dar es Salaam, Tume imeandaa utaratibu tofauti wa kuwapata Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ambapo kila Kata watatoka Wajumbe wanane (8) ambao wataungana na Madiwani wa Kata na Madiwani wa Viti Maalum. Kwa msingi huo, kutakuwa na jumla ya Wajumbe 18,169 watakaohudhuria Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar, kutakuwa na Mabaraza ya Katiba ya Wilaya, Ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa 13. Kila Shehia itawakilishwa na Wajumbe watatu (3), ambao wataungana na Madiwani wa Wadi, Madiwani wa Viti Maalum na

Madiwani wa kuteuliwa waliopo kazini kwa sasa. Kwa msingi huo, Wajumbe wote wa Mabaraza ya Katiba kwa Zanzibar watakuwa 1,198.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaopenda kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya watatakiwa kuwasilisha majina yao kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa kwa Tanzania Bara na kwa upande wa Tanzania Zanzibar watawasilisha kwa Sheha kwa tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Viongozi wote katika ngazi za Wilaya na Serikali za Mitaa, mwongozo huo utakapokuwa umekamilika kusimamia kikamilifu utaratibu ambao utawekwa na Tume. Kwa kufanya hivyo, Wajumbe ambao watashiriki katika Mabaraza ya Katiba watapatikana kwa njia za kidemokrasia na hivyo, kufanikisha Vikao vya Mabaraza ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa wananchi watasoma hiyo rasimu ya Mwongozo sasa na kutoa maoni yao, ili kuuboresha kabla haujafanyiwa maamuzi ya mwisho na baadaye mwongozo huo utakapokuwa umekamilika ndipo utaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi wote, wote kwa ujumla wetu kushiriki kikamilifu katika kuuboresha Mwongozo huo na pia kuwapata Wajumbe watakaoshiriki katika Mabaraza hayo, kwa mujibu wa Sheria na vilevile Wajumbe hao washiriki kikamilifu katika Vikao vya Mabaraza ya Katiba na kutoa maoni kwa Rasimu ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza dhamira ya uwazi na ujenzi wa pamoja wa utawala bora nchini kwa kuwashirikisha wananchi, nchi yetu imekuwa mionganii mwa nchi 33 za Umoja wa Afrika zilizoamua kwa hiari yake kuijunga na Mpango wa Bara la Afrika wa Kujitathmini Kiutawala Bora (*The African Peer Review Mechanism - APRM*). Tanzania ilijunga na mchakato huo mwaka 2004 na Bunge liliuridhia mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu wa kujitathimini Kiutawala Bora ni muhimu kwetu na unaakisi Sera zetu na za Waasisi wa Taifa hili juu ya Kujikosoa na Kujisahihisha. Aidha, unahuishisha Viongozi wa Afrika na unatoa fursa kwa wananchi kutathmini hali ya utawala bora katika nchi zao na kuainisha kwa pamoja mambo mazuri yanayopaswa kuendelezwa na yale yenyе changamoto za kufanyiwa kazi. Mionganoni mwa sababu za nchi yetu kujeunga na Mpango huu ni kutokana na ukweli kwamba Watanzania tuna mengi ya kuifundisha Afrika na watu wake kuhusu utawala bora na sisi pia kujifunza kutoka kwa wenzetu.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, baada ya zoezi la muda mrefu la kukusanya maoni nchi nzima kuhusu Mpango huu ambapo Waheshimiwa Wabunge nao walishiriki kutoa maoni yao kuhusu utawala bora, sasa hivi nchi yetu, imefikia hatua muhimu katika mchakato huo wa kujitathmini kiutawala bora.

Tarehe 26 Januari, 2013, Ripoti ya Hali ya Utawala Bora hapa nchini iliwasilishwa mbele ya Wakuu wa Nchi za APRM Addis Ababa, Ethiopia ambapo Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu alipata fursa ya kuzungumzia mwelekeo wa nchi yetu katika kujenga Taifa imara zaidi katika kipindi cha miaka 50 ijayo.

Mheshimiwa Spika, katika Ripoti hiyo ambayo itatumika kama rejea, zimeainishwa juhudhi zetu kubwa za kulinda amani nchini. Pamoja na kuimarisha utawala bora wa Sheria na Haki za Binadamu. Aidha, kupitia Ripoti hiyo, wenzetu katika masuala ya kuendesha utawala bora, Barani Afrika na Duniani kwa ujumla wametambua jitihada zetu pamoja na mambo mengine katika kuulinda Muungano, kuimarishwa kwa mapambano dhidi ya rushwa na zaidi ya yote wamejua sura ya Tanzania katika ukombozi na utetezi wa amani Afrika ambao nchi yetu imepongezwa sana kwa juhudhi zake. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Ripoti hiyo imeainisha changamoto ambazo wenzetu wa Afrika wanadhani tunapaswa kuzifanyia kazi zaidi. Changamoto hizo ni pamoja na suala la kushughulikia Kero za Muungano, kuimarisha zaidi juhudzi za kuondoa umaskini na kuilinda amani ya nchi yetu hasa kutokana na chokochoko za Kidini zilizoanza kujitokeza. Tumeaswa kuutumia vyema mchakato wa sasa wa Mabadiliko ya Katiba kuijenga Tanzania bora zaidi katika miaka 50 ijayo.

Mheshimiwa Spika, kuwasilishwa kwa Ripoti hiyo ya *APRM* kwa Wakuu wa Nchi wa Mpango huu ndiyo mwanzo sasa wa Serikali yetu kuimarisha maeneo yaliyoonekana kuwa tunafanya vyema. Pia hatua hiyo inatoa fursa ya kuanza kutekeleza Mpangokazi wa Miaka Mitano ambao umeainisha namna gani ya kuyafanyia kazi maeneo ambayo wananchi waliyaona kuwa yanapaswa kufanyiwa kazi zaidi. Suala hili liliwekewa msisitizo na Mheshimiwa Rais katika Hotuba yake ya Mwisho wa Mwezi Januari, 2013 aliyoitao kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na manufaa ya *APRM* kama daraja kati ya Serikali na wananchi la kutatua matatizo yetu kwa pamoja, Serikali itaendelea kuiimarisha Taasisi ya *APRM* hapa nchini ili iweze kuwa kitovu chetu cha fikra katika kushauri kuhusu masuala ya utawala bora nchini. Vile vile, kuiwezesha Taasisi hii kuendelea kuwa kiungo kati ya Serikali yetu na wananchi wake katika kutathmini na kutupatia mrejesho juu ya mipango na Sera zetu za maendeleo.

Aidha, Serikali itaendelea kufadhili shughuli za *APRM*, kuiimarisha Taasisi kwa rasilimali watu na fedha kwa ajili ya kazi pana zaidi za kutoa ushauri, kuunganisha Wadau mbalimbali na kuendelea kuratibu tathmini nyingine katika siku zijazo kwa lengo la kujipa nafasi ya kujikosoa ili kujisahihisha. Napenda kutumia nafasi hii, kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama wakishirikiana na Sekretariati ya *APRM* Tanzania kwa kazi nzuri sana waliyofanya ambayo imetuwezesha kufikia hatua hayo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa, mwezi Machi 2012, Mheshimiwa Rais aliridhia kuanzisha Mikoa Mipyä Minne (4) na Wilaya Mpya 19. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali sasa imekamilisha mchakato wa kuanzisha maeneo hayo Mapya ya Utawala, kwa kuanzisha Mikoa Minne ya Geita, Simiyu, Njombe na Katavi. Aidha, imekamilisha uanzishwaji wa Wilaya 19 za Buhigwe, Busega, Butiama, Chemba, Gairo, Ikungi, Itilima, Kakonko, Kalambo, Kaliua, Kyerwa, Mbogwe, Mkalama, Mlele, Momba, Nyang'wale, Nyasa, Uvinza na Wang'ing'ombe. Mikoa na Wilaya hizo tayari zimeshaanza kufanya kazi na kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Vilevile, Mheshimiwa Rais alishafanya uteuzi wa Viongozi Wakuu wa Mikoa na Wilaya Mpya.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kupeleka Watumishi na kuanza kujenga miundombinu muhimu katika maeneo husika. Hata hivyo, pamoja na dhamira njema ya Serikali ya kuanzisha maeneo hayo, bado zipo changamoto nyingi, ikiwemo kupata Watumishi wa kutosha ambazo Serikali inaendelea kuzitatua.

Mheshimiwa Spika, ili kupeleka huduma karibu zaidi na wananchi, Serikali pia iliazimia kuanzisha Halmashauri Mpya 37. Uanzishaji wa Halmashauri hizo unaendelea na upo katika hatua mbalimbali kwa kuzingatia makundi yafuatayo:-

Kundi la Kwanza, linahusu Halmashauri Mpya nane za Manispaa, Miji na Jiji pamoja na Halmashauri Moja (1) ya Wilaya ambazo mchakato wa uanzishaji wake tayari umekamilika Kisheria na zimeanza kufanya kazi. Kundi hili linajumuisha Halmashauri za Jiji la Arusha, Manispaa ya Illemela, Manispaa ya Lindi, Halmashauri ya Mji wa Kahama, Halmashauri ya Mji wa Masasi, Halmashauri ya Mji wa Makambako, Halmashauri ya Mji wa Geita, Halmashauri ya Mji wa Bariadi na Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo. Halmashauri hizo tayari zimepata Hati na kupangiwa Wakurugenzi, isipokuwa Jiji la Arusha tunakamilisha uteuzi wake.

Kundi la Pili, linajumuisha Halmashauri Kumi (10) ambazo mchakato wa kuzianzisha umekamilika na tayari zimetangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 23 Novemba, 2012. Halmashauri hizo ni Kalambo, Nsimbo, Mlele, Bumbuli, Ushetu, Msalala, Mbogwe, Busega, Momba na Kyerwa. Halmashauri hizo kwa sasa zinaandalialiwa Hati ili zianze, zitafuatiwa na uteuzi wa Wakurugenzi, tayari kwa ajili ya kuanza shughuli za utekelezaji katika Halmashauri hizo.

Kundi la Tatu, ni Halmashauri za Wilaya Kumi (10) ambazo mchakato wake, uko katika hatua ya uhakiki ambao sasa umekamilika na Amri za Uanzishwaji zimesainiwa na wakati wowote zitatangazwa katika Gazeti la Serikali. Kundi hili linajumuisha Halmashauri za Wilaya za Buhigwe, Kaliua, Nyang'hwale, Wang'ing'ombe, Chembu, Mkalama, Gairo, Nyasa, Itlima na Kakonko. Aidha, zipo Halmashauri nyingine Nne (4) katika kundi hili ambazo Amri zake zinakamilishwa na hatimaye zitasainiwa hivi karibuni. Halmashauri hizo ni Butiama, Tarime, Uvinza na Ikungi.

Mheshimiwa Spika, kundi la nne, linajumuisha Halmashauri nne ambazo Mchakato wa uanzishaji wake umekamilika isipokuwa taratibu za Kisheria haziwezi kuanza kwa sababu baadhi ya Kata katika Halmashauri hizo ni mpya, hivyo hakuna Madiwani. Halmashauri hizo nne (4) ni za Miji ya Kasulu, Handeni, Tunduma na Nzega. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu kuna Kata 14 na kati ya hizo, Kata sita ni mpya na hazina Madiwani. Kwa upande wa Halmashauri ya Mji wa Handeni ina jumla ya Kata 12, kati ya Kata hizo tisa ni mpya na hazina Madiwani. Aidha, Halmashauri ya Mji wa Tunduma ina Kata tano mpya na zote hazina Madiwani na Halmashauri ya Mji wa Nzega ina Kata 10 na kati ya hizo Kata tatu ni mpya na hazina Madiwani.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha maeneo hayo mapya ni kuwawezesha wananchi kupata huduma karibu zaidi. Nitoe wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Watendaji wote kuwaongoza wananchi kutumia fursa hiyo ya kuanzishwa kwa maeneo hayo katika kujiletea maendeleo. Serikali kwa upande wake itaendelea kupeleka huduma

zaidi karibu na wananchi ili kuongeza kasi ya maendeleo katika maeneo hayo. Vile vile Serikali itaweka utaratibu wa kuzipatia Halmashauri zinazoanzishwa Watumishi hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Novemba, 2012, Bunge lilipitisha Azimio Na. 9/2012 kuhusu kuitaka Serikali kuchukua hatua dhidi ya Watanzania walioficha fedha haramu nje ya nchi kufuatia Hoja Binafsi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe. Azimio hilo linahitaji, pamoja na mambo mengine, Serikali iwasiliane na Benki ya Dunia kupitia Kitengo cha *Asset Recovery Unit* ili mabilioni yanayomilikiwa na Watanzania katika Mabenki nje ya nchi ambapo hufichwa kwa kukwepa kulipa kodi yarudishwe na kwamba Watanzania wote wenye akaunti za fedha nje ya nchi waeleze wamezipataje ili TAKUKURU iwachukulie hatua za Kisheria dhidi ya watu wote wenye kumiliki fedha na mali kinyume na mapato yao halali. Aidha, iliazimiwa na Bunge na Serikali ikakubali kwamba, katika Mkutano wa Bunge wa 11 italeta Taarifa ya hatua iliyochukuliwa ili kuziba mianya ya utoroshaji wa fedha nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Desemba, 2012, Mheshimiwa Rais aliridhia kuundwa kwa Kamati Maalum ya Kitaifa kushughulia hoja hiyo ya kuitaka Serikali kuchukua hatua dhidi ya Watanzania walioficha fedha haramu nje ya nchi. Kamati hiyo inaundwa na Wajumbe wanane wanaotoka katika Taasisi za Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; Jeshi la Polisi; Benki Kuu ya Tanzania; Usalama wa Taifa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kazi za Kamati hiyo ni zifuatazo:-

- (i) Kuchunguza na kubaini majina ya Watanzania wanaodaiwa kuficha fedha nje ya nchi kinyume na Sheria na Kanuni za Nchi;
- (ii) Kuchunguza iwapo fedha hizo ni haramu au la;
- (iii) Kutambua Mabenki na nchi zilizofichwa fedha hizo;

- (iv) Kuandaa mashtaka dhidi ya Watanzania watakaobainika kuficha fedha haramu nje ya nchi; na
- (v) Kuishauri Serikali jinsi ya kuzuia uhalifu wa makosa ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imeanza kazi zake rasmi tarehe 9 Januari, 2013 kwa kupanga namna ya kutekeleza kazi zake ikiwemo kukusanya taarifa kuhusu Watanzania wanaodaiwa kutorosha fedha haramu nje ya nchi na kuangalia namna ya kupata taarifa muhimu nje ya nchi. Kamati hiyo inaratibiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi yake kwa ufanisi ni wazi kwamba, itahitaji kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wananchi kwa kutoa taarifa mbalimbali kuhusu suala hili. Hivyo, naomba kutoa wito kwa wananchi wote wenye taarifa sahihi na za kweli zinazoweza kuisadia Kamati kutekeleza kazi hii, kujitokeza kutoa maoni yao kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kushirikiana kwa karibu na Kamati iliyoundwa na Serikali. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wabunge nao kutoa ushirikiano wa kufanikisha kazi ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napenda niwashukuru wote waliofanikisha Mkutano huu wa Kumi wa Bunge. Kipekee nikushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kutuongoza vizuri ndani ya Bunge lako Tukufu. Nimshukuru vile vile, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha Vikao vya Bunge kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. Nimshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake kwa huduma nzuri walizozitoa wakati wote tukiwa hapa.

Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru Watendaji wa Serikali na Taasisi mbalimbali kwa kutekeleza majukumu yao vizuri ili kufanikisha shughuli za Bunge zilizopangwa. Niwashukuru Waandishi wa Vyombo vya Habari kwa kutufikishia habari kwa wananchi juu ya yale yaliyojiri hapa Bungeni na kwa wakati. Vile vile, navishukuru Vyombo vya Ulinzi

na Usalama kwa kazi yao nzuri na Madereva wote kwa huduma zao kwa washiriki wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niwatakie safari njema na sasa nitoe hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi Siku ya Jumanne tarehe 9 Aprili, 2013 saa tatu asubuhi kwenye Ukumbi huu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeungwa mkono, tumshukuru sana Waziri Mkuu kwa hotuba yake, sasa tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge waliiimba
Wimbo wa Taifa*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa naomba nimshukuru Waziri Mkuu kwa maneno ya busara ya kufunga Kikao chetu cha Bunge la Kumi. Pia nichukue nafasi hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi tulioifanya katika Mkutano huu wa Kumi, haidhuru kulikuwa na dosari mbalimbali, tena nydingi tupu, kwa hiyo nadhani tumetia aibu kwa wananchi wetu, kweli kabisa tumetia aibu. Mimi sijasema nani, lakini tumetia aibu, sisi kama kama Wabunge wa Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ndugu zangu nadhani ni wakati mzuri wa sisi wenyewe kutafakari. Ni vizuri kutafakari, nchi kama Marekani, pamoja na tofauti zao zote, lakini kuna uzalendo ndani yake.

Waheshimiwa Wabunge, jamani sisi tunalinda amani ya nchi hii. Narudia kila siku! Kujadili hoja kwa msingi wa hoja jamani si vibaya, na naomba hili suala tuendelee nalo. Haidhuru umoja wa Vyama

vyenye Wabunge humu ndani walikaa jana na moja ya azimio lao tuangalie Kanuni za Bunge na sisi tuko tayari kufanya hivyo. Pia walisisitiza, tujitahidi kutatua matatizo yetu kwa njia ya amani. Wamesisitiza katika lile azimio lao. Tujitahidi kwa sababu amani ni tunu tuliyopewa na Mwenyezi Mungu na inabidi ilindwe.

Waheshimiwa Wabunge, zaidi ya hapo nasema hapa ndani kila mtu anatawaliwa na Kanuni. Hata mimi kama Spika, natawaliwa na Kanuni, hata kama nina makosa, tutafute Kanuni namna ya kumfanyia kazi Spika, lakini tusifanye, vitendo ambavyo vinaonekana mbele ya uso wa watu kwamba sisi hatuna nidhamu.

Naomba sana hili tulizingatie na kila mtu awe mtu mzima, kwa sababu tumepewa dhamana na watu wengi sana, kila tunakotoka wanatutegemea kufanya vile walivyokuwa wametutegemea sisi tufanye. Bado naendelea kuomba Serikali muongeze fedha za kuweza kuisimamia *TVya TBC*. (*Makofii*)

Safari hii ilikuwa inakatika katika sana, kwa hiyo naamini wananchi hawakuiona vizuri. Tuimarishe hiyo *TV* kwa sababu ndiyo *TV* ya wananchi.

Waheshimiwa Wabunge mimi kama kiongozi wenu, mkisema yote, hata mkinirushia matusi mimi nakubali, si ndiyo maana ya kiongozi! Kiongozi ni jalala, kiongozi yoyote ni jalala! Kwa hiyo, yote yanayokuja wala! Ni sehemu ya wajibu ambao mimi ninao. Lakini najua mimi ni Spika, mtaendelea kunijibu kwa mujibu wa taratibu na hamna namna nyingine. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mtuelewe, mimi ni jalala, mkisema vyovyote wala haisumbui sana, kwa sababu *dustbin* ukimwaga kila kitu inapokea tu! Ukienda Chama Tawala unaambiwa wewe unapendelea Upinzani, ukienda Upinzani wanasema unapendelea Chama Tawala, maana yake sipendelei, ndiyo maana yake! (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nisiseme maneno mengi, nashukuru kwa kazi tuliyofanya, lakini tumejifunza, tumeona kwenye hoja binafsi, inhabidi tuweke utaratibu mzuri zaidi, kwa sababu hapa ndipo hatukuelewana sana. Tuweke utaratibu ulio mzuri zaidi kwa sababu tulikuwa tumetoa nafasi kwa hoja binafsi nyingi kipindi hiki na inaelekea bado haijaaelewaka vizuri, lakini naamini hatutaacha zile hoja kuzileta, tutazileta bado, siyo kwamba tumeziondoa. Tulitaka kuondoa shari ambayo ilikuwa inaendelea, lakini siyo kwamba zimeondolewa kwa maana kwamba hazitakuja.

Waheshimiwa Wabunge, nirudie tu, tufuate kanuni zetu, wale wenyе hoja zao wanaweza kuzifufua tena ili ziweze kuja kwa wakati wake.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba niwatakie safari njema, huko mnakokwenda mkafanye kazi zenu kwa mujibu wa tarabu na mkawahudumie wananchi kama inavyostahili. (*Makofi*)

Naomba nitoe maelezo kwamba, hizi fomu tumekosea kidogo, mahali pa kujaza majina palikuwa hapaonekani, ingawa wamerekebisha sasa hivi. Mzirudishe hapa Dodoma au Dar es Salaam, kusudi kazi nyingine ziweze kuendelea. Kama mmerudisha ni vizuri, ni hapa Dodoma au Dar es Salaam. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba niwatakie safari njema, naahirisha kikao cha Bunge, mpaka tarehe 9 Aprili, 2013 saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

*(Saa 11.25 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 9 Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO I

ISSN 0856 --- 035X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BILL SUPPLEMENT

NO. 4

5th October, 2012

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 40 Vol. 93 dated 5th October, 2012

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam, by Order of Government

THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2012

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Sections Title

**PART I
PRELIMINARY PROVISIONS**

1. Short title.
2. Amendment of certain written laws.

**PART II
AMENDMENT OF THE ANTI-MONEY LAUNDERING ACT,
(CAP. 423)**

3. Construction.
4. Amendment of section 3.

PART III
AMENDMENT OF THE ANTI-TRAFFICKING IN PERSONS ACT,
(CAP. 432)

5. Construction.
6. Amendment of section 3.

PART IV
AMENDMENT OF THE MAGISTRATES' COURTS ACT,
(CAP. 11)

7. Construction.
8. General amendment of the Act.
9. Amendment of section 2.

PART V
AMENDMENT OF THE LAND ACT,
(CAP. 113)

10. Construction.
11. Amendment of section 2.
12. General Amendment.

PART VI
AMENDMENT OF THE PUBLIC AUDIT ACT,
(CAP. 418)

13. Construction.
14. Amendment of section 37.
15. Amendment of section 38.
16. Amendment of section 39.
17. Repeal of section 40.

PART VII
AMENDMENT OF THE PUBLIC SERVICE RETIREMENT BENEFITS ACT,
(CAP. 371)

- 18. Construction.
- 19. Amendment of section 9.

PART VIII
AMENDMENT OF THE REGULATION OF LAND TENURE
(ESTABLISHED VILLAGES) ACT,
(CAP. 267)

- 20. Construction.
- 21. Amendment of section 2.

PART IX
AMENDMENT OF THE WARD TRIBUNAL ACT,
(CAP. 206)

- 22. Construction.
- 23. Amendment of section 19.
- 24. Amendment of section 22.
- 25. Amendment of section 23.

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,
5th October, 2012

OMBENI Y. SEFUE,
Secretary to the Cabinet

A BILL

for

An Act to amend certain written laws.

ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I

PRELIMINARY PROVISIONS

PART I

PRELIMINARY PROVISIONS

- Short title 1. This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No. 3) Act, 2012.

Amend
ment of
certain
written
laws

2. The written laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner provided for in their respective Parts.

Construc
tion
Cap.
423

3. This Part shall be read as one with the Anti-Money Laundering Act, hereinafter referred to as the "principal Act."

Amend
ment of
section 3

4. The principal Act is amended in section 3, in the definition of the term "terrorist financing" by-

(a) deleting the word "or" appearing at the end of paragraph (a);

(b) deleting a "full stop" appearing at the end of paragraph (b) and substituting for it the word "; or";

(c) adding immediately after paragraph (b) the following new paragraph:

" (c) any other act constituting terrorist financing as provided in the Prevention of Terrorism Act."

PART II

AMENDMENT OF THE ANTI - MONEY LAUNDERING ACT, (CAP. 423)

PART III
AMENDMENT OF THE ANTI-TRAFFICKING IN PERSONS ACT,
(CAP. 432)

Construction
Cap.
432

5. This Part shall be read as one with the Anti-Trafficking in Persons Act, hereinafter referred to as the "Principal Act."

Amendment of section 3

6. The principal Act is amended in section 3 by inserting in its appropriate alphabetical order the following new definition:

"court" means the Court of Resident Magistrate or the District Court".

PART IV
AMENDMENT OF THE MAGISTRATES' COURTS ACT,
(CAP. 11)

Construction
Cap.11

7. This Part shall be read as one with the Magistrates' Courts Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

General amendment of the Act

8. The principal Act is generally amended by deleting the words "primary court magistrate" wherever the words appear in the Act and substituting for them the word "magistrate".

Amendment of section 2

9. The principal Act is amended in section 2 by deleting the definition of the term "magistrate" and substituting for it the following new definition:

"magistrate" means a district magistrate or a resident magistrate and includes a civil magistrate and honorary magistrate;"

PART V
AMENDMENT OF THE LAND ACT,
(CAP. 113)

Construc
tion Cap.
113

10. This part shall be read as one with the Land Act, hereinafter referred to as the "Principal Act".

Amend
ment of
section 2

11. The principal Act is amended in section 2 by deleting the definition of the term "Land Division of the High Court" and substituting for it the following new definition:

"High Court" means the High Court of Tanzania established under Article 108 of the Constitution of the United Republic;"

General
Amend
ment

12. The principal Act is generally amended by deleting the term "Land Division of the High Court" wherever it appears in the Act and substituting for it the term "High Court".

PART VI
AMENDMENT OF THE PUBLIC AUDIT ACT,
(CAP. 418)

Construction
Cap.
418

13. This Part shall be read as one with the Public Audit Act, hereinafter referred to as the "principal Act."

Amendment of
section
37

14. The principal Act is amended in section 37 by deleting subsection (3).

Amendment of
section
38

15. The principal Act is amended by deleting section 38 and substituting for it the following-

38.-(1) The Public Accounts Committee, Local Authorities Accounts Committee and Parastatal Organisations Accounts Committee shall discuss the reports of the Controller and Auditor-General after they have been tabled in the National Assembly.

(2) For the purpose of response to discussion under subsection (1), the accounting officers shall respond to the Controller and Auditor General's report and shall prepare an action plan of the intended remedial actions for submission to the Paymaster General;

(3) In preparing the responses and

action plans, the accounting officer shall take into account the observations and recommendations of the oversight committee on financial affairs established by the National Assembly.

(4) The Paymaster General shall consolidate responses and action plan received under subsection (2) and shall-

- (a) submit a consolidated report of responses and action plan to the Minister who shall lay it before the National Assembly; and
- (b) submit to the Controller and Auditor-General a copy of such consolidated report.

(5) Upon completion of discussions and hearing, the parliamentary oversight committees shall prepare and submit to the National Assembly a report which may include comments and recommendations.

(6) The reports submitted in accordance with subsection (5) shall be discussed by the National Assembly together with the consolidated report of the responses and action plan submitted by the Minister under subsection 4(a)".

Amend
ment of
section
39

16. The principal Act is amended by deleting section 39 and substituting for it the following-

39. All audit reports issued by the Controller and Auditor General shall be public documents after being tabled in the National Assembly."

Repeal
of
section
40

17. The principal Act is amended by repealing section 40.

PART VII

AMENDMENT OF THE PUBLIC SERVICE RETIREMENT BENEFITS ACT, (CAP. 371)

Construc
tion
Cap.
371

18. This Part shall be read as one with the Public Service Retirement Benefits Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amend
ment of
section 9

19. The principal Act is amended in section 9(4) by-

(a) deleting paragraphs (a), (b), (c) and (d) and substituting for them the following:

"(a) in the case of the rank of a Warden or Wardress, the age of voluntary retirement shall be forty five years and compulsory age of retirement shall be fifty years;

- (b) in the case of the officer of the rank of a Corporal, Sergeant, Staff sergeant or Regiment Sergeant Major the age of voluntary retirement shall be fifty years and the age of compulsory retirement shall be fifty five years;
- (c) in the case of the officer of the rank of Assistant Inspector, Inspector, Assistant Superintendent, Superintendent, Senior Superintendent, Assistant Commissioner, Senior Assistant Commissioner, Deputy Commissioner, Commissioner or Commissioner General the age of voluntary retirement shall be fifty five years and the age of compulsory retirement shall be sixty years".

PART VIII
AMENDMENT OF THE REGULATION OF LAND TENURE
(ESTABLISHED VILLAGES) ACT,
(CAP. 267)

Construc
tion Cap.
267

20. This Part shall be read as one with the Regulation of Land Tenure (Established Villages) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amend
ment of
section 2

21. The principal Act is amended in section 2 by deleting the definition of the term "High Court" and substituting for it the following new definition:
" "High Court" means the High Court of

the United Republic of Tanzania established under Article 108 of the Constitution of the United Republic;"

PART IX

AMENDMENT OF THE WARD TRIBUNAL ACT, (CAP. 206)

Construction
Cap.
206

22. This Part shall be read as one with the Ward Tribunal Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of
section
19

23. The principal Act is amended in section 19 by deleting the words "Primary Court Magistrate" wherever the words appear in that section and substituting for them the word "magistrate".

Amendment of
section
22

24. The principal Act is amended in section 22 by deleting the words "Primary Court Magistrate" wherever the words appear in that section and substituting for them the word "magistrate".

Amendment of
section
23

25. The principal Act is amended in section 23 by deleting the words "Primary Court Magistrate" appearing in subsections (2) and (3) and substituting for them the word "magistrate".

OBJECTS AND REASONS

This Bill makes legislative proposal for amendment of laws specified in Part II to Part IX with a view to remedy shortfalls that have been experienced in the course of administration and implementation of those laws. The amendments are aimed at facilitating effective implementation of the amended laws.

This Bill is divided into Nine Parts.

Part I provides for the preliminary provisions which include the short title and a statement underlying the purpose of the Bill.

Part II proposes amendment to the Anti-Money Laundering Act, Cap 423. Under this Part, section 3 of the Act is amended by adding a new paragraph (c) in the definition of the term "terrorist financing" so as to incorporate in that definition acts specified under the Prevention of Terrorism Act which will now constitute acts of terrorist financing.

Part III proposes amendment to the Anti-Trafficking in Persons Act, Cap. 432. In this Part section 3 of the Act is amended by adding the definition of the term "court". The term court is not currently defined in the Act; the addition of the definition in the Act will clarify on the appropriate court to institute a suit arising from the offences prescribed under this Act.

Part IV proposes amendment of the Magistrates' Courts Act, Cap.11. It is proposed under this Part that, the Act be generally amended by deleting the words "primary court magistrate" wherever they appear in the Act and substituting for them the word "magistrate." Clause 5 proposes to amend section 2 whereas the definition of the term "magistrate" is substituted by the new definition

which includes district magistrate, or resident magistrate, civil magistrate and honorary magistrate. The proposed amendment intends to phase out the primary magistrates so as to allow resident magistrate to preside over cases tried by the Primary Courts.

Part V proposes amendment to the Land Act, Cap. 113. Under the said proposal, the definition of the term "Land Division of the High Court" is substituted generally for the definition of the term "High Court" and the term "High Court Land Division" is substituted generally for the term "High Court". The amendments are intended to enable the High Court of Tanzania to exercise its jurisdiction over the land matters instead of the Land Division of the High Court which is no longer recognized by other Land laws.

Part VI proposes amendment to the Public Audit Act Cap. 418. Under this part sections 37, 38 and 39 are amended generally and section 40 is repealed, so as to provide for a Chronological response by Government on the Controller and Auditor General's report to be laid before the National Assembly. The amendments further seek to provide for the report of the Parliamentary oversight committees together with consolidated responses and action plan of the Government to be simultaneously discussed by the National Assembly.

Part VII proposes amendments to the Public Service Retirement Benefits Act, Cap. 371. The amendments are intended to be effected in section 9(4) whereby the age of voluntary and compulsory retirement to the prisons' officers are extended to match with the age of retirement of police officers.

Part VIII proposes amendment to the Regulation of Land Tenure (Established Village) Act, Cap 267. Under the said proposal the definition of the term "High Court" is substituted with the intention to enable the High Court of Tanzania to exercise its jurisdiction over the land matters instead of the Land Division of the High Court which is no longer recognized by other Land laws.

Part IX proposes the amendment to the Ward Tribunal Act, Cap. 206. Under the said proposal, section 19, 22 and 23 of the Act are amended by deleting the words "Primary Court Magistrate" wherever they appear in those sections and substituting for them the word "magistrate". The proposal intends to phase out primary magistrate so as to allow primary courts to be presided over by other magistrates prescribed under these amendments, especial Resident magistrates.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu wa Sheria unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali zilizoainishwa kwenye Sehemu ya Pili hadi Sehemu ya Tisa ili kuondoa mapungufu ambayo yamedhihirika wakati wa kutekeleza baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria hizo. Marekebisho yanakusudio la kuwezesha utekelezaji bora wa sheria zinazorekebishwa.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tisa.

Sehemu ya Kwanza inaweka masharti ya Utangulizi, ambayo yanajumuisha jina la Muswada pamoja na maudhui ya Muswada.

Sehemu ya Pili ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, Sura ya 423 kwa kuongeza aya (c) kwenye tafsiri ya neno kufadhili gaidi ("terrorist financing"). Lengo la kuongeza aya hiyo ni kujumuisha matendo yanayokatazwa chini ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi kama matendo yanayozuiwa chini ya Sheria hii.

Sehemu ya Tatu ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisheso kwenye Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 kwa kuongeza tafsiri ya neno Mahakama. Kwa sasa Sheria haina tafsiri ya neno "mahakama", marekebisheso yanayopendekezwa yana kusudio la kutoa ufanuzi juu ya Mahakama inayopaswa kufungua mashtaka endapo sheria imekiukwa.

Sehemu ya Nne inakusudia kufanya marekebisheso kwenye Sheria ya Mahakama za Mahakimu , Sura ya 11. Kifungu cha nne kinapendekeza marekebisheso ya jumla ndani ya Sheria hiyo, kwa kufuta maneno "hakimu wa mahakama ya mwanzo" popote lilipo ndani ya Sheria na badala yake kuingiza neno "hakimu". Kifungu cha tano kinapendekeza kufanya marekebisheso kwenye kifungu cha pili, kwa kufuta tafsiri ya neno "hakimu" na kuingiza tafsiri mpya inatakayo jumuisha Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu Wakazi. Marekebisheso hayo yana kusudio la kufuta sifa za mahakimu wa mahakama za mwanzo ili kuwawezesha Mahakimu Wakazi au Mahakimu wa Wilaya kusikiliza kesi katika Mahakama za Mwanzo.

Sehemu ya Tano inapendekeza kufanyiwa marekebisheso Sheria ya Ardhi,Sura ya 113. kwa kufuta tafsiri ya neno "Land Division of the High Court" na badala yake kubadilisha tafsiri hiyo na tafsiri ya neno "High Court" na kufuta maneno "High Court Land Division" popote yanapoonekana ndani ya Sheria badala yake yasomeke maneno "High Court". Marekebisheso hayo yanalenga kuipa mamlaka Mahakama Kuu ya Tanzania kusikiliza kesi za Ardhi badala ya Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi pekee.

Sehemu ya Sita inapendekeza kufanya marekebisheso kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma Sura 418. Marekebisheso haya yanapendekeza kurekebisha vifungu vya 37, 38,39 na kufuta kifungu cha 40 ili kuweka utaratibu mzuri wa Serikali kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowasilishwa Bungeni. Marekebisheso hayo pia yanakusudio la kuweka utaratibu wa Bunge

kujadili taarifa ya Kamati za Bunge sambamba na majibu na mpango mkakati wa Serikali.

Sehemu ya Saba inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mafao ya Kustaafu kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371. Marekebisho katika Sheria hii yanapendekezwa kufanywa katika kifungu cha 9(4) ambapo umri wa hiari na umri wa lazima wa kustaafu Maafisa Magereza unaongezwa ili ulingane na umri wa kustaafu kwa Maofisa wa Polisi.

Sehemu ya Nane inapendekeza kufanyiwa marekebisho katika Sheria ya Kusimamia Umiliki wa Ardhi katika Vijiji vilivyokwisha anzishwa, Sura ya 267 kwa kufuta tafsiri ya neno "High Court" na badala yake kubadilisha tafsiri hiyo kwa lengo la kuipa mamlaka Mahakama Kuu ya Tanzania kusikiliza kesi za Ardhi badala ya Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi pekee.

Sehemu ya Tisa inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mabaraza ya Kata, Sura 206. Kifungu cha 7 kinapendekeza kufanya marekebisho kwenye vifungu 19, 22 na 23 vya Sheria, kwa kufuta maneno "Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo" popote yanapotokea katika Sheria na badala yake kuingiza neno "hakimu". Marekebisho hayo yana kusudio la kufuta hadhi ya Hakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kuwawezesha Mahakimu kama inavyopendekezwa katika Muswada huu ili waweze kusikiliza kesi katika Mahakama za Mwanzo.

Dar es Salaam,
3 Oktoba, 2012

FREDERICK M. WEREAMA,
Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. FREDERICK M.
WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL DURING THE SECOND READING OF
A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS
AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2012"**

Made under S.O. 86(10) (b)

The Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Act, 2012" is amended generally as follows:

A In Clause 4(c) by deleting the proposed : paragraph (c) and substituting for it the following:

"(c) knowingly solicits support for, or rendering financial support to a terrorist, group or entity which is associated with terrorist acts."

B: By -

deleting Clauses 8 and 9 and substituting for them the following:

"Amend
ment of
section 6

8. The principal
Act is amended in

section 6(1) by adding the words "or a Resident Magistrate" after the word "magistrate" appearing in paragraph (a).

Amendment of section 7

9. The principal Act is amended by repealing section 7 and substituting for it the following:

"Assessors

7. In any proceeding in a magistrates' court in which any rule of customary or Islamic law is in issue or relevant, the court may, and when directed by an appropriate judicial authority, sit with an assessor or assessors, and every such assessor shall be required,

before judgment, to give his opinion as to all questions relating to customary or Islamic law in issue, or relevant to the proceeding; save that in determining the proceeding the court shall not be bound to conform with the opinion of the assessors."

C By - inserting the following new : provisions-

Amendm
ent of
section
13

10. The principal Act is amended in section 13 by deleting the word "Kiswahili" appearing in subsection (1) and substituting for it the words "either Kiswahili or English."

Amendm
ent of
section
18

11. The principal Act is amended in section 18(1) by deleting paragraph (b) and substituting for it the following:

“(b)in all matrimonial Cap. 29 proceedings in the manner prescribed under the Law of Marriage Act.”

Amendm
ent of
Part VI

12. The principal Act is amended in Part VI by-

deleting the words “PRIMARY COURT MAGISTRATES” appearing in the heading of that Part and substituting for them the words “A MAGISTRATE IN THE PRIMARY COURT”; and

deleting the words "*Primary Court Magistrates*" appearing in sub-heading (b) and substituting for them the words "*a Magistrate in the Primary Court*".

Amendment of section 58

13. The principal Act is amended in section 58 by adding the words "or resident magistrate" immediately after the words "primary court magistrate" wherever they appear in that section."

(b) renumbering Clauses 10 to 13 as Clauses 14 to 17 respectively.

D By-
:

(a) deleting Clause 14;

(b) renumbering Clauses 15 to 25 as Clauses 18 to 28 respectively.

E: In Clause 18 as renumbered by deleting the proposed section 38 and substituting for it the following –

Parliamentary oversight committee

38.-(1) The Public Accounts Committee, Local Authorities Accounts Committee and Parastatal Organisations Accounts Committee shall discuss the reports of the Controller and Auditor-General and the consolidated report referred to under subsection 2(a) after they have been tabled in the National Assembly.

(2) For the purpose of preparation of a consolidated report refereed to under subsection (1)-

the accounting officers shall prepare an action plan of the intended remedial

actions for submission to the Paymaster General;

the Paymaster General shall consolidate responses and action plan received under subsection (2) and shall:

submit a consolidated report of responses and action plan to the Minister who shall lay the report to the National Assembly;

submit to the Controller and Auditor General a copy of such

consolidated report.

(3) The report of the Minister under subsection (2) (b) (i) shall be laid before the National Assembly concurrently with the report of the Controller and Auditor General.

(4) Upon completion of discussions and hearing, the parliamentary oversight committees shall prepare and submit to the National Assembly a report which may include comments and recommendations.

(5) The reports submitted in accordance with subsection (4) shall be discussed by the National Assembly together with the consolidated report of the responses and action plan submitted by the Minister under

subsection (2)(b)(i).

F: In Clause 19 as renumbered by-

designating the proposed section 39
as section 39(1); and

adding a new subsection as follows:

"(2) Every statutory report that constitutes a public document shall be discussed by the National Assembly after it has been deliberated upon by the Parliament Oversight Committees in the manner prescribed under section 38(5), and in accordance with the procedures prescribed by the Parliament."

G By deleting Clause 20 as renumbered : and substituting for it the following-

"Amend
ment of
section
40

20. The principal Act is amended by repealing section 40 and substituting for it the following-

"Annual Audit report of Controller and Auditor General

40. In preparing the Annual Audit report, the Controller and Auditor General shall incorporate an implementation status of the action plan prepared by accounting officers and consolidated by the Paymaster General."

H: In Clauses 26, 27 and 28 as renumbered by deleting the word "magistrate" and substituting for it the words "Primary Court Magistrate or Resident Magistrate".

Dodoma,
6th February, 2013

FMW
AG

**SCHEDULE OF AMENDMENT SUBMITTED BY HON. SELEMANI JAFO FOR
THE SCHEDULE OF AMMENDMENT MOVED BY THE HON. FREDERICK M.
WEREMA, THE ATTORNEY GENERAL DURING THE SECOND READING
OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS
(MISCELLANEOUS AMMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2012"**

Made under S.O. 86(9, 11) and 88(2)

On the last line of schedule of amendment on section 9

Add the word "**customary**" between the word 'the' and'

Remove the full stop and add the following words "**but, shall bound
to conform with the opinion of the Islamic assessors on matter relating
marriage, divorce, and inheritance.**"

The section shall read:-

In any proceeding in a magistrates' court in which any rule of customary or Islamic law is in issue or relevant, the court may, and when directed by an appropriate judicial authority, sit with an assessor or assessors, and every such assessor shall be required, before judgment, to give his opinion as to all questions relating to customary or Islamic law in issue, or relevant to the proceeding; save that in determining the proceeding the court shall not be bound to conform with the opinion of the customary assessors, but, shall bound to conform with the opinion of the Islamic assessors on matter relating marriage, divorce, and inheritance.

Selemani Said Jafo (MP)
Kisarawe Constituency

**SCHEDULE OF AMMENDMENT TO BE MOVED BY HON. HALIMA MDEE,
MEMBER OF PARLIAMENT - KAPEWE CONSTITUENCY DURING THE SECOND
READING OF A BILL TITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS
AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2012"**

Made under S.O. 88(2)

The Bill titled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2012" is amended generally as follows:-

A: By

Deleting the entire section 15 of the Act.

Dodoma

HALIMA MDEE
(MP)

7th February, 2013

SCHEDULE OF AMMENDMENT TO BE MOVED BY HON. DR. HAMISI KIGWANGALLA (MP), NZEGA CONSTITUENCY DURING THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2012"

Made under S.O. No. 88(2), (6), 86(11) AND 57(7)

The Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2012" is generally amended as follows:-

B: By-

Deleting Clause 9 and substituting for it the following:

(9) The principal Act is amended by repealing section 7 and substituting for it the following:

(7) In any proceeding in a magistrates' court in which any rule of customary or Islamic law is in issue or relevant, the court shall, and when directed by an appropriate judicial authority, sit with an assessor or assessors, and every such assessor shall be required, before judgment, to give his opinion as to all questions relating to customary or Islamic law in issue, or relevant to the proceedings; and that in determining the proceeding the court shall be bound to conform with the opinion of the assessors.

I beg to submit,

Dr. Hamisi Kigwangalla (MP)
Nzega Constituency

DODOMA, February 7, 2013

**SCHEDULE OF AMMENDMENT TO BE MOVED BY HON. HALIMA MDEE,
MEMBER OF PARLIAMENT - KAPELE CONSTITUENCY DURING THE SECOND
READING OF A BILL TITLED “THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS
AMMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2012”**

Made under S.O. 88(2)

The Bill titled “The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2012” is amended as follows:-

A: By

Deleting the entire Clause 19 as amended.

.....
HALIMA MDEE (MP)

Dodoma

7th February, 2013